**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

-----------

# MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2017/18

**TUME YA MIPANGO**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**JUNI 2017**

## YALIYOMO


SURA YA KWANZA ---------- 5
UTANGULIZI ---------- 5
1.1 Rejea ---------- 5
1.2 Mazingira Yanayoongoza Mpango ---------- 6
1.3 Mpangilio wa Kitabu ---------- 6

SURA YA PILI ---------- 8
HALI YA UCHUMI ---------- 8
2.1. Utangulizi ---------- 8
2.2. Mapititio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2016 ---------- 8
2.2.1. Uchumi wa Dunia ---------- 8
2.2.2. Uchumi wa Afrika na Kanda ---------- 9
2.2.3. Uchumi wa Taifa ---------- 10
2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ---------- 10
2.2.3.2 Mchango wa Kisekta katika Pato la Taifa ---------- 11
2.2.3.3 Wastani wa Pato la kila Mtu ---------- 12
2.2.3.4 Hali ya Upatikanaji wa Chakula Nchini ---------- 12
2.2.3.5 Mfumuko wa Bei ---------- 13
2.2.3.6 Ukuzaji Rasilimali ---------- 14
2.2.3.7 Sekta ya Nje ---------- 15
2.2.3.8 Sekta ya Fedha ---------- 16
2.2.3.9 Thamani ya Shilingi ---------- 17
2.2.3.10 Deni la Taifa ---------- 18
2.3. Idadi ya Watu na Mabadiliko ya Maisha ---------- 18
2.3.1 Ongezeko na Idadi ya Watu ---------- 18
2.3.2 Mabadiliko ya Maisha ---------- 19
2.3.2.1 Upatikanaji wa Huduma Msingi za Kijamii ---------- 19
2.3.2.2 Kasi ya Uhamiaji Mijini ---------- 19
2.3.2.3 Tofauti ya Kipato ---------- 20
2.3.3 Mwenendo na Viashiria vya Umaskini ---------- 20

SURA YA TATU ---------- 23
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO, 2016/17 ---------- 23
3.1. Utangulizi ---------- 23
3.2. Utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo 2016/17 ---------- 23
3.2.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ---------- 23
3.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2016/17 ---------- 24
3.2.2.1 Miradi ya Kielelezo ---------- 24
3.2.2.2 Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda ---------- 28
3.2.2.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Viwanda na Maendeleo ya Watu ---------- 41

3.2.2.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ---------- 51
3.2.2.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango ---------- 73
3.2.2.6 Maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa ---------- 74
3.3. Ushiriki wa Sekta Binafsi ---------- 75
3.3.1. Usaidizi wa Serikali katika Miradi ya Sekta Binafsi ---------- 75
3.3.2. Miradi Inayotekelezwa na Sekta Binafsi ---------- 76
3.3.3. Miradi ya Ubia na Serikali ---------- 77
3.4. Miradi Iliyofuatiliwa na Changamoto za Utekelezaji na Kinga ---------- 77
3.4.1 Miradi Iliyofuatiliwa ---------- 77
3.4.2 Changamoto za utekelezaji na Kinga ---------- 83

SURA YA NNE ---------- 85
VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18 ---------- 85
4.1 Utangulizi ---------- 85
4.3 Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla ---------- 85
4.4 Miradi ya Kipaumbele ---------- 86
4.4.1 Miradi ya Kielelezo ---------- 86
4.4.2 Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda ---------- 90
4.4.3 Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Watu ---------- 98
4.4.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ---------- 111
4.4.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango ---------- 130
4.4.6 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa ---------- 132
4.5 Ushiriki wa Sekta Binafsi ---------- 132
4.5.1 Miradi ya Sekta Binafsi Moja kwa Moja ---------- 132
4.5.2 Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ---------- 133
4.6 Uwekezaji wa Mashirika na Taasisi za Umma ---------- 133

SURA YA TANO ---------- 135
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2017/18 ---------- 135
5.1 Utangulizi ---------- 135
5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2017/18 ---------- 135
5.3 Ugharamiaji wa Mpango ---------- 135
5.3.1 Vyanzo vya Mapato ya Ndani ---------- 135
5.3.2 Vyanzo vya Mapato ya Nje ---------- 136
5.3.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ---------- 136
5.3.4 Uwekezaji wa Mashirika ya Umma ---------- 136
5.3.5 Ugharamiaji Kupitia Taasisi za Fedha za Ndani ---------- 136

SURA YA SITA ---------- 137
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ---------- 137
6.1 Utangulizi ---------- 137
6.2 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango ---------- 137
6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango ---------- 138

SURA YA SABA ---------------------------------------------------------------------------------------- 139
VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA KINGA -------------------------------------- 139
7.1 Utangulizi ---------------------------------------------------------------------------------------- 139
7.2 Vihatarishi katika Kutekeleza Mpango------------------------------------------------------ 139
7.2.1 Vihatarishi vya Nje ---------------------------------------------------------------- 139
7.2.2 Vihatarishi vya ndani.-------------------------------------------------------------- 139
7.3 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi ----------------------------------------------------- 140
7.3.1 Vihatarishi vya Nje ---------------------------------------------------------------- 140
7.3.2 Viharatishi vya Ndani -------------------------------------------------------------- 141

KIAMBATISHO NA. I:MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KUPITIA UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI, MIFUKO YA HIFADHI ZA JAMII NA MASHIRIKA UMMA ------------ 142

KIAMBATISHO NA. II:BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO, 2017/18-------------------------- 151

KIAMBATISHO NA. III:RATIBA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA, 2017/18 ---------------------------------------------------------- 161

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Rejea

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na hivyo unaendelea kutekeleza maeneo manne ya kipaumbele ya: (i) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; (ii) Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na watu; (iii) Mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na (iv) Usimamizi wa utekelezaji. Aidha, lengo kuu la Mpango huu ni kuhakikisha rasilimali na fursa za nchi zinatumika kujenga uchumi wa viwanda na kuboresha maisha ya watanzania.

Katika mwaka 2017/18, Serikali kwa upande wake imetenga Shilingi bilioni 11,999.6, sawa na asilimia 38 ya bajeti ya mwaka 2017/18, ya Shilingi bilioni 31,699.7 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 8,969.8 ni fedha za ndani na bilioni 3,029.8 za nje. Ikilinganishwa na mwaka 2016/17 ambapo bajeti ya maendeleo ilikuwa asilimia 40 ya bajeti yote ya Serikali, asilimia 38 inaweza kuonekana kama ni kidogo, lakini kiuhalisia bajeti ya maendeleo ya Serikali kwa mwaka 2017/18 imeongezeka ikilinganishwa na Shilingi bilioni 11,820.5 mwaka 2016/17. Aidha, msingi wa kutenga asilimia 38, ya bajeti ya maendeleo ni mpangilio wa utekelezaji wa baadhi ya miradi. Miradi kama ya reli ya kati, maeneo maalum ya uwekezaji Bagamoyo na Kurasini, Miradi ya Mchuchuma na Liganga na Bandari ya Bagamoyo itakuwa katika hatua za awali za utekelezaji na hivyo mahitaji halisi ya fedha yanaonekana kuwa yatakuwa chini ya mtiririko wa fedha uliootewa awali. Isitoshe kiasi cha asilimia 38 bado kinakidhi hitajio la Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21, la kutenga kati ya asilimia 30 hadi 40 ya bajeti ya mwaka.

Changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa kwa mwaka 2016/17, ni upatikanaji wa fedha na mtiririko wa mgawanyo katika vipaumbele vingi. Kutokana na hili, msukumo wa kipekee umewekwa katika miradi mahsusi, kwa maana ya ukubwa wa uwekezaji na matokeo tarajiwa kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wenyewe. Miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge); kufufua Shirika la Ndege la Tanzania; uchimbaji wa makaa ya mawe na Ujenzi wa mitambo ya kufua umeme Mchuchuma na kiwanda cha chuma Liganga; ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) mpaka Tanga (Tanzania); ununuzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu; uanzishwaji wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi kimiminika - Lindi; uanzishaji wa Kanda Maalum za Uchumi za Bagamoyo,

Tanga, Kigoma, Ruvuma na Mtwara; uanzishwaji wa Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; kukamilisha ununuzi wa ndege; kusomesha kwa wingi kwenye fani na ujuzi maalum na adimu kuendana na mahitaji ya maendeleo ya viwanda tarajiwa; na uimarishaji wa huduma za jamii na ustawi wa maisha ya watu. Hivyo, kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, kipaumbele cha kwanza cha mgao utakuwa unaelekezwa katika kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa miradi hii na ziada kuelekezwa kwingineko. Ni muhimu kwa hiyo matayarisho ya kuanza kwa miradi hii ikakamilishwa haraka na kwa uhakika.

Kwa ajili ya kuimarisha kasi ya utekelezaji, msukumo pia umewekwa katika kuboresha mpangilio wa utafutaji na ukusanyaji mapato ya Serikali na fedha za maendeleo. Hii ni pamoja na kuimarisha huduma na uwezeshaji wa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Hatua pia zimechukuliwa kuimarisha ushiriki wa Benki za maendeleo nchini kuchangia katika kutafuta na kukopesha fedha kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sanjari na hili hatua za makusudi zitachukuliwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara na hivyo kuinua ushiriki wa sekta binafsi.

## 1.2 Mazingira Yanayoongoza Mpango

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Msukumo wake ni kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano hasa kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea tokea 2016/17.

Utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 umezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Agenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Vile vile, umezingatia mwenendo wa uchumi kitaifa, kikanda na kidunia kwa mwaka 2016 na maoteo kwa mwaka 2017. Umezingatia pia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 na changamoto za utekelezaji zilizojitokeza.

## 1.3 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mpango kimegawanyika katika sura saba (7): Sura ya kwanza ni utangulizi; sura ya pili inaainisha mapitio ya hali ya uchumi wa Dunia, kikanda na Kitaifa kwa mwaka 2016; Sura ya tatu inahusu utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17; Sura ya nne inaainisha maeneo ya kipaumbele kwa 2017/18; Sura ya tano inahusika na ugharamiaji wa Mpango wa 2017/18; Sura ya sita inaainisha mfumo na mpangalio wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ya

utekelezaji; na Sura ya saba inabainisha uwezekano wa vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na kinga zinazoweza kuchukuliwa.

# SURA YA PILI

# HALI YA UCHUMI

## 2.1. Utangulizi

Sura hii inapitia kwa kifupi hali ya uchumi wa Dunia na Kikanda kwa mwaka 2016. Aidha, inabainisha hali ya uchumi kitaifa katika kipindi hicho, ambapo viashiria kama vile Pato la Taifa na ukuaji wa uchumi; pato la kila mtu; hali ya chakula; mfumuko wa bei; idadi ya watu na mabadiliko ya kijamii; mwelekeo wa umaskini; ukuzaji wa mitaji; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Taifa; na mapato na matumizi ya Serikali.

## 2.2. Mapititio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2016

### 2.2.1. Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia iliendelea kupungua kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Kwa mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na ukuaji asilimia 3.2 kwa mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ni matokeo ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea, ambapo kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea kilikuwa asilimia 1.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2015. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma katika masoko mengi duniani, kupungua kwa tija ya uzalishaji kwa baadhi ya shughuli na kushuka kwa kasi ya uwekezaji. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 4.1 kama ilivyokuwa mwaka uliotangulia. Ukuaji huu kwa nchi zinazoendelea ulichangiwa zaidi na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa nchi za China na nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na kuporomoka kwa bei za bidhaa, hasa bidhaa ghafi katika soko la dunia, kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi na kupungua kwa uhitaji wa bidhaa katika masoko mengi duniani. **Jedwali Na. 2.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Dunia kuanzia mwaka 2011 hadi 2016 na matarajio ya mwaka 2017.

**Jedwali 2.1: Ukuaji wa Pato la Dunia (2011-2016) na Matarajio (2017)**

| | Halisi (Asilimia) | | | | | | Matarajio (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
| Dunia | 4.2 | 3.4 | 3.3 | 3.4 | 3.2 | **3.1** | 3.5 |
| Nchi Zilizoendelea | 1.7 | 1.2 | 1.1 | 1.8 | 1.9 | **1.7** | 2.0 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 6.2 | 5.2 | 5.0 | 4.6 | 4.1 | **4.1** | 4.5 |
| Nchi Zinazoibukia Barani Asia | 7.7 | 6.8 | 7.0 | 6.8 | 6.6 | **6.4** | 6.4 |
| Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara | 5.0 | 4.2 | 5.2 | 5.1 | 3.4 | **1.4** | 2.6 |
| Tanzania | 7.9 | 5.1 | 7.3 | 7.0 | 7.0 | **7.0** | 7.2 |
| Kenya | 6.1 | 4.5 | 5.7 | 5.3 | 5.6 | **6.0** | 5.3 |
| Uganda | 6.8 | 2.6 | 3.9 | 4.9 | 5.0 | **4.7** | 5.0 |
| Rwanda | 7.5 | 8.8 | 4.7 | 7.0 | 6.9 | **5.9** | 6.1 |

| | Halisi (Asilimia) | | | | | | Matarajio (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
| Burundi | 4.2 | 4.0 | 4.5 | 4.7 | -4.1 | **-1.0** | 0.0 |

**Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa, Januari, 2017

Kwa mwaka 2017 uchumi wa Dunia unatarajiwa kuimarika hususan kwa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea. Hata hivyo, sera na hatua za Serikali mpya ya Marekani, kujitoa kwa Uingereza katika Umoja wa Ulaya na hali ya amani na usalama katika maeneo mbalimbali Duniani zinaweza kuwa na athari katika mwenendo wa uchumi wa Dunia ijapokuwa kwa sasa ni vigumu kutabirika.

Kwa upande mwingine Shirika hilo limethibitisha kuwa, mfumuko wa bei duniani katika mwaka 2016 uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 2.9 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2015. Mfumuko uliongezeka kutokana na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha za ndani kwa baadhi ya nchi na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa ya *La Nina* na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo, hasa ya chakula. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka kufikia asilimia 0.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.3 mwaka 2015. Kwa upande wa nchi zinazoendelea, za Asia, uliongezeka hadi asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2015, na kwa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ulifikia asilimia 11.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 ilivyokuwa mwaka 2015.

### 2.2.2. Uchumi wa Afrika na Kanda

Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi asilimia 1.4 mwaka 2016, hasa kutokana na changamoto za upatikanaji wa mikopo kutoka masoko ya kimataifa na hivyo kushindwa kutekeleza miradi iliyopangwa katika kipindi hicho, kuendelea kwa migogoro ya kisiasa kwa baadhi ya nchi (Burundi, Libya, Chad, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), na kuporomoka kwa bei za mazao ghafi, hususan, dhahabu na mafuta ya petroli.

Kasi ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilishuka kutoka asilimia 6.5 mwaka 2015 hadi asilimia 5.3 mwaka 2016 ijapokuwa Jumuiya hii iliendelea kuongoza kwa ukuaji miongoni mwa Jumuiya mbalimbali za Afrika. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi katika Jumuiya hii kulichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei za bidhaa na kudorora kwa uchumi wa dunia. Maoteo ya mwenendo wa uchumi katika ukanda huu yanaonesha utakua kwa asilimia 5.7 mwaka 2017 na 6.0 mwaka 2018. Matarajio haya yanazingatia hatua zinazochukuliwa na nchi za ukanda wa Afrika Mashariki katika kuboresha mazingira ya uwekezaji katika uzalishaji na uendeshaji biashara kama vile kuwa na maeneo tengefu ya ujenzi wa viwanda (industrial parks), hususan, vya nguo, bidhaa za ngozi, kilimo, madawa na vifaa tiba.

Mfumuko wa bei katika nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2016 uliendelea kuwa wa kiwango cha tarakimu moja, ambapo Rwanda ilikuwa na asilimia 7.1, Uganda asilimia 5.4, Tanzania asilimia 5.2, Kenya asilimia 6.3 na Burundi asilimia 5.6. Aidha, kufikia Machi 2017, mfumuko wa bei kwa nchi hizi ulipanda, ambapo kwa Burundi ulifikia asilimia 21.10, Rwanda asilimia 13.0; Kenya asilimia 10.28; Uganda asilimia 6.4 na Tanzania asilimia 6.4. Hali hii ilichangiwa na ukame katika maeneo mengi ya ukanda huu kutokana na kuchelewa kwa msimu wa mvua.

Kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, yaani SADC, kasi ya ukuaji wa uchumi ilishuka kutoka asilimia 1.9 mwaka 2015 hadi asilimia 1.1 mwaka 2016. Kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya hii kulichangiwa na uhaba wa nishati ya umeme pamoja na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa ya La Nina. Pamoja na kasi ya kushuka kwa ukuaji, Jumuiya hii iliendelea kuwa ya tatu kwa ukuaji miongoni mwa Jumuiya za barani Afrika na uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 1.4 mwaka 2017. Mfumuko wa bei uliongezeka hadi kufikia asilimia 10.5 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2015. Makadirio haya yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na ukame; utekelezaji usioridhisha wa sera za mapato na matumizi pamoja na sera za fedha. Matarajio ni kuwa mfumuko wa bei utapungua kufikia asilimia 8.7 mwaka 2017 kutokana na kushuka kwa gharama za bidhaa, bei ya mafuta na uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme; na kuimarika kwa hali ya hewa.

### 2.2.3. Uchumi wa Taifa

#### 2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Pato la Taifa kwa mwaka 2016 lilikua kwa wastani wa asilimia 7.0, kama ilivyokuwa mwaka 2015. Kiwango hiki ni chini ya maoteo ya kufikia asilimia 7.2 kutokana na ukuaji wa baadhi ya shughuli kushindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji. Baadhi ya shughuli za kiuchumi ambazo zilishindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji ni pamoja na: sekta ya kilimo iliyokua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 2.9; biashara na matengenezo asilimia 6.7 dhidi ya asilimia 7.8; huduma za malazi na chakula asilimia 3.7 kinyume na maoteo ya asilimia 8.0; na huduma za utawala asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 6.3. Pamoja na hayo, zipo shughuli za kiuchumi zilizokua na hata kuzidi maoteo. Baadhi ya shughuli za uchumi zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: ujenzi (asilimia 13.0); habari na mawasiliano (asilimia 13.0); usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8); uchimbaji madini na mawe (asilimia 11.5); na shughuli za fedha na bima (asilimia 10.7). **Jedwali Na. 2.2** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi mwaka 2010 hadi 2016.

**Jedwali Na. 2.2: Ukuaji wa Shughuli Mbalimbali za Kiuchumi Mwaka 2010 hadi 2016**

| Shughuli za Kiuchumi | Ukuaji (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** |
| Kilimo | 2.7 | 3.5 | 3.2 | 3.2 | 3.4 | 2.3 | 2.1 |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 7.3 | 6.3 | 6.7 | 3.9 | 9.4 | 9.1 | 11.5 |
| Uzalishaji Viwandani | 8.9 | 6.9 | 4.1 | 6.5 | 6.8 | 6.5 | 7.8 |
| Umeme | 13.4 | -4.3 | 3.3 | 13.0 | 9.3 | 5.8 | 8.5 |
| Usambazaji Maji Safi na Udhibiti Maji taka | 2.2 | -1.2 | 2.8 | 2.7 | 3.7 | 0.1 | 4.3 |
| Ujenzi | 10.3 | 22.9 | 3.2 | 14.6 | 14.1 | 16.8 | 13.0 |
| Biashara na Matengenezo | 10.0 | 11.3 | 3.8 | 4.5 | 10.0 | 7.8 | 6.7 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 3.7 | 4.1 | 6.7 | 2.8 | 2.2 | 2.3 | 3.7 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 10.7 | 4.4 | 4.2 | 12.2 | 12.5 | 7.9 | 11.8 |
| Habari na Mawasiliano | 24.4 | 8.6 | 22.2 | 13.3 | 8.0 | 12.1 | 13.0 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 12.6 | 14.8 | 5.1 | 6.2 | 10.8 | 11.8 | 10.7 |
| Sughuli za kitaaluma, Kisayansi na Kiufundi | 29.9 | 4.8 | -5.8 | 5.4 | 0.5 | 6.8 | 6.3 |
| Utawala na Ulinzi | 8.6 | 5.1 | 23.8 | 12.2 | 6.0 | 4.7 | 6.7 |
| Upangishaji Nyumba | 1.8 | 1.9 | 2.0 | 2.1 | 2.2 | 2.2 | 2.4 |
| Elimu | 6.4 | 5.6 | 7.4 | 4.3 | 4.8 | 6.3 | 8.1 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 3.3 | 5.3 | 11.4 | 8.8 | 8.1 | 4.7 | 5.2 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 5.6 | 5.8 | 6.6 | 5.6 | 5.8 | 6.0 | 7.2 |
| **Pato la Taifa** | **6.4** | **7.9** | **5.1** | **7.3** | **7.0** | **7.0** | **7.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2017

Jedwali Na. 2.2 vile vile, linaonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani ukiwa ni asilimia 7.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na 6.5 mwaka 2015. Hali hii imechangiwa na msukumo wa Serikali katika kuimarisha uzalishaji wa nishati ya umeme na usambazaji huduma za maji nchini. Kwa ujumla sekta ya viwanda nchini imeendelea kuonesha mwenendo wa kuimarika sawa na msisitizo wa Mpango wa Pili wa maendeleo. Kuimarika kwa ukuaji wa uzalishaji viwandani kunaakisi hatua thabiti za maboresho ya mazingira na uendeshaji biashara zimeendelea kuchukuliwa kuakisi azma ya nchi. Japo kumekuwa na hatua za kuimarika kwa viashiria vya mazingira ya biashara nchini bado ipo haja ya kuimarisha zaidi uwianifu wa sera, sheria, taratibu na mfumo taasisi.

### 2.2.3.2 Mchango wa Kisekta katika Pato la Taifa

Mchango wa shughuli za kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2015. Shughuli za viwanda na ujenzi zilichangia asilimia 25.2 ya Pato la Taifa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 24.3 mwaka 2015, ambapo mchango wa sekta za huduma (ikijumuisha biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha na bima, upangishaji majumba, elimu na afya) ulikuwa asilimia 39.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 40.0 mwaka 2015. **Jedwali Na. 2.3** linaonesha mchango wa kisekta katika Pato la Taifa mwaka 2010 hadi 2016.

**Jedwali Na. 2.3: Mchango wa Kisekta katika Pato la Taifa Mwaka 2010 hadi 2016.**

| | Mchango (Asilimia) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli za Kiuchumi** | **2010** | **2011** | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** |
| **Kilimo** | **29.9** | **29.4** | **31.1** | **31.2** | **28.8** | **29.0** | **29.1** |
| Mazao | 16.6 | 16.5 | 18.0 | 17.5 | 16.1 | 15.6 | 15.5 |
| Mifugo | 9.1 | 8.7 | 8.5 | 8.2 | 7.3 | 7.9 | 7.7 |
| Misitu | 2.2 | 2.2 | 2.5 | 3.1 | 3.1 | 3.5 | 3.9 |
| Uvuvi | 2.1 | 2.1 | 2.2 | 2.4 | 2.2 | 2.1 | 2.0 |
| **Viwanda na Ujenzi** | **20.3** | **22.8** | **21.8** | **22.7** | **23.2** | **24.3** | **25.2** |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 4.1 | 5.1 | 4.9 | 4.2 | 3.7 | 4.0 | 4.8 |
| Uzalishaji Viwandani | 6.9 | 7.6 | 7.5 | 6.4 | 5.6 | 5.2 | 5.1 |
| Usambazaji Umeme | 0.9 | 0.6 | 0.9 | 0.8 | 1.1 | 1.0 | 0.9 |
| Usambazaji Maji Safi na Udhibiti Maji taka | 0.6 | 0.5 | 0.4 | 0.5 | 0.5 | 0.4 | 0.4 |
| Ujenzi | 7.8 | 9.0 | 8.1 | 10.8 | 12.4 | 13.6 | 14.0 |
| **Huduma** | **44.2** | **42.7** | **41.9** | **41.0** | **40.9** | **40.0** | **39.1** |
| Biashara na Matengenezo | 10.1 | 10.6 | 10.4 | 10.2 | 10.5 | 10.7 | 10.7 |
| Usafirishaji na Uhifadhi mizigo | 5.8 | 5.2 | 4.4 | 4.2 | 4.3 | 4.3 | 4.3 |
| Malazi na Huduma ya chakula | 1.6 | 1.4 | 1.4 | 1.3 | 1.1 | 1.1 | 1.0 |
| Habari na Mawasiliano | 2.6 | 2.4 | 2.4 | 2.3 | 2.1 | 2.0 | 2.0 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 3.2 | 3.4 | 3.4 | 3.3 | 3.4 | 3.6 | 3.6 |
| Upangishaji Nyumba | 4.6 | 4.3 | 4.3 | 3.8 | 3.7 | 3.2 | 3.0 |
| Sughuli za kitaaluma, Kisayansi na Kiufundi | 1.7 | 1.5 | 1.3 | 1.3 | 1.3 | 1.2 | 1.2 |
| Utawala na Ulinzi | 6.1 | 6.3 | 6.5 | 7.0 | 6.6 | 6.4 | 6.3 |
| Elimu | 3.1 | 2.8 | 2.6 | 2.7 | 2.7 | 2.5 | 2.3 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1.7 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.7 |
| **Pato la Taifa** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

### 2.2.3.3 Wastani wa Pato la kila Mtu

Pato la Taifa kwa mwaka 2016 lilifikia Shilingi milioni 103,744,606 (kwa bei za mwaka husika). Kiasi hiki cha Pato kikigawiwa kwa idadi ya watu wanaokadiriwa kuwepo Tanzania Bara, ya watu 48,676,698, inafanya wastani wa Pato la kila mtu kufikia Shilingi 2,131,299 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 1,918,897 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hata hivyo, katika thamani ya Dola za Marekani, wastani wa Pato la kila mtu liliongezeka kidogo kutoka Dola 967.5 mwaka 2015 hadi Dola 979.1 mwaka 2016, kumaanisha kuwa bado tuna safari ndefu ya kuingia katika kundi la uchumi wa kati. Kiwango cha chini cha uchumi wa kati ni kufikia Dola 1,043. Hivyo basi, kasi ya ongezeko la Pato la mwananchi katika thamani ya Dola haina budi kuongezeka. Hii itawezekana kwa kutanzua changamoto mbili: kwanza, kuongeza mauzo na thamani ya mauzo nje ya nchi sambamba na kupunguza uagizaji kutoka nje; na pili, kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu nchini.

### 2.2.3.4 Hali ya Upatikanaji wa Chakula Nchini

Kiwango cha upatikanaji wa chakula nchini hujumuisha kile kilichohifadhiwa katika maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, maghala ya wafanyabiashara binafsi na kile kilichohifadhiwa katika kaya. Katika kipindi kinachoishia Machi 2017,

kiwango cha nafaka kilichokuwa katika maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kilikuwa tani 86,444[1] ikilinganishwa na kiwango cha tani 68,727 cha Machi 2016. Serikali imeendelea kutoa chakula kusaidia maeneo yenye upungufu nchini kukabiliana na madhara ya ukame uliojitokeza.


Katika kipindi cha mwaka kinachoishia Machi 2017, bei za mazao karibu yote ya chakula iliongezeka, isipokuwa mchele. Ongezeko hili lilitokana na taharuki ya hali ya hewa, upungufu wa vyakula katika maeneo mbalimbali nchini na baadhi ya wafanyabishara kuanza kuzuia mazao katika maghala kwa matarajio ya kuongezeka kwa bei na hivyo kujipatia faida kubwa. Hata hivyo upungufu uliotokea katika masoko ulikuwa mdogo ikilinganishwa na kipindi kilichopita hivyo haukuathiri hali ya upatikanaji wa chakula nchini. Serikali imeendelea kusisitiza wananchi kulima mazao ya muda mfupi na yanayohimili ukame ili kukabiliana na tishio la upungufu wa mvua nchini. Aidha, msukumo umeendelea kuwekwa katika kujenga hifadhi ya chakula kitaifa. Hili ni hitajio la msingi katika ujenzi wa uchumi wa viwanda unaohitaji "specialization". Aidha, uhakika wa upatikanaji wa chakula na nafuu ya bei ni masuala ya msingi katika kuimarisha uchumi kwa jumla na gharama za uzalishaji viwandani, hasa mishahara.

### 2.2.3.5 Mfumuko wa Bei

Katika mwaka 2016, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2015. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 6.5 Januari 2016 hadi asilimia 5.5 Juni 2016. Aidha, mfumuko wa bei uliendelea kupungua zaidi hadi asilimia 5.0 Desemba 2016. Hadi Machi 2017 mfumuko wa bei uliongezeka kidogo kufikia asilimia 6.4 na kuendelea kubaki asilimia 6.4 Aprili 2017. Kuimarika kwa mwenendo wa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na: mwenendo wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na ndani ya nchi; kuimarika kwa bei za vyakula nchini; na kuwepo kwa sera madhubuti za usimamizi wa bajeti na fedha. Matarajio ni kubaki na mfumuko wa bei katika kiwango cha tarakimu moja kutokana na matarajio ya uzalishaji mzuri wa chakula na kuimarika kwa sera za usimamizi wa fedha na bajeti. **Kielelezo Na. 2.1** kinaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Machi 2017 ambapo kiwango cha juu kilikuwa asilimia 6.5 Januari 2016 na kiwango cha chini kilikuwa asilimia 4.5 kwa kipindi cha Septemba hadi Oktoba 2016.

[1] Kiwango hiki hakijumuishi kiasi cha chakula kilichohifadhiwa katika maghala ya wafanyabiashara binafsi, ambacho kwa kawaida huchukua sehemu kubwa zaidi ya chakula kilichopo nchini.

**Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2016 – Machi 2017)**




**Chanzo**: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Machi, 2017

Mfumuko wa bei katika nchi za Afrika Mashariki uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja katika mwaka 2016 ambapo wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi za Rwanda ulikuwa asilimia 7.1, Uganda asilimia 5.4, Tanzania asilimia 5.2, Kenya asilimia 6.3 na Burundi asilimia 5.6. Aidha, kwa mwezi Machi 2017, mfumuko wa bei ulikuwa mkubwa zaidi kwa nchi zote kama ifuatavyo: Burundi asilimia 21.10, Rwanda asilimia 13.0; Kenya asilimia 10.28; Uganda asilimia 6.4 na Tanzania asilimia 6.4. **Jedwali Na. 2.4** linaonesha mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Machi 2017.

**Jedwali Na. 2.4: Mfumuko wa Bei katika nchi za Afrika Mashariki, Januari 2016 hadi Machi 2017.**

| Nchi | Jan '16 | Feb '16 | Mac '16 | Apr '16 | Mei '16 | Jun '16 | Jul '16 | Ago '16 | Sept '16 | Okt '16 | Nov '16 | Des '16 | Jan '17 | Feb '17 | Mac '17 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tanzania | 6.5 | 5.6 | 5.4 | 5.1 | 5.2 | 5.5 | 5.1 | 4.9 | 4.5 | 4.5 | 4.8 | 5.0 | 5.2 | 5.5 | 6.4 |
| Kenya | 7.8 | 6.8 | 6.5 | 5.3 | 5.0 | 5.8 | 6.4 | 6.3 | 6.3 | 6.5 | 6.7 | 6.4 | 6.99 | 9.04 | 10.28 |
| Uganda | 7.3 | 6.9 | 6.2 | 5.0 | 5.3 | 5.9 | 5.1 | 4.8 | 4.2 | 4.1 | 4.6 | 5.7 | 5.9 | 6.7 | 6.4 |
| Burundi | 6.3 | 6.7 | 4.3 | 2.6 | 2.7 | 3.9 | 3.9 | 6.6 | 7.0 | 6.0 | 7.1 | 9.6 | 12.9 | 20.9 | 21.10 |
| Rwanda | 6.6 | 6.1 | 5.8 | 4.4 | 4.4 | 6.3 | 7.8 | 7.5 | 7.4 | 9.1 | 9.1 | 11.0 | 12.0 | 13.4 | 13.0 |

**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

### 2.2.3.6 Ukuzaji Rasilimali

Ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 3.4 kutoka shilingi milioni 24,717,206 mwaka 2015 kufikia Shilingi milioni 25,558,140 mwaka 2016. Hata hivyo, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulipungua na kuwa asilimia 24.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 27.2 mwaka 2015. Ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 ulipungua kwa asilimia 4.3

kutoka Shilingi milioni 13,733,585 mwaka 2015 kufikia Shilingi milioni 13,140,451 mwaka 2016.

### 2.2.3.7 Sekta ya Nje

### (a) Mauzo ya Bidhaa na Huduma

Katika mwaka 2016, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma kati ya Tanzania na nchi mbalimbali uliendelea vizuri. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 na kufikia dola za Marekani milioni 9,285.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola milioni 8,918.1 mwaka 2015. Aidha, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje kwa mwaka 2016 ilipungua kwa asilimia 14.0 kutoka Dola za Marekani milioni 12,528.2 mwaka 2015 na kufikia dola za Marekani milioni 10,772.3. Mwenendo huo ulitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje isipokuwa malighafi za viwandani, sambamba na kupungua kwa malipo ya usafirishaji, huduma za kiserikali, na huduma za biashara nyingine.

Katika mwaka 2016, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 1,489.5 ikilinganishwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 3,594.7 mwaka 2015, sawa na kupunguza nakisi kwa asilimia 58.6. Hali hii kwa kiasi kikubwa, ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kupungua kwa uagizaji bidhaa nje ya nchi. Kufuatia hili, urari wa malipo yote, kwa mwaka 2016, ukijumuisha urari wa biashara ya bidhaa na huduma, mapato ya vitega uchumi, uhamisho wa mali, malipo ya kawaida, uhamisho wa mitaji na malipo ya fedha katika uwekezaji ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 199.1 mwaka 2015. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za usafirishaji na usafiri na biashara ya utalii sambamba na kupungua kwa malipo ya usafirishaji kufuatia kupungua kwa gharama za uagizaji bidhaa kutoka nje.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2017, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilikuwa Dola za Marekani milioni 2,224.8. Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia, huduma za utalii, dhahabu, bidhaa za mboga mboga na matunda. Thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ilikuwa Dola za Marekani milioni 2,203.6.

### (b) Akiba ya Fedha za Kigeni

Hadi kufikia Desemba 2016, Akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani milioni 4,325.6 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 4,093.7 Desemba 2015. Kiasi hicho kilikuwa kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.2. Kiwango hiki ni zaidi ya kiwango cha chini kilichowekwa katika hatua za mtangamano wa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki cha angalau miezi 4.0. Kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni kulichangiwa zaidi na kuendelea kuongezeka

kwa rasilimali za kigeni katika benki za kibiashara. Kufikia Machi 2017, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,482.6, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.3.

#### 2.2.3.8 Sekta ya Fedha

**(a) Ujazi wa Fedha na Karadha**

Katika mwaka 2016, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 22,760.4 kutoka shilingi bilioni 22,115.3 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Ukuaji huu ulikuwa chini ya kiwango cha ukuaji wa asilimia 18.8 cha mwaka 2015. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye mabenki na mikopo kwa sekta binafsi na Serikali kuu. Kupungua kwa mikopo kwa Serikali kuu kulitokana na kuongezeka kwa mapato ya Serikali pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya Serikali. Aidha, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kumechangiwa na tahadhari zinazoendelea kuchukuliwa na mabenki katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu.

**(b) Mwenendo wa Mikopo ya Benki Kishughuli**

Mikopo ya mabenki kwa sekta binafsi kwa mwaka 2016 ilikua kwa asilimia 7.2 kufikia Shilingi bilioni 16,608.9 kutoka Shilingi bilioni 15,492.7 mwaka 2015. Ukuaji huu ulikuwa chini ya ukuaji wa mwaka 2015 wa asilimia 24.8 na kufikia wastani wa asilimia 16.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 17.1 mwaka 2015. Ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za uzalishaji katika kilimo, uchukuzi na mawasiliano, viwanda, huduma za kifedha, umeme, majengo na ujenzi ulipungua kwa kasi zaidi mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. Mikopo kwa shughuli za madini na uchimbaji mawe, biashara, utalii, hoteli na migahawa na shughuli binafsi iliimarika, japo kwa kasi ndogo, ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Sehemu kubwa ya mikopo hiyo ilielekezwa katika shughuli za biashara, zikipata wastani wa asilimia 21 ya mikopo yote na kufuatiwa na shughuli binafsi zilizokuwa na asilimia 18.6. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa ukwasi katika mabenki kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ubora hafifu wa rasilimali za baadhi ya mabenki ambao ulipelekea mabenki hayo kuchukua tahadhari kwa kuongeza kiasi wanachotenga kwa ajili ya mikopo chechefu (NPLs) na kupunguza maoteo ya faida.

Katika kipindi cha Januari 2017 hadi Machi 2017, utoaji wa mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi uliendelea kuimarika ambapo uliongezeka kwa shilingi bilioni 77.4 na kufikia shilingi bilioni 16,686.30. Hivyo, zimeanza kujitokeza ishara njema za ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi hususan katika shughuli za uzalishaji viwandani, mikopo binafsi na mikopo katika sekta za mahoteli na mighahawa. Hii ni chachu kwa uwekezaji wa sekta binafsi nchini na ukuaji wa uchumi.

### (c) Mwenendo wa Viwango vya Riba


Katika mwaka 2016 viwango vya riba za amana na za mikopo vilipungua ikilinganishwa na viwango hivyo mwaka uliotangulia. Riba za amana za muda maalum zilipungua kutoka wastani wa asilimia 9.30 hadi wastani wa asilimia 8.78. Viwango vya riba za amana za mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.16 mwaka 2015 hadi asilimia 11.03 mwaka 2016. Vile vile, viwango vya riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.22 kufikia asilimia 12.87 mwaka 2016. Mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki. Kufuatia hali hiyo, tofauti kati ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kufikia asilimia 1.83 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 3.06 mwaka 2015. Hata hivyo, riba katika soko la fedha baina ya benki iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 13.49 mwezi Desemba 2016 kutoka asilimia 7.29 muda kama huo mwaka 2015. Riba kwenye dhamana za Serikali ilipungua kutoka asilimia 18.25 mwezi Desemba 2015 kufikia wastani wa asilimia 15.12 mwezi Desemba 2016.

Hadi kufikia Machi 2017, riba za amana za muda maalum ziliongezeka kidogo hadi asilimia 10.85; riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka hadi asilimia 12.03; na riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja ziliongezeka hadi asilimia 18.07. Kuongezeka kwa riba za mikopo kunatokana na mabenki kuchukua tahadhari kwa kuongeza kiasi wanachotenga kwa ajili ya mikopo chechefu na kupunguza maoteo ya faida, ilihali kuongezeka kwa riba za amana kulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki kutafuta amana kutoka kwa wateja. Hata hivyo, riba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 8.16 na riba kwenye dhamana za Serikali ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 14.52. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa ukwasi katika mabenki kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu.

### 2.2.3.9 Thamani ya Shilingi

Thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani imeendelea kupungua thamani kwa wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.8 mwaka 2015. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa Shilingi 2,177.07 mwaka 2016 ikilinganishwa na Shilingi 1,985.39 mwaka 2015. Aidha, mwishoni mwa mwaka 2016, Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa Shilingi 2,172.6 ikilinganishwa na Shilingi 2,148.5 mwishoni mwa mwaka 2015. Hadi kufikia Machi 2017, Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,223.9. Hii ilitokana na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti. **Kielelezo Na. 2.2** kinaonesha mwenendo wa thamani ya Shilingi kati ya Machi 2016 na Machi 2017.

**Kielelezo Na. 2.2: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, Machi 2016 – Machi 2017**




**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania, 2017

### 2.2.3.10 Deni la Taifa

Hadi Machi 2017, Deni la Taifa lilifikia Shilingi bilioni 50,806.5 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 45,867.8 Machi, 2016, sawa na ongezeko la asilimia 10.8 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho deni la Serikali ni Shilingi bilioni 42,883.6 na deni la sekta binafsi ni Shilingi bilioni 7,922.9. Deni la Serikali limeongezeka kwa asilimia 9.2 kutoka Shilingi bilioni 39,274.6 Machi, 2016 hadi Shilingi bilioni 42,883.6 Machi, 2017. Kati ya deni la Serikali, deni la ndani ni Shilingi bilioni 12,073.7 sawa na asimilia 28.1 na deni la nje ni Shilingi bilioni 30,809.9 sawa na asilimia 71.9. Ongezeko la Deni la Serikali lilitokana na mikopo mipya kutoka vyanzo vya masharti nafuu na ya kibiashara, malimbikizo ya riba ya deni la nje kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo zinazotakiwa kutoa msamaha wa madeni lakini bado hazijatoa pamoja na kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola za Marekani. Fedha za mikopo hiyo zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo hususan katika sekta za ujenzi (barabara), nishati, uchukuzi, elimu na maji.

## 2.3. Idadi ya Watu na Mabadiliko ya Maisha

### 2.3.1 Ongezeko na Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.7 kwa mwaka, ambapo kufikia mwaka 2016 ilikadiriwa kuwa na watu 48,676,698. Kwa makadirio haya, Tanzania Bara inakuwa ni nchi ya tano kwa idadi ya watu Barani Afrika, ikitanguliwa na nchi nne (4) ambazo ni Nigeria, Ethiopia, Misri na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Idadi kubwa ya watu na kasi ya ongezeko imekuwa ni changamoto kubwa katika harakati za kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma. Kwa kuzingatia hali hii, Serikali

imeendelea kutekeleza sera zinazolenga kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu, hasa kwa kuongeza na kuboresha upatikanaji wa elimu msingi hususan kwa wasichana. Aidha, idadi kubwa ya watu kwa upande mwingine ni fursa pia kwa maana ya soko la bidhaa na huduma.

### 2.3.2 Mabadiliko ya Maisha

#### 2.3.2.1 Upatikanaji wa Huduma Msingi za Kijamii

Upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii umeonekana kuchangia kasi ya kupunguza umaskini. Zipo juhudi mbalimbali zinazochukuliwa kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma, hususan za afya kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamiii. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania 2015/16, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka watoto 51 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi kufika watoto 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16. Vile vile, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka watoto 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi watoto 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16. Masuala mengine yanayoonekana kuwa na matokeo mazuri kwa jamii katika kinga za afya ni pamoja na usafi wa mazingira, upatikanaji wa maji safi na salama, na pia nyumba na makazi bora. Hivyo, mkakati wa makusudi utaendelea kutekelezwa kuboresha maeneo haya muhimu kwa ustawi wa jamii.

#### 2.3.2.2 Kasi ya Uhamiaji Mijini


Kumekuwa na kasi kubwa ya uhamiaji mijini. Asilimia 30 ya idadi ya watu nchini kwa sasa wanaishi mijini. Kasi hii ya mabadiliko ya idadi ya watu na uhamiaji ni changamoto hasa katika utoaji wa huduma. Serikali imeendelea kuboresha huduma za jamii ili ziendane na ongezeko kubwa la ukuaji wa idadi ya watu nchini. Kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kutekeleza sera zitakazopunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu hasa kwa kuongeza na kuboresha huduma za uzazi wa mpango hususan kwa maeneo ya vijijini. Elimu na muda wa wasichana kukaa masomoni imeonekana kuwa na ufanisi mkubwa zaidi katika suala hili. Wasichana na akina mama waliosoma licha ya kuchelewa kuanza kuzaa wanatumia uzazi wa mpango na hivyo kuwa na wastani mdogo wa uzazi/watoto. Katika jitihada za kupunguza ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohama kutoka vijijini kwenda mijini, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu, afya, na upatikanaji wa maji, umeme na barabara vijijini. Aidha, hatua zinaendelea kuchukuliwa kuimarisha uzalishaji, tija na faida kwa shughuli za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo, masoko, miundombinu ya umwagiliaji, na kuondoa utitiri wa kodi katika shughuli za kilimo. Hatua pia zinachukuliwa kupanua shughuli zisizo za kilimo vijijini, ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa shughuli za viwanda na biashara.

### 2.3.2.3 Tofauti ya Kipato

Kipimo cha mgawanyo wa kipato miongoni mwa wananchi (Gini coefficient) kwa upande wa Tanzania Bara kinaonesha kuwa tofauti ya kipato imepungua kutoka 0.37 mwaka 2006/7 hadi 0.34 mwaka 2011/12. Hata hivyo, imedhihirika kuwa tofauti ya kipato ni kubwa zaidi kati ya jiji la Dar es Salaam na maeneo ya miji mingine ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Hali hii imechangiwa na tofauti ya upatikanaji wa huduma, miundombinu, fursa za ajira, athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi katika shughuli msingi za jamii husika.

Kwa kuzingatia haya, Serikali imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, afya, maji, kilimo, umeme, barabara na huduma za mpango wa uzazi hususan, kwa maeneo ya vijijini. Aidha, kumekuwa na mwitikio mzuri wa wananchi katika ujenzi na hifadhi ya maeneo ya makazi. Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza kasi ya kuwaletea wananchi maendeleo na usawa wa kipato. **Kielelezo Na. 2.3** kinaonesha tofauti ya kipato kwa maeneo mbalimbali nchini.

**Kielelezo Na. 2.3: Tofauti ya Kipato (Gini Coefficient) kwa Maeneo Mbalimbali Nchini**




**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango, 2012


### 2.3.3 Mwenendo na Viashiria vya Umaskini

Kutokana na utekelezaji madhubuti wa mipango na sera za Serikali zinazolenga kuboresha maisha ya watu, idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini imeendelea kupungua. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2012, umaskini umepungua kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi asilimia 28.2 mwaka 2012. Hii ni sawa na kupungua kwa asilimia 10.8 katika kipindi cha miaka 20 (1992 hadi 2012). Shabaha ya Serikali ni kupunguza kiwango cha umaskini kufikia asilimia 16.7 mwaka 2020 na asilimia 12.7 mwaka 2025. Pamoja na

kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa idadi ya Watanzania wanaokosa mlo kwa siku au kuishi kwa mlo mmoja inapungua kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 9.7 na kufikia asilimia 5.7 na asilimia 4.4 kwa mwaka 2020 na 2025 kwa mtiririko huo. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na: kuimarisha uzalishaji na tija katika kaya; kuongeza fursa za ajira mijini na vijijini; mpango wa kusaidia kaya maskini; kutoa mikopo nafuu kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Mfuko wa SELF.


Taarifa ya Utafiti rejewa inaonesha kuwa umaskini vijijini umepungua kutoka asilimia 39.4 mwaka 2007 hadi asilimia 33.3 mwaka 2012 ikimaanisha kuwa umaskini umepungua lakini chini ya wastani wa kitaifa. Mantiki yake ni kuwa matokeo ya kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi imelikwepa kundi kubwa la wananchi wa vijijini, ambao wengi wao hutegemea shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi. Sekta hizi zimekuwa na tija na kasi ndogo ya ukuaji kwa kipindi chote. Matokeo yake ni kuwa wakulima na wafugaji wameshindwa kufaidika na mafanikio ya ukuaji wa uchumi. Taarifa ya Hali ya Umaskini katika ngazi za Mikoa na Wilaya (Poverty Mapping) ya mwaka 2016 inaonesha kuwa hali ya umaskini kwa baadhi ya Wilaya ni kubwa kati ya kiwango cha asilimia 50.2 hadi asilimia 62.8. Shabaha ya Serikali ni kupunguza wastani wa umaskini vijijini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 33.3 hadi kufikia asilimia 19.7 na 15 mwaka 2020 na mwaka 2025 kwa mtiririko huo. **Kielelezo Na. 2.4** (a) - (b) kinaonesha mwenendo wa viashiria vya umaskini nchini.

**Kielelezo Na. 2.4(a): Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini Nchini, Umaskini wa Chakula**




**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**Kielelezo Na. 2.4(b): Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini Nchini, Umaskini wa Mahitaji ya Msingi**




**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

Kwa kadiri ya tathmni, maeneo yaliyo na ajira mbadala zaidi ya kilimo, upatikanaji wa uhakika wa miundombinu na huduma za jamii, na kilimo cha umwagiliaji yamepunguza umaskini kwa kasi na uendelevu. Hivyo, pana haja ya kuwa na mkakati wa makusudi wa kuchochea ukuaji na mabadiliko ya uchumi hususan kuongeza tija na thamani katika uzalishaji na shughuli ambazo zinaajiri watu wengi, hasa wa vijijini. Kilimo na mabadiliko ya uchumi wa kijijini sharti upewe msukumo zaidi. Wananchi na jamii hawana budi kuelimishwa faida za kujikita (specialize) katika uzalishaji au shughuli maalum. Uchafuzi wa mazingira na kasi ya mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa katika sekta ya kilimo na ustawi wa jamii. Pana haja ya kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya hifadhi na uvunaji wa maji ya mvua na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Hifadhi za mazingira, hasa matumizi endelevu ya misitu na maeneo oevu, hazina budi kupewa msukumo stahiki. Sheria na miundo ya Serikali za Mitaa na Vijiji inapaswa kupitiwa kwa lengo la kuweka wajibu wa kuhifadhi, kulinda na kuendeleza mazingira na usafi. Yote haya yatachangia kwa kiwango kikubwa juhudi za kupunguza umaskini.

Kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya umaskini kati ya mwaka 2007 na mwaka 2012 na juhudi dhahiri za Serikali katika kuinua tija na uzalishaji katika sekta za kilimo na kuongeza ajira mbadala katika sekta za viwanda, biashara na huduma, kuna matarajio makubwa kwamba viwango vya umaskini vitapungua. Serikali inategemea kupata takwimu mpya za hali ya umaskini nchini baada ya Utafiti wa Hali ya Kipato na Matumizi ya Kaya Binafsi, unatarajiwa kufanyika mwaka ujao wa fedha.

## SURA YA TATU

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO, 2016/17

### 3.1. Utangulizi

Sura hii inapitia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17, bajeti na mwenendo halisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yafuatayo: Miradi ya kielelezo; viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; uimarishaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji; na miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

### 3.2. Utekelezaji wa Bajeti na Mpango wa Maendeleo 2016/17

#### 3.2.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

Katika mwaka 2016/17, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 11,820.503 kwa bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 8,702.697 zilikuwa za ndani na bilioni 3,117.805 za nje. Hadi Aprili 2017, fedha zilizokuwa zimetolewa ni Shilingi bilioni 4,516.7, sawa na asilimia 38 ya bajeti ya maendeleo, ikijumuisha fedha zilizotolewa kwa Halmashauri. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha Shilingi bilioni 3,608.9 fedha za ndani na bilioni 907.8 fedha za nje. Kwa ujumla kiasi cha fedha kilichotolewa ni chini ya maoteo ya mtiririko wa fedha kwa kipindi husika. Hii ilichangiwa na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya kibiashara kufuatia majadiliano na Washirika wa Maendeleo na mabenki kuchukua muda mrefu pia kupanda kwa riba ya mikopo ya kibiashara katika soko la fedha kimataifa hivyo Serikali kufikia uamuzi wa kuahirisha kuchukua mikopo husika. Hata hivyo, kwa upande wa miradi ambayo ina vyanzo vya fedha mahsusi kama vile Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mfuko wa Barabara, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Mfuko wa Maji na Mfuko wa Reli ilipatiwa fedha zote zilizokusanywa katika kipindi husika.

Serikali inaendelea na majadiliano na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha fedha za misaada na mikopo nafuu zinapatikana kama zilivyoahidiwa; kuimarisha makusanyo ya ndani ya Serikali; na kuendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi nchini kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Majadiliano ya Serikali na benki ya Credit Suisse ili kupata mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi kilichobaki yapo katika hatua za mwisho.

Sehemu kubwa ya fedha za maendeleo zilizotolewa zilielekezwa katika miradi ya

ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja, usambazaji wa maji vijijini na mijini, usambazaji wa umeme vijijini, ruzuku na mikopo ya elimu ya juu, ununuzi wa ndege, kuimarisha hospitali za rufaa, matayarisho ya ujenzi wa reli ya kati kwa *Standard Gauge*, na upanuzi wa viwanja vya ndege.

### 3.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 2016/17

#### 3.2.2.1 Miradi ya Kielelezo

Miradi hii imeibuliwa kutoka katika maeneo manne (4) ya kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Miradi hii inapewa msukumo wa kipekee katika utekelezaji kutokana na ukubwa wake; mchango wake katika uchumi, kuzalisha ajira, na mapato ya Serikali; na mchango wake katika kuwezesha sekta nyingine kukua na kuongeza tija. Miradi hii inajumuisha ile ya Kielelezo.

**(i) Ujenzi wa Reli ya Kati**

Mradi huu unahusisha ujenzi wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam – Morogoro - Isaka – Mwanza (km 1,219) na matawi yake ya Tabora - Kigoma (km 411); Isaka - Rusumo (km 371); Keza - Ruvubu (km 36); na Kaliua – Mpanda - Karema (km 321). Utekelezaji wa mradi huu unaratibiwa na Shirika Hodhi la Rasilimali za Reli (RAHCO) chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi).

Hatua iliyofikiwa ni kusainiwa kwa mkataba wa kusanifu na kujenga awamu ya kwanza ya mradi kutoka Dar es Salaam – Morogoro (Km 205) ambapo mkandarasi ameanza matayarisho ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa kambi, ofisi pamoja na kuimarisha kiwanda cha kukarabati mataruma. Taratibu zinazoendelea ni kupata fedha na mikataba ya kandarasi kwa sehemu za reli zilizobakia za: Morogoro hadi Makutupora (Km 336); Makutupora hadi Tabora (Km 294); Tabora hadi Isaka (Km 133); na Isaka hadi Mwanza (Km 249).

**(ii) Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Mradi unahusisha uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya, kulipa madeni pamoja na kuongeza mtaji wa kuanzia wa kuiwezesha uendeshaji wa shughuli za ATCL. Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa ndege mbili (2) zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ambazo zilianza kutoa huduma tangu Oktoba 2016. Vile vile, maandalizi ya ununuzi wa ndege nyingine 4 yamekamilika, ambapo malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 56.89 yamefanyika. Kati ya ndege hizo, moja inategemewa kuwasili Julai 2017; mbili Juni 2018, na ya mwisho, ambayo itakuwa ya masafa marefu inategemewa kuwasili Julai 2018.

### (iii) Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga

Serikali inaendelea na mpango wa kutumia rasilimali za Makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kuwa nyenzo na msingi mkuu wa uchumi wa viwanda nchini. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2016/17 kwa mradi wa Mchuchuma na Chuma Liganga ni malipo ya fidia kwa wananchi wa Mundindi na Mkomang'ombe watakaotoa maeneo yao kwa ajili ya mradi; uthamini wa eneo la kuhamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi. Kwa upande wa mradi wa Liganga shughuli zilizopangwa ni Uthamini wa eneo la kuhamishia wananchi wanaopisha mradi; na kuchangia ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi na kusimamia utekelezaji wa Kampuni ya ubia. Hatua iliyofikiwa ni kukubaliana kwa mfumo wa utekelezaji na ugharamiaji ambapo mwekezaji atajenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuuendesha (Build Own and Operate, BOO) na mauzo ya umeme kwa TANESCO hayatajumuisha gharama za uwekezaji (Capacity charge). Mazungumzo yanayoendelea hivi sasa ni ya bei ya umeme. Muafaka pia umefikiwa kuhusu vivutio vilivyoombwa na mwekezaji kwa lengo la kutafuta manufaa zaidi kwa Taifa katika mradi huo ambapo suala hilo sasa lipo katika utaratibu wa kuwasilishwa kwenye ngazi ya maamuzi ili mradi uanze. Fedha za kulipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi tayari zipo kwenye akaunti ya kampuni ya ubia. Utekelezaji wa malipo ya fidia utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa taratibu husika.

### (iv) Uanzishwaji wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi

Mradi huu ulitengewa Shilingi billioni 2. Kazi zilizofanyika ni: kupima ubora wa udongo; kuandaliwa kwa vitalu vya mbegu za miwa; na taratibu za kupata wataalam wa kufanya upembuzi yakinifu, uchunguzi wa mbegu za miwa, tathmini ya athari za mazingira na ujenzi wa barabara za kuingia katika eneo la mradi zinaendelea.

### (v) Ujenzi wa Mitambo ya Kusindika Gesi Kimiminika

Mradi unalenga kuendeleza gesi asilia inayozalishwa katika kina kirefu baharini kwa kuichakata gesi hiyo na kuigeuza kuwa kimiminika kwa lengo la kuisafirisha nje ya nchi ikiwa imesindikwa na pia gesi hiyo iweze kutumika ndani ya nchi. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na makampuni ya mafuta ya kimataifa na wadau wengine.

Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kupatikana kwa eneo la mradi Likong'o mkoani Lindi; kuundwa kwa timu ya majadiliano na kuandaliwa kwa hadidu za rejea, kupitia nyaraka muhimu zinazohusu mradi (sera, sheria, mikataba, kanuni na mikakati ya Serikali); na kuanza kwa majadiliano na kampuni zinazoshiriki katika mradi juu ya masuala yatakayozingatiwa katika kuandaa mkataba kati ya kampuni husika na Serikali (Host Government Agreement – HGA).

### (vi) Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi

### a. Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo

Mradi wa Bagamoyo SEZ unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itatekelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Merchants Port Holding Company Limited* (CMPort) ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman (State General Reserve Fund-SGRF). Awamu hiyo itahusisha eneo la hekta 3,000 ambapo hekta 800 ni kwa ajili ya ujenzi wa bandari (Sea port) na hekta 2,200 ni eneo maalum la Viwanda (Portside Industrial City). Awamu hiyo itahusisha pia ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) ili kuunganisha eneo la mradi na maeneo mengine ya nchi. Eneo linalobakia la hekta 6,800 litaendelezwa katika Awamu ya Pili itakayokwenda sambamba na awamu ya kwanza kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa mradi. Hatua iliyofikiwa ni kulipa fidia ya Shilingi bilioni 26.66 zilizowezesha kutwaa eneo lenye ukubwa wa hekta 2,399.6. Serikali kupitia EPZA na kwa ushirikiano na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imelipa jumla ya Shilingi bilioni 1.7 ikiwa ni fidia ya eneo lenye ukubwa wa hekta 161.2 lililotengwa kwa matumizi ya *Technology Park*. Hii inafanya jumla ya fidia iliyolipwa kuwa ni Shilingi bilioni 28.37 kwa eneo lenye jumla ya hekta 2,560.8. Ili kuongeza kasi ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, Serikali imeamua kuwa sekta binafsi ipewe nafasi kubwa ya kutekeleza mradi huu ikiwepo kulipa fidia ambapo wawekezaji wamewasilisha andiko la kuendeleza hekta 3,000, na andiko hilo linapitiwa na wataalam kabla ya kuendelea na majadiliano kati ya Serikali na wabia hao.

### b. Eneo Maalum la Uwekezaji la Mtwara

Mradi unahusisha uendelezaji wa eneo maalum la uwekezaji katika Bandari ya Mtwara. Hatua iliyofikiwa ni kutengwa kwa hekta 10 kati hekta 110, kuwa bandari huru (Freeport Zone) kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi na kulikodisha eneo hili kwa wawekezaji wa sekta ya mafuta na gesi; kuwekwa saini mkataba kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalum ya uwekezaji na kukabidhi eneo la hekta 10; na kuendelea na maandalizi ya kuweka miundombinu hususan barabara katika eneo hilo. Bandari ya Mtwara pia inamiliki eneo lenye ukubwa wa hekta 2,600 kwa ajili uwekezaji ambapo litapangiwa matumizi kulingana na mahitaji yatakayojitokeza.

### (vii) Kituo cha Biashara cha Kurasini

Eneo la Kurasini limekabidhiwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA) kwa madhumuni ya kulifanya kuwa kituo cha biashara na huduma. Eneo lina ukubwa wa ekari 62 na kiasi cha fidia kilicholipwa ni Shilingi bilioni 101.04 kwa wafidiwa 1,019. Ili kutekeleza dhana hii, eneo lilitangazwa kwa wawekezaji Desemba, 2016 ambapo makampuni matatu yameonesha nia ya kuliendeleza eneo hilo hususan ujenzi wa miundombinu ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya

viwanda katika eneo hilo.

**(viii) Kusomesha kwa Wingi kwenye Fani na Ujuzi adimu na maalum kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na watu na kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu**

Katika mwaka 2016/17, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ilitengwa Shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kuratibu programu ya kukuza ujuzi na stadi za kazi katika viwanda, kilimo-biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA na madini hususan mafuta na gesi. Hatua iliyofikiwa ni: Vijana 1,000 kati ya 3,000 waliodahiliwa wamehitimu mafunzo ya ushonaji wa nguo kwa vitendo kupitia Viwanda vya Tooku-DSM na Mazava Morogoro na vijana 950 kati yao wameajiriwa; Vijana 100 kati ya 1,000 wameanza mafunzo ya kutengeneza bidhaa za ngozi kwenye Chuo cha DIT – Mwanza; kuanzia Machi, 2017 Vijana 4,300 wameanza mafunzo ya kurasimisha ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa elimu yanayoendeshwa na VETA katika fani za utalii, ujenzi, ufundi umeme na ufundi makenika; kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana 4,600; kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu 4,000; kutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 13,400 waliopo kazini. Miongozo ya mafunzo kwa Vitendo na Uanagenzi (Internship and Apprenticeship Training Frameworks) imeandaliwa.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeendelea kugharamia mafunzo kwa wanafunzi 404 katika fani za afya ambapo wanafunzi 387 wanaendelea na masomo katika vyuo ndani ya nchi na wananfunzi 17 vyuo vya nje ya nchi. Katika kuboresha huduma za kibingwa nchini, wanafunzi 96 wa fani za kubadilisha figo, matibabu ya saratani kwa mionzi, upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa wenye matatizo ya kusikia, na moyo wapo masomoni ambapo wanafunzi 52 wapo katika vyuo vya ndani na wanafunzi 44 wapo katika nchi za India, Afrika Kusini, na Israel.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini inasomesha vijana 341 katika fani na stadi za mafuta na gesi kwa ngazi za vyeti, stashahada na shahada za uzamili na uzamivu nje ya nchi. Vijana 191 wanasomea shahada za uzamili na uzamivu ambapo 115 wapo nje ya nchi na 76 katika vyuo vya ndani. Vijana 150 wanasoma VETA katika ngazi ya vyeti.

Katika mwaka 2016/17, Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi mahususi ya kuongeza ujuzi adimu kama ifuatavyo:

**(i) Ujenzi wa Hospitali Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili:** Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa hospitali ya kufundishia - Kampasi ya Mloganzila. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa hospitali ya

kufundishia - Kampasi ya Mloganzila ambapo watumishi wapya 50 wameajiriwa na wameanza mafunzo kabilishi na Watumishi wengine 131 wa kada za afya wamepewa barua za ajira na wengine wameanza mafunzo katika hospitali ya Mloganzila. Hospitali hii ina uwezo wa kuchukua wagonjwa zaidi ya 600 kwa wakati mmoja na itaanza kutoa huduma mwaka 2017/18 kwa kuimarisha ufundishaji wa wanafunzi madaktari kwa vitendo pamoja na kutoa huduma.

**(ii) Hospitali ya rufaa ya Benjamin Mkapa - Dodoma:** Hatua iliyofikiwa katika kuendeleza na kuboresha utoaji wa huduma za afya ni: kufunga mitambo ya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ikiwemo *MRI, CT – Scan*, *Mammography, General Purpose x-Ray, Fluoroscopy*, *Ultrasound* na *dental x-ray machin*e; na kununuliwa kwa vifaa vya *DNA, Analyser, Dignator PCR na convectional PCR*.

### 3.2.2.2 Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

#### 3.2.2.2.1 Uzalishaji Viwandani

**(a) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka**

Mradi unahusu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda. Mradi utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya malighafi kwa matumizi ya viwanda, hususan, vya madawa, vioo na sabuni. Katika mwaka 2016/17, zilitengwa Shilingi bilioni 1.7 fedha za ndani kwa ajili ya kufanya tafiti za kiteknolojia na kiuchumi (*Techno-Economic study*); kukamilisha utafiti wa kina wa athari za kimazingira; tathmni ya ardhi na mali kwa malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuanza kulipa fidia. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa utafiti wa awali wa njia bora ya uvunaji wa magadi *(brine evaporation simulation by solar ponds);* kukamilika kwa utafiti wa kina kwa lengo la kubaini chanzo cha kuaminika cha maji safi *(detailed hydrological study)* kwa matumizi ya jamii na kiwanda, usanifu wa miundombinu ya maji na utayarishaji wa *Bill of Quantities (BoQ).* Serikali kupitia NDC imekutana na kampuni mbili kutoka China ambazo zimeonesha nia ya awali ya kuwekeza katika mradi huu. Kampuni hizo ni *Inner Mongolia Berun Holding Company Ltd*. na *China National Complete Plants Import and Export Cooperation Ltd* ambazo zimekwisha tembelea mradi na kuchukua sampuli za magadi soda kwa ajili ya utafiti wa kimaabara.

**(b) Mradi wa Kufufua Kiwanda cha General Tyre**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuwezesha kiwanda kuanza uzalishaji. Shilingi milioni 150 fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa kupata gharama za kufufua kiwanda ambapo Kamati ya Watalaam iliundwa kwa ajili ya kuishauri Serikali juu ya: aina ya teknolojia ya

uzalishaji wa matairi inayofaa kutumika; uwezo wa uzalishaji (idadi ya matairi kwa mwaka); upatikanaji wa malighafi; mfumo bora wa uwekezaji; athari za mradi na teknolojia itakayotumika kwa mazingira na jinsi ya kuondoa au kupunguza athari hizo; na soko la matairi. Hatua iliyofikiwa ni kupokelewa kwa taarifa ya kamati ambayo inaonesha kuwa eneo kilipo kiwanda tayari limezungukwa na makazi ya watu na liko mbali na malighafi zinakopatikana Tanga na Morogoro na hivyo linaweza lisiwe rafiki kwa mazingira, gharama kubwa ya usafirishaji; mitambo na teknolojia iliyopo katika kiwanda imepitwa na wakati hivyo inahitajika kufungwa mitambo inayotumia teknolojia ya kisasa itakayowezesha kiwanda kufanya kazi kwa ufanisi na ushindani katika soko; na eneo dogo la kiwanda ambalo linashindwa kuzalisha aina mbalimbali za matairi. Kwa kuzingatia haya, Serikali inatafakari matumizi sahihi zaidi ya eneo la kiwanda na kuangalia namna bora ya kuendesha kiwanda kwa ubia na sekta binafsi ambapo hisa za Serikali zitakuwa thamani ya rasilimali za kiwanda zilizopo.

### (c) Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha

Eneo la viwanda la TAMCO, Kibaha lina ukubwa wa ekari 232. Katika mwaka 2016/17 zilitengwa Shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo kidogo cha kupoozea umeme; ujenzi wa miundombinu ya msingi kwa ajili ya viwanda hasa mfumo wa maji safi na maji taka, bwawa la maji taka (Oxidation ponds) na tanki la maji; na ujenzi wa mtandao wa barabara. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa mgawanyo wa eneo la viwanda la TAMCO Kibaha ambapo viwanda vya nguo na mavazi vimetengewa ekari 95 viwanda vya magari vimetengewa ekari 64 na eneo la ekari 73 limetengwa kwa ajili ya sekta ya madawa na vifaa tiba. Aidha, wawekezaji waliokwishajitokeza na kupewa maeneo ni pamoja na Kampuni ya Global Packaging walioanzisha kiwanda cha vifungashio na kampuni ya kuunganisha matrekta ya URSUS. Aidha, wawekezaji walio katika majadiliano ili kuwekeza katika eneo hilo ni pamoja na kampuni ya magari ya TATA.

### (d) Mradi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta

Mradi wa kuunganisha Matrekta kwa kutumia makubaliano na kampuni ya URSUS ya Poland katika eneo la viwanda, TAMCO-Kibaha. Mradi huu unatokana na Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Poland. Kufuatia mkataba huo Serikali ya Poland imetoa mkopo wa gharama nafuu wa Dola za Marekani milioni 110 kwa NDC. Mradi unalenga: ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta na kuyasambaza (kuyauza) utakaogharimu Dola za Marekani milioni 55.0; ujenzi wa Maghala ya nafaka kwa gharama ya Dola za marekani milioni 55.0; na uanzishwaji wa vituo vinane (8) kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja ambavyo vitatumika kwa ajili ya uuzaji wa matrekta, zana na vifaa vingine. Hatua iliyofikiwa ni kuunganishwa kwa matreka 6 na kufanyiwa majaribio na CAMARTEC ili kuhakiki ubora wake. Serikali imesaidia

kufanikiwa kwa hatua za utekelezaji wa mradi kwa kufanya yafuatayo:-kukabidhiwa kwa eneo la ujenzi wa mradi; kukamilika michoro na kupatikana kwa makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho; kutolewa kwa msamaha wa kodi; kuingiza matrekta na zana zake ambapo jumla ya matrekta 204 na majembe (disc harrows and disc ploughs) 220 yameshaingizwa nchini na kubainishwa kwa maeneo nane (8) ya uanzishwaji wa vituo vya kuhudumia wateja wa matrekta kiufundi.

**(e) Maeneo ya Viwanda KMTC (Kilimanjaro) na Kange (Tanga)**

Shirika la Taifa la Maendeleo linaendelea na uboreshaji wa maeneo ya viwanda (Industrial Parks) katika maeneo yake yaliyopo katika mikoa ya Kilimanjaro (KMTC) na Tanga (Kange) kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa viwanda vipya. Katika kipindi hiki hatua zilizofanyika ni pamoja na kupima na kugawa viwanja kwa wawekezaji watarajiwa, kuendeleza miundombinu ya msingi kama vile majengo (industrial sheds), mtandao wa barabara, mifumo ya umeme, maji safi na maji taka. Tayari kiasi cha Shilingi milioni 280.1 zimetumika katika eneo la Kange, na Shilingi milioni 163.1 katika eneo la KMTC. Serikali kwa upande wake imeendelea kutoa ruzuku kwa utekelezaji wa majukumu ya NDC katika mradi huu.

**(f) Kiwanda cha Viuadudu - TAMCO, Kibaha**

Kiwanda kinalenga kuzalisha viuadudu (biolarvicides) kwa ajili ya kuua viluilui kwenye mazalia ya mbu waenezao malaria. Mradi umegharimu kiasi cha Shilingi bilioni 62.4 na majaribio ya mitambo yamefanyika kama ilivyopangwa, na kiwanda kimeanza uzalishaji. Katika mwaka 2016/17, Shilingi bilioni 6.787 zilitolewa na Serikali ambapo Shilingi bilioni 2.187 zilitolewa kwa ajili ya: kulipa malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi wa kiwanda; malipo kwa LABIOFAM ili kukamilisha ujenzi wa kiwanda na kuanza uzalishaji; kulipa malimbikizo ya bili za umeme na maji na kodi ya ardhi ya TAMCO; na kulipa sehemu ya malimbikizo ya deni la mkandarasi wa ujenzi wa barabara. Vile vile, lita 101,080 za viuadudu zilizalishwa na kuuzwa Niger (lita 100,000) na Taasisi ya Madaktari Wasio na Mipaka (lita 440), Kampuni ya Mabao Investment and General Pest Control (lita 200) na Halmashauri ya Mji wa Geita (lita 440).

**(g) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO**

Katika mwaka 2016/17, zilitengwa shilingi bilioni 6.05 kwa ajili ya: kuboresha na kujenga miundombinu ya mitaa ya viwanda vidogo katika mikoa ya Morogoro, Dar es salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; kuimarisha ubunifu wa teknolojia na kutoa huduma za kiufundi; kutoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini; kujenga uwezo wa wajasiriamali kupata na kutumia taarifa za masoko kupitia TEHAMA; na kuboresha utoaji huduma za kifedha. Hadi kufikia Machi utekelezaji ni: kutengwa kwa maeneo ya viwanda vidogo katika mikoa ya Dar es Salaam (Vingunguti

Industrial Estate, hekta 12.9), Mbeya (Kitalu U, hekta 8.44), Mwanza (Nyankato Industrial Estate, hekta 2.7), na Morogoro (Eneo la viwanda Kihonda, hekta 6.0); kukamilika kwa maandalizi ya mipango ya biashara na matumizi bora ya ardhi; kutengenezwa na kuboreshwa kwa teknolojia mpya 30 kupitia vituo vya SIDO katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Lindi, Mbeya na Shinyanga ambazo zimesaidia kuanzishwa kwa viwanda 185 na ajira 524 katika wilaya mbalimbali chini ya mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja; kozi 230 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 5,750; kutolewa kwa ushauri wa kuanzisha na kuendeleza biashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 8,911; na kufikiwa kwa wajasiriamali 2,732 kwa huduma za taarifa za masoko kwa kupitia TEHAMA.

**(h) Uendelezaji Wajasiriamali:** kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF), Shilingi bilioni 2.4 fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali ambao unatoa mikopo midogo kwa wenye viwanda na wafanyabiashara wadogo. Chini ya mfuko huo, jumla ya mikopo 1,715 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.457 ilitolewa kupitia ofisi za SIDO za mikoa ya Tanzania Bara ambayo iliwezesha upatikanaji wa ajira 6,310.

#### 3.2.2.2.2 Madini

#### a) Biashara ya Madini, Uchimbaji na Ukaguzi wa Migodi Nchini

Katika kusimamia biashara ya madini nchini na kuhakikisha kuwa madini yanawanufaisha wananchi, Serikali imeendelea kusimamia utumiaji wa malighafi za madini zinazopatikana hapa nchini. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzuia uingizaji wa makaa ya mawe na jasi toka nje ya nchi. Serikali ilitoa mafunzo juu ya ushiriki wa Watanzania katika uwekezaji nchini (local content). Mafunzo haya yalifanyika katika kanda sita (6) nchi nzima ambazo ni Kanda ya Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Kaskazini. Ili kuimarisha hali ya Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira kwa wachimbaji wa migodi katika maeneo mbalimbali nchini, Serikali iliendelea kufanya ukaguzi kwenye migodi ya wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa ili kuhakikisha wamiliki wanafuata Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake. Katika kipindi hiki, jumla ya migodi 1,115 ilikaguliwa ambapo migodi mikubwa ilikuwa minne (4), ya kati 52 na midogo 1,059.

#### b) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa leseni za madini. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2016 jumla ya maombi ya leseni 6,521 ya utafutaji na uchimbaji madini yalipokelewa. Kati ya hayo, maombi 386 ni ya utafutaji mkubwa, maombi 6,122 ni ya uchimbaji mdogo na maombi 13 ni ya uchimbaji wa kati. Baada ya uchambuzi wa maombi hayo, jumla ya leseni 2,540 zilitolewa, kati ya hizo leseni 193 ni za utafutaji mkubwa, 6 za uchimbaji wa kati na 2,341 za uchimbaji mdogo.

### c) Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini

Ili kuendeleza uchimbaji mdogo nchini, Serikali imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Februari, 2017 Serikali imetenga maeneo 11 kwa ajili ya wachimbaji madini wadogo yaliyopo maeneo ya: Msasa na Matabe Mkoani Geita; Biharamulo na Kyerwa Mkoani Kagera; Itigi Mkoani Singida; D-Reef, Ibindi na Kapanda Mkoani Katavi; Ngapa Mkoani Songea; Nzega Mkoani Tabora na Kitowelo Mkoani Lindi. Maeneo hayo yana ukubwa wa takriban hekta 38,567.

### d) Mradi wa Dhahabu wa Buhemba

Shirika la Taifa la Madini - STAMICO lilifanya uchambuzi yakinifu kuona uwezekano wa kujenga kiwanda cha kuchenjua mabaki ya dhahabu katika mgodi wa Buhemba. Katika mwaka 2016/17 Shilingi bilioni 17.5 zimetengwa kwa ajili ya kununua mashine ya kuchenjua mabaki ya dhahabu, kufanya upembuzi yakinifu katika miamba migumu na kuchoronga miamba migumu. Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa tathmini na ukadiriaji wa mashapo ya madini.

### e) Mradi wa Kununua Madini ya Bati

Katika kuimarisha soko la wachimbaji wadogo wa madini ya bati toka mwaka 2014 STAMICO ilianza kununua madini kutoka kwa wachimbaji wadogo wa vijiji vya Kabingo, Murongo, Syndicate na Rugasha Wilaya ya Kyerwa, Kagera. Katika mwaka 2016/17 Shilingi bilioni 1.12 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madini hayo. Hatua iliyofikiwa ni kununuliwa kwa kilo 1,205 za madini ghafi ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo ambapo tani 18.08 za madini hayo ziliuzwa na kulipatia Shirika Shilingi milioni 325.49.

### 3.2.2.2.3 Kilimo

Kilimo ni moja ya maeneo yanayotoa fursa ya kipekee kwa maendeleo ya viwanda nchini. Fursa hizo ni pamoja na upatikanaji wa malighafi za uzalishaji viwandani; masoko ya viwanda vya uzalishaji zana na pembejeo za kilimo; kuongeza kipato cha wananchi wengi na hivyo kuinua utashi wa soko la ndani; na upatikanaji wa chakula nafuu kwa wakazi wa mijini na wafanyakazi viwandani, kitu ambacho ni muhimu katika kuongeza uhimilivu wa bei. Hivyo yafuatayo yalizingatiwa katika mpango wa 2016/17.

### (a) Kilimo cha Mpunga na Miwa

Katika mwaka 2016/17 zilitengwa Shilingi bilioni 4.35 fedha za ndani kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa tani 290,000 na sukari tani 150,000 ili kutosheleza soko la ndani na kuuza ziada nje ya nchi; kukamilisha upatikanaji wa hatimiliki za mashamba makubwa sita (6); kuwezesha upatikanaji wa mashamba mapya ya uwekezaji katika mikoa ya Katavi, Kigoma, Rukwa, Tabora, Lindi na

Ruvuma; kuandaa kanzidata na mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa vijiji vinavyozunguka mashamba 12 ya uwekezaji; kupima na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la Ludewa na Rufiji; na kutoa hatimiliki za kimila kwa wakulima wadogo (outgrowers) katika eneo la Kilombero na Rufiji Chini. Hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa program ya muda mrefu na muda mfupi ya upimaji na umilikishaji wa ardhi hususan kwa matumizi ya kilimo. Serikali imetoa shamba lenye ukubwa wa hekta 10,000 lililopo Makurunge wilayani Bagamoyo kwa Kampuni ya Bakhresa Group of Companies kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari. Hatua za awali za kulima na baadae kujenga kiwanda cha kusindika miwa zimeanza.

**(b) Kilimo cha Mahindi**

Katika mwaka 2016/17 zilitengwa Shilingi bilioni 7.27 fedha za ndani na bilioni 10.55 fedha za nje kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maghala na masoko ya kimkakati ya Mulongo, Sirari, Kabanga, Kahama na Kyerwa; ukarabati wa maghala matano katika skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa, Mvumi, Kigugu na Mbogo zilizopo katika mikoa ya Manyara na Tabora; ununuzi wa vifaa katika maghala 98 ya COWABAMA yaliyopo katika halmashauri 12 nchini; upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maghala katika mikoa 12 ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati na Kanda ya Magharibi; na ukarabati wa magahala 26 katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa maghala 106 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Mbeya, Songea, Kalambo, Mbozi, Momba na Njombe; na kuendelea na ukarabati/ujenzi wa maghala 48 katika Halmashauri za Wilaya za Songea, Mlele, Nsimbo, Kalambo, Mbozi, Njombe, Wanging'ombe, Mpanda, Sumbawanga na Mbeya ambayo inatekelezwa kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili.

**(c) Huduma za Umwagiliaji**

**(i) Huduma ya Umwagiliaji Kupitia Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP):** Katika mwaka 2016/17, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya umwagiliaji ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 103 na maghala 53 pamoja na kuendelea kujenga skimu 37 ambazo ujenzi wake haukukamilika. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu za Kilosa kwa Mpepo (Halmashauri ya Malinyi), Simbo (Igunga) na skimu ya Ibanda (Halmashauri ya Sengerema na Geita) na Bwawa la Gidahababierg (Halmashauri ya Hanang'). Vile vile, usanifu katika skimu za Rudewa (Kilosa) na Endagaw (Mbulu) umekamilika. Serikali pia inaendelea na ujenzi katika skimu za Usoke Mlimani (hekta 530) katika Halmashauri ya Urambo na Mforo (hekta 290) katika Halmashauri ya Mwanga. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kuwapata

makandarasi wa ujenzi wa skimu za Hangangadinda (hekta 250) katika Halmashauri ya Madaba na Igongwa (hekta 300) katika Halmashauri ya Misungwi zinaendelea. Serikali pia imeendelea kupitia Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kazi hiyo itakamilika katika mwaka 2018/2019.

(ii) **Huduma ya umwagiliaji kupitia Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za wakulima Wadogo (Small scale Irrigation Development Project-SSIDP):** Katika mwaka 2016/17 Serikali ilipanga kuendelea na ukarabati na uboreshaji wa skimu 45 za umwagiliaji za awamu ya kwanza zenye jumla ya hekta 13,722. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa skimu zote 45. Kukamilika kwa ukarabati na uboreshaji wa skimu hizo kumeongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 7,012 kutoka hekta 461,326 mwaka 2015/16 hadi hekta 468,338 mwaka 2016/17 (sawa na ongezeko la asilimia 1.52).

### (d) Kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Chakula

Katika mwaka 2016/17 Shilingi bilioni 61.75 fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula - NFRA wa kuhifadhi mazao kutoka tani 246,000 hadi tani 496,000 za nafaka katika kanda za: Arusha (Babati), Dodoma (Dodoma), Makambako (Makambako na Mbozi), Shinyanga (Shinyanga), Songea (Songea) na Sumbawanga (Sumbawanga na Mpanda) kwa kuwezesha upatikanaji wa maeneo na kukamilisha taratibu za kupata makandarasi na kuanza ujenzi wa maghala na vihenge vya kisasa (Silos) na kukamilisha ujenzi wa ghala la Mbozi lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za nafaka. Hatua iliyofikiwa ni kukamilisha taratibu zote za upatikanaji wa fedha kupitia ufadhili wa Serikali ya Poland kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Wakala umeanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi kwa: kufanya upembuzi yakinifu wa mradi (Technical Feasibility, Basic Designs and Cost estimates); kufanya uchunguzi wa udongo kwenye maeneo yote ya ujenzi; kufanya mchakato wa zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalamu mwelekezi wa kusimamia mradi na mkandarasi wa kutekeleza ujenzi; kufanya tathmini ya athari za mazingira katika maeneo yote ya mradi. Wakala pia umenunua jumla ya tani 62,099.3 za mahindi sawa na asilimia 62 ya lengo ililojiwekea. Hii inafanya akiba ya chakula hadi Machi 2017 kufikia tani 86,443.8.

### (e) Uongezaji Tija na Uzalishaji wa Mpunga

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuongeza tija na uzalishaji wa mpunga; kuinua kipato cha mkulima kupitia teknolojia ya Kilimo Shadidi; kuboresha miundombinu ya umwagiliaji; kuboresha masoko kwa kujenga ghala moja kwa kila skimu; kuboresha miundombinu ya barabara kwa ajili ya skimu za Njage na Mvumi; kuongeza uzalishaji na ubora wa mbegu katika Halmashauri za

Mvomero, Kilosa na Kilombero; na kuendelea na skimu za Mbogokomtonga na Kigugu (Halmashauri ya Mvomero), Mvumi (Halmashauri ya Kilosa), Msolwa Ujamaa na Njage (Halmashauri ya Kilombero). Hatua iliyofikiwa ni: Wagani na mafundi sanifu 48 na wakulima 456 wamepatiwa mafunzo ya Kilimo Shadidi na watapatiwa ruzuku ya pembejeo katika mfumo wa uchangiaji; na mashamba ya mfano 80 yameanzishwa kwa ajili ya kupeleka teknolojia ya Kilimo Shadidi. Kituo cha KATRIN kiliweza kuzalisha tani 3 za mbegu kwa ajili ya uzalishaji. TOSCI walizalisha aina 11 za mbegu ambapo aina 8 zilipitishwa; jumla ya mashamba ya mfano 120 yameanzishwa katika Halmashauri za Kilombero, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijini, Gairo, Malinyi na Ulanga kwa ajili ya kupeleka aina 13 za mbegu kwa wakulima; na upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Njage, Msolwa Ujamaa, Mvumi na Kigugu umefikia asilimia 70; na hatua za kumpata mtaalamu mwelekezi wa kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa maghala matano (5) - ghala moja kwa kila skimu zimekamilika na ujenzi unatarajia kuanza mwaka 2017/18.

**(f) Tafiti za Kilimo**

Mradi ulilenga kuimarisha vituo vya utafiti. Katika mwaka 2016/17, Shilingi milioni 854 fedha za ndani na milioni 53 fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya kuzalisha tani 10 za mbegu mama za mpunga; kutafiti teknolojia za kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani kwa mazao ya kipaumbele; kukarabati na kuimarisha vituo 12 vya utafiti nchini; na kuboresha aina 13 za mbegu ya mpunga. Hatua iliyofikiwa ni: kuzalisha aina 35 za mbegu mpya za mazao ya Mahindi (9), Mpunga (2), Karanga (3), Korosho (16), Maharage (2) na Viazi vitamu (3). Mbegu mama za awali *(Breeder and Pre-basic seeds*) za mazao mbalimbali za msimu 2015/16 zimezalishwa. Mbegu mama zilizozalishwa ni: Pamba kilo 2,600 na Viazi mviringo miche 60,000. Mbegu mama zilizozalishwa ni: Pamba kilo 2,600 na Viazi mviringo miche 60,000; Muhogo pingili 2,008,000; Viazi vitamu vipando 3,476,750; Viazi mviringo kilo 5,150; Mpunga kilo 2,940; Mahindi kilo 11,300; Ngano kilo 1,560; Soya kilo 1,900; Maharage kilo 43,900; Migomba miche 1,830 na Parachichi miche 3,390. Pia vizazi *(germplasm)* 1,228 vya mbegu za Mpunga na 172 vya Ulezi vilikusanywa na kutunzwa vituoni.

**(g) Upatikanaji wa Pembejeo**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima nchini ili kuinua tija. Hatua iliyofikiwa ni: Upatikanaji wa mbolea wa kiasi cha tani 277,935 sawa na asilimia 57 ya mahitaji ya tani 485,000 ya mbolea; kutolewa kwa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazao ya mahindi na mpunga katika mikoa 25 ya Tanzania Bara kwa kaya 378,900 kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania - TFC. Kupatikana kwa jumla ya tani 30,823 kati ya tani 32,394 za mbolea sawa na asilimia 95 ya lengo, ambapo kati ya hizo, tani 12,850 ni za mbolea ya kupandia sawa na asilimia 89 ya lengo la tani14,421 na tani

17,973 ni za mbolea ya kukuzia sawa na asilimia 100 ya lengo. Kusambazwa kwa mbolea kiasi cha tani 26,999 sawa na asilimia 83 katika maeneo ya mauzo ya Kampuni ya TFC katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na jumla ya tani 23,515 sawa na asilimia 73 ya lengo zimeshawafikia wakulima na kazi ya usambazaji inaendelea.

**(h) Ushiriki wa Vijana Katika Kilimo (Kambi ya Mkongo ) – Rufiji**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuandaa shamba la kilimo la ekari 220, kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kupima na kupata hatimiliki, na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana. Hatua iliyofikiwa ni vijana 261 kupata mafunzo kwa vitendo juu ya kilimo cha mbogamboga, bustani, ufugaji wa mbuzi, kuku wa kienyeji, nyuki na sungura. Eneo la kambi limekwa miundombinu ya umwagiliaji wa matone, umeme wa nguvu za jua, kisima cha maji, jengo la jiko la shamba na bustani ya maonesho kwa ajili ya kilimo cha zao la muhogo na uzalishaji wa mbegu za muhogo. Vile vile, zaidi ya vijiji 20 vya vijana vimeanzishwa katika wilaya mbalimbali baada ya kupata mafunzo kwenye kambi hii vikiwemo RUSUYA (Mkuranga), RUYOFO, Faraja Group, Kiemi Group na Amani Group (Rufiji), Maisha *Youth Agriculture Group* (Bagamoyo), Viwawaki (Kisarawe) na *Vision Group* (Kibaha). Kati ya vikundi hivyo, vinne (4) vimeunganishwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 3.2.2.2.4 Mifugo

**(a) Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji Katika Sekta ya Mifugo**

Katika mwaka 2016/17 zilitengwa Shilingi milioni 791.55 fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa mitamba na mbegu bora kwenye mashamba matano (5) kwa kununua ng'ombe wazazi; kuimarisha vituo vya uhimilishaji vya NAIC - Usa River na Sao Hill; ujenzi wa minada miwili (2) ya mpakani Longido na Kirumi; kukarabati minada ya upili ya Nyamatala na Kasesya ili kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na kuwezesha operesheni ya kuthibiti biashara ya mifugo kwenye minada na masoko ili kuhakikisha mifugo inafikishwa machinjioni. Hatua iliyofikiwa ni: kununuliwa kwa *chiller* kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha hewa baridi ya Naitrojeni katika kituo cha NAIC –Usa River (Arusha) na jumla ya wataalam wa uhimilishaji 230 kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro, mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na Ziwa walipata mafunzo kupitia *Land O' Lakes International Development* kwenye mradi wa *Public Private Partinership for Artificial Insemination Delivery* – PAID; kuhimilishwa kwa ng'ombe 457,557 ukilinganisha na ng'ombe 120,688 mwaka 2015/16 na kuzalishwa kwa dozi za mbegu 100,000; ujenzi wa mazizi ya kuhifadhia mbuzi katika mnada wa Nyamatala na kituo cha Polisi; kukamilika kwa ujenzi wa kishushio na kipakilio cha mifugo (loading and unloading ramp); na ukarabati wa mfumo wa maji na usimikaji wa matenki ya kuhifadhi maji katika mnada wa Pugu.

**(b) Miundombinu ya Maji na Maeneo ya Malisho**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuainisha na kutenga maeneo ya maji na malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Shilingi bilioni 2 zilitengwa kwa ajili ya kuchimba malambo 5 katika Wilaya za Lindi, Chunya, Kilindi, Kilosa na Rufiji; kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za malisho kwenye mashamba nane (8) ya malisho kwa kuyapatia mashine na vitendea kazi; kutambua, kutenga na kutangaza kwenye gazeti la Serikali maeneo ya nyanda za malisho kwenye vijiji 50 vya Wilaya za Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Mpanda, Kaliua, Kilombero, Iramba, Kiteto, Igunga, Lindi na Kilindi; na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo yaliyotengwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 20. Hatua iliyofikiwa ni: kuimarishwa kwa shamba la kuzalisha mbegu bora za malisho la Langwira kwa kukarabati ofisi iliyoezuliwa na upepo mwaka 2015 na kujengwa kuwa banda la kuhifadhi hei na mbegu bora za malisho; kuzalishwa kwa marobota ya hei 456,016 na mbegu za malisho bora za nyasi kilo 3,717.1 na jamii ya mikunde kilo 731.5.

**(c) Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Mifugo**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga madarasa matatu (3) katika kampasi za Madaba na Kikulula; ukarabati wa darasa moja na hosteli katika Chuo cha Mafunzo ya Mifugo – Morogoro; ukarabati wa maktaba katika vyuo vya Mabuki na Kikulula na kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ili kuongeza wataalam wa uvuvi na teknolojia mbalimbali kuhusu uvuvi na ufugaji wa samaki. Hatua iliyofikiwa ni: Wakala kuendelea na zoezi la udahili wa wanafunzi ambapo wanafunzi 1,962 kati ya hao 726 ni wa Stashahada na 1,236 ni wa Astashahada; wanachuo 1,324 (Stashahada 582 na 742 Astashahada) watahitimu mafunzo yao juni 2017; jumla ya ng'ombe 1,695 walifanyiwa tafiti katika taasisi sita kati ya saba zilizopo chini ya TALIRI na kuzalisha na kuhifadhi kosaafu za mbuzi 1,116 aina ya Malya wa asili ya chotara katika vituo vya Mpwapwa, Tanga, Mabuki, West Kilimanjaro, Naliendele na Kongwa; kutolewa elimu kwa wadau 5,430 kupitia mafunzo, mikutano na semina; kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya kukarabati darasa moja Kikulula; ukarabati wa maabara 3 za Parasitologia katika Kampasi za Mpwapwa, Morogoro na Madaba na kuziwekea vifaa vipya vya kisasa ambapo vifaa vya maabara hizo vimeshaingia nchini. Ukarabati wa jengo la kompyuta (Computer lab), ofisi na nyumba mbili za watumishi umefanyika katika Kampasi za Madaba, Morogoro na Kituo cha Kikulula; kujengwa kwa banda la nguruwe katika Kampasi ya Buhuri kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na uzalishaji; kutolewa mafunzo ya wiki mbili kwa wafugaji 37 katika Kampasi ya Tengeru na kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI).

**(d) Kudhibiti Magonjwa ya Milipuko na ya Kipaumbele**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo, kuzalisha chanjo za mifugo Kibaha na kununua chanjo ya kichaa cha mbwa. Hatua iliyofikiwa ni: kusambazwa kwa dozi 17,600 za chanjo ya Kichaa cha Mbwa kwa Mamlaka ya Mji Kibaha (4,800), Wilaya za Kibaha (4,700), Kisarawe (4,100), Dodoma (1,000) na Kondoa (3,000); dozi 30,055,100 za chanjo ya I-2 ya ugonjwa wa mdondo, dozi 680,900 za chanjo ya Kimeta na dozi 121,550 za chanjo dhidi ya ugonjwa wa Chambavu, dozi 10,000 za ugonjwa wa Kitupa Mimba zimezalishwa na kusambazwa nchini. Sampuli 1,632 za mifugo na wanyama pori zilipokelewa na kufanyiwa uchunguzi; na jumla ya sampuli 493 za vyakula vya mifugo zilifanyiwa uchunguzi.

**(e) Kuwezesha Uwekezaji wenye Tija Katika Ranchi za Taifa (NARCO)**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuwezesha NARCO kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa Ruvu na kununua ng’ombe wazazi 1,200. Hatua iliyofikiwa ni: kuzalishwa kwa mitamba 634 katika Ranchi za NARCO kuzalishwa na kukuza ndama 3,753 kutokana na ng’ombe wazazi 5,294; kununua ng’ombe 1,864 kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya programu ya unenepeshaji; kuchinja ng’ombe 2,134 wakiwa wamenenepeshwa; na kuuza ng’ombe 3,892; Vile vile, NARCO imesimamia na kutoa ushauri wa ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wadogo wadogo ambapo ranchi hizo zimewekeza ng’ombe 60,546, mbuzi 6,735 na kondoo 3,428; na kupatikana kwa mkopo wa riba nafuu wa Dola za Kimarekeni milioni 50 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Ushirikiano wa Kiuchumi wa Serikali ya Korea (EDCF) kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa machinjio ya Ruvu, kuongeza idadi ya mifugo, kujenga viwanda kwenye eneo la ranchi ya Ruvu na kutengeneza bidhaa za ngozi.

**3.2.2.2.5 Uvuvi**

**(a) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga bandari ya uvuvi ambayo itawezesha meli zinazovua katika bahari kuu kutia nanga nchini ili kuwezesha Serikali kusimamia kwa ufanisi uvuvi katika bahari kuu. Shilingi milioni 500 fedha za ndani na milioni 24 fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu ili kubaini eneo ambalo litafaa kwa ujenzi wa bandari kati ya maeneo mawili (2) yaliyopendekezwa ya Mikindani (Mtwara) na Bagamoyo (Pwani). Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kwa majadiliano na Mtaalamu Mwelekezi ambaye anatarajiwa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuainisha maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa bandari ya uvuvi. Eneo la Gati Namba 6 katika Bandari ya Dar es Salaam lililopo chini ya Mamlaka ya Bandari – TPA limeboreshwa wakati maandalizi ya awali ya ujenzi wa bandari kamili yanaendelea.

### (b) Kuimarisha Ufugaji wa Viumbe Majini

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuimarisha ufugaji wa samaki wa maji baridi katika vituo vitano (5) vya kuzalisha vifaranga vya samaki vya Mwamapuli - Tabora, Ruhila - Songea, Kingolwira - Morogoro, Nyigedi - Lindi na Nyamirembe - Chato na vituo viwili (2) vya samaki wa maji chumvi vya Machui - Tanga na Mbegani – Bagamoyo; kuchimba mabwawa 5 ya kukuzia samaki katika kituo cha Machui - Tanga; kujenga na kufunga vifaa vya *hatchery* katika vituo vya maji chumvi vya Machui - Tanga na Mbegani-Bagamoyo; kujenga *hatchery*, ofisi na kufunga vifaa vya *hatchery* katika vituo 5 vya ufugaji samaki maji baridi vya Mwamapuli-Igunga, Ruhila-Songea, Kingolwira-Morogoro, Nyengedi - Lindi na Nyamirembe - Chato. Hatua iliyofikiwa ni: kukarabati mabwawa ya kuzalisha samaki katika vituo vya Ruhila (Songea) na Mwamapuli (Igunga – Tabora); kukarabati vituo vitano (5) vya uzalishaji samaki wa maji baridi; kuwekwa kwa vitotoleshi (Incubators 15) vya samaki aina ya perege katika kituo cha Kingolwira vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga 11,520,000 kwa mwaka; kuzalishwa kwa vifaranga 421,368 katika vituo vya serikali vya Ruhila (153,000), Mwapuli (120,000), Machui (10,000) na TAFIRI- Mwanza (138,368); kuzalishwa kwa vifaranga 253,200 vya samaki aina ya tilapia na vifaranga 30,700 aina ya sato; kupandikizwa kwa vifaranga 3,000 katika mabwawa ya asili ya Ngerengere na Bwawani yaliyopo Morogoro. Kukarabatiwa kwa vituo viwili (2) vya uzalishaji samaki maji bahari vya Bagamoyo na Machui na kuanza kukuza samaki 3,450. Kuzalishwa kwa vifaranga 13,697,904 aina ya perege katika mashamba ya watu binafsi.

### (c) Kuimarisha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi

Katika mwaka 2016/17 zilitengwa Shilingi milioni 400 fedha za ndani na bilioni 2.2 fedha za nje kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya uvuvi katika vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi, mialo, karakana ya kutengenezea maboti (Boatyards) na vituo vya uthibiti wa ubora na viwango; kuimarisha ushirikishwaji wa jamii za uvuvi na kuimarisha doria katika maeneo ya kipaumbele. Hatua iliyofikiwa ni: kuendesha doria yenye siku kazi 6,118 katika maeneo ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi ambapo yalikamatwa makokoro 695, kamba za kokoro mita 100,920, nyavu za makila 6,592, nyavu za dagaa (chini ya mm 8) 5,145, nyavu za utalii 3,865, baruti 59, mitungi ya gesi 74, "detonators" 105, "compressors" 3, Mbolea aina ya Urea kilo 41, Mitumbwi 87, vifaa vya kuzamia jozi 44, boti 232 na Injini ya boti 1; watuhumiwa 241 walikamatwa kwa makosa mbalimbali ya uvunjaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi na kufikishwa mahakamani; na MATT kufanya ukaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam uliowezesha kukamatwa kwa kontena la nyavu haramu. Vile vile, kaguzi 585 za kuhakiki ubora wa samaki na mazao yake zimefanyika ambapo jumla ya kilo 6,393,239 na samaki hai wa mapambo 112,020 walikaguliwa kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

#### (d) Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Uvuvi

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuiwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI). Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa mawili (2) na kuweka umeme katika Kampasi ya Mikindani; kuendelea na ujenzi wa Hostel mbili (2) kwa Kampasi ya Gabimori (Rorya); kuendelea na ukarabati katika vituo vya Nyegezi na Kibirizi (Kigoma); kufanyika kwa sensa ya wavuvi na vyombo vyao katika ziwa Victoria; na kufanyika kwa tafiti ya wingi wa samaki kwa njia ya *hydroacoustic* katika ziwa Victoria ambapo mpaka sasa takwimu ya hali ya uvuvi katika ziwa hilo inaonesha kuwa samaki aina ya Sangara walipungua toka tani 651,353 mwaka 2014 hadi tani 621,253 mwaka 2015. TAFIRI ilifanya utafiti wa uhifadhi wa mazingira kwa lengo la kupunguza upotevu wa misitu na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika vijiji vilivyo katika mwambao wa ziwa Tanganyika; na usambazaji wa teknolojia ya ubanikaji mzuri wa samaki iliyojumuisha majiko sanifu ya kubanika samaki kwa vikundi vya BMU, wachakataji wa samaki na jamii zinazohusika na uvuvi.

### 3.2.2.2.6 Maliasili na Misitu

#### (a) Mradi wa Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management (KILORWEMP)

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Ubelgiji katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Rufiji. Lengo la mradi huu ni usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhi oevu ya Bonde la Kilombero na Mto Rufiji ili kuboresha maisha ya wananchi. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi na kujenga uwezo kwa WMAs za ILUMA na JUHIWANGUMWA; kuwekwa alama za mipaka ya maeneo kwa upande wa ILUMA na kugharamia mafunzo ya watumishi.

#### (b) Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bioanuai Tanzania

Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bioanuai Tanzania (Enhancing the Forest Nature Researve Network for Biodiversity conservation in Tanzania) unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na UNDP. Mradi unatekelezwa katika Misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia 12 kwa kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa hifadhi hizo na kuboresha miundombinu ya hifadhi ili kukuza utalii na ustawi wa ikolojia. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kutangazwa kwa misitu ya hifadhi asilia mipya nane (8) kwenye gazeti la Serikali na kusafishwa na kuwekewa *beacons* misitu hiyo nane; kukamilika kwa mipango ya usimamizi wa misitu kumi na mbili; kununuliwa magari mapya matano pamoja na kuanza kwa ujenzi wa ofisi sita (6) za wahifadhi na vituo (Ranger posts) kumi na tano (15).

### (c) Mradi wa Kuwezesha Jamii Katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mabadiliko ya Tabia Nchi

Mradi wa kuwezesha jamii katika usimamizi shirikishi wa misitu na mabadiliko ya tabia nchi (Empowering Communities through Training on PFM, REDD+ and Climate Change Initiatives - ECOPRC) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Norway. Mradi huu upo chini ya Usimamizi wa Chuo cha Misitu Olmotonyi na unatekelezwa kwa pamoja na mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), Taasisi ya *Regional Community Forestry Training Centre for Asia and Pacific (RECOFTC)* ya Thailand na Chuo kikuu cha Kilimo Sokoine. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuwezesha Halmashauri za Wilaya na NGO's kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Hewa Ukaa na Ukataji Miti (MKUHUMI) na Mabadiliko ya Tabianchi; kuboresha miundombinu ya Chuo cha Misitu-Olmotonyi; na kuendeleza programu hiyo katika wilaya za Bagamoyo, Kilombero, Kiteto na Same.

## 3.2.2.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Viwanda na Maendeleo ya Watu

Ujenzi wa uchumi wa viwanda una mahitaji tofauti ya rasilimali watu ikilinganishwa na mahitaji ya uchumi wa kilimo. Tafiti zinaonesha kuwa Tanzania ina upungufu mkubwa wa rasilimali watu yenye ustadi na weledi wa shughuli za uchumi wa viwanda. Hivyo, msukumo umewekwa katika kuongeza weledi na upatikanaji wa mahitaji halisi ya rasilimali watu kwa uzalishaji na usimamizi wa viwanda ukilenga maeneo yafuatayo:-

### 3.2.2.3.1 Elimu, Sayansi na Teknolojia

### A. Elimumsingi

Msukumo katika elimumsingi ni kutoa elimu bila malipo na kuimarisha ubora na ufaulu katika ngazi hii ya elimu. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

### (a) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kutekeleza programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (P4R) ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa shule 274 ikiwemo shule za sekondari 132 na msingi 142 katika halmashauri 119 ikijumuisha ujenzi wa madarasa 1,081, vyoo 2,802, Mabweni 200, Mabwalo 9, majengo ya utawala 6, na nyumba 11 za walimu ; kukamilika kwa ukarabati wa vyuo vya ualimu kumi (10) vya Tabora, Korogwe, Klerruu, Butimba, Morogoro, Tukuyu, Kasulu, Songea, Mpwapwa na Marangu; ununuzi na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na kemikali kwa ajili ya maabara za vyuo vya ualimu vya Kasulu, Korogwe, Tukuyu, Butimba na Tabora; ununuzi wa vifaa vya maabara kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari 1,625; na uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya Kiada nakala 1,958,628 vya kidato cha 1-4 na nakala 541,372 kwa kidato cha 5-6.

### (b) Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuandaa, kuchapa na kusambaza mitaala pamoja na machapisho ya mihtasari na kiongozi cha mwalimu kwa ajili ya elimu ya awali, darasa la I – VI, kuhuisha mitaala ya stashahada na shahada ya ualimu ili kuingiza masuala ya KKK. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 6,492,843 vya elimu ya awali, nakala 6,862,800 vya darasa I, nakala 6,862,800 vya darasa la II na nakala 6,818,181 vya darasa la III; kutoa mafunzo kwa walimu 519 kutoka katika shule na vitengo 252 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum (wasioona na wenye ulemavu wa kusikia) wa darasa la I na la II; walimu 22,995 wanaofundisha Darasa la III na IV kutoka mikoa 19; na walimu 16,079 wa elimu ya awali.

## B. Ufundi na Teknolojia

### (a) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa vyuo vitano (5) vya mikoa ya Njombe, Kagera, Rukwa, Geita na Simiyu. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kuanza kwa ujenzi wa chuo cha mkoa wa Njombe; kukamilika kwa makabrasha ya ujenzi wa vyuo vya Kagera, Rukwa, Geita na Simiyu.

### (b) Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa jengo la kufundishia la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) awamu ya pili. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kufundishia (*DIT Teaching Tower Complex*) ambapo shughuli za usimikaji wa miundombinu ya umeme, mabomba, lifti na ujenzi wa sakafu unaendelea.

### (c) Kuimarisha Tafiti, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendeleza juhudi za kujenga uchumi wa viwanda kwa kuimarisha uwezo wa nchi wa kufanya tafiti na uratibu wa sayansi na teknolojia ili kuchochea ubunifu katika maendeleo. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa maandalizi ya Mwongozo wa kutambua Wabunifu na Wagunduzi nchini (*National Inventions and Innovations Guidelines*); ukarabati na ununuzi wa vifaa vya maabara katika kituo cha utafiti wa Uvuvu (TAFIRI – Sota); kuchochea ubunifu wa vijana kwa kuhamasisha uanzishwaji wa atamizi (incubations) katika Vyuo vikuu vya Tumaini (Kiota Hub), Nelson Mandela, Sokoine, Dodoma, Zanzibar, na miji ya Sengerema na Moshi (Kili Hub). Kupitia atamizi ya TEHAMA ya Dar es Salaam (DTBi), kampuni changa 25 zimeanzishwa, 14 zikiwa kwenye jengo la COSTECH na nyingine 11 zikiwa kwenye maeneo tofauti zikijikita katika maeneo ya: *software development; mobile payment systems; microfinance, na back-up & recovery*. Kupitia Ukumbi wa Ubunifu (Buni Innovation Space), COSTECH imezisaidia kampuni changa 43 kupitia programu ya *mentorship* na kusaidia kuboreshwa kwa

mawazo bunifu saba (7) ambayo ni: Maoni App, Kodi Yangu, Fuel-Less generator, Smart Mtaa, Ungane App, Fedha Zetu na D-pay. Kati ya mawazo haya saba, manne (Maoni App, Kodi Yangu, Smart Mtaa na Fedha Zetu) kwa sasa yanatumika na wahitaji wanaweza kupakua kupitia simu za viganjani.

## C. Elimu ya Juu

### (a) Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Katika mwaka 2016/17 Shilingi bilioni 483.79 zilitengwa kwa ajili ya mikopo na ruzuku kwa wanafunzi 122,374 ikijumuisha wanafunzi 28,094 wa mwaka wa kwanza na 94,280 wanaoendelea na masomo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 427.55 zilitokana na mfuko mkuu wa Serikali na Shilingi bilioni 56.24 zilitokana na marejesho kutoka kwa wanufaika wa mikopo. Vile vile, urejeshaji wa mikopo umeendelea kuimarika katika kipindi hiki ambapo hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya Shilingi bilioni 76.01 zimekusanywa ukilinganisha na Shilingi bilioni 30.27 zilizokusanywa kwa mwaka mzima wa 2015/16, hii ni takribani asilimia 151.14 ukilinganisha na mwaka 2015/16. Hadi Mei, 2017 kiasi cha Shilingi bilioni 401.86 kimetolewa kwa wanafunzi 122,374 ambapo wanafunzi 28,094 ni wapya na wanafunzi 94,280 wanaoendelea na masomo. Aidha, kati ya fedha hizo zilizotolewa, Shilingi bilioni 395.69 ni mikopo kwa wanafunzi 121,882 na Shilingi bilioni 6.17 ni ruzuku kwa wanafunzi 492.

### (b) Upanuzi wa Taasisi za Elimu ya Juu

Msukumo pia umewekwa katika kupanua fursa za elimu ya juu na ufundi kwa kujenga miundombinu ya vyuo ikijumuisha madarasa, vyumba vya mihadhara, karakana na maabara. Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizotekelezwa ni:-

**(iii) Ujenzi, Upanuzi na Ukarabati Miundombinu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:** Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo ujenzi na kukarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, kituo cha polisi, nyumba za wahadhiri na miundombinu ya mfumo wa maji taka. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa hosteli mpya sita (6) za ghorofa nne (4) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,840; kukamilika kwa asilimia 98 ya ukarabati wa hosteli ya Kijitonyama na ununuzi wa samani na kuanza kutumika; kukamilika kwa ukarabati wa mabweni 6; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba nane (8) za wafanyakazi; na ukarabati wa miundombinu ya majitaka katika eneo la Kitivo cha Uhandisi na Teknolojia.

**(iv) Upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa miundombinu ya vituo vya chuo kwa mikoa (7) ya Geita, Ruvuma, Rukwa,

Kilimanjaro, Singida, Mara na Pwani. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya kituo cha Geita; ukarabati wa miundombinu ya kituo cha Mwanza bado unaendelea; na matengenezo madogo madogo yamefanyika katika majengo ya makao makuu ya Chuo, Bungo - Kibaha na majengo ya makao makuu ya muda ya Chuo Kinondoni - Dar es Salaam.

(v) **Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ardhi:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa maabara na ukarabati wa hosteli za wanafunzi awamu ya sita. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa michoro ya usanifu majengo ya jengo la ardhi na uhandisi; kukamilika kwa michoro ya awali ya usanifu majengo na kufanyika kwa uchunguzi wa udongo (Soil Test) eneo la ujenzi wa mabweni ya wanafunzi; na kukamilika kwa michoro ya awali ya usanifu majengo na kufanyika kwa uchunguzi wa ardhi eneo la ujenzi wa maabara ya matumizi mbalimbali (Multi Purpose Laboratory). Kuboreshwa kwa zahanati iliyopo kuwa kituo cha afya, ununuzi wa samani na vifaa vya ofisi, na kukamilisha ukarabati wa majengo matano (5) ya hosteli na madarasa 57.

(vi) **Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuhakikisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ikiwemo vyumba vya mihadhara, maabara, na vyumba vya kompyuta. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa moja (1) linalojumuisha Ofisi, vyumba vya Semina, madarasa na maabara za Kompyuta katika Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ukaa Nchini (National Carbon Monitoring Centre) kwa ufadhili wa Serikali ya Kifalme ya Norway; kukamilika kwa asilimia 99 ya ujenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Utafiti wa Afya ya Mazingira na Viumbe Maji (African Centre for Health of Acquatic Resources - ACHAR) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Norway (NORAD).

#### 3.2.2.3.2 Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii

#### (a) Mipango ya Afya na Uendeshaji

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya tathmini ya vituo vya kutolea huduma pamoja na kubaini mchango wa Serikali kwa miradi inayotekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) pamoja na utekelezaji wa mipango ya afya na uendeshaji inayofadhiliwa na Mfuko wa Afya wa Pamoja. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni Kukamilika kwa tathmini ya ubora wa vituo vya kutolea huduma na kutoa nyota kwa vituo husika kutokana na uwezo wake; na

Kupanua Community Score Card katika mikoa 6 ya BRN na kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 - 2017.

**(b) Mradi wa Kupunguza Vifo vya akina Mama Vinavyotokana na Uzazi**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kugharamia kazi mbalimbali zinazotekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Pamoja wa Afya, kutekeleza Mradi wa Malipo kwa Ufanisi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na uimarishaji wa mifumo ya afya nchini (Heatlh Systems Strengthening). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kutolewa kwa mafunzo ya utekelezaji wa mpango wa Malipo kwa Ufanisi kutoka katika ngazi ya jamii hadi Makao Makuu ya Halmashauri; Kutoa motisha (*Startup Funds*) kwa mikoa ya Mwanza, Pwani na Shinyanga; na kutolewa kwa *matching fund* ya CHF pamoja na uhakiki wa matokeo ya viashiria vya ufanisi katika sekta ya afya kulingana na makubaliano ya wadau wa maendeleo.

**(c) Hospitali ya Rufaa Mbeya**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za X-Ray na kununua vifaa tiba. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kunuliwa kwa mashine za kisasa za maabara (Cobas Machine), *histopathology*, kutolea dawa ya usingizi, vipimo vya damu (hermatology) na kuendelea na ujenzi wa jengo la radiolojia.

**(d) Taasisi ya Saratani Ocean Road**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa vyumba vya kuweka vifaa vya mionzi (Bunkers) na ununuzi mitambo ya tiba ya saratani. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya kuweka vifaa vya mionzi (Bunkers) na kuendelea na taratibu za ununuzi wa mitambo ya *LINAC 1* na *CT Simulator* ili kuwezesha mashine hizi kufungwa.

**(e) Mradi wa kuimarisha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi Hospitali za Rufaa**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kupelekwa kwa Shilingi bilioni 112.2 Bohari ya Dawa kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini; ukusanyaji wa damu salama; na kuboreshwa kwa upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini.

**(f) Hospitali ya Taifa Muhimbili**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ununuzi wa vifaa tiba na kujenga mfumo wa kujikinga. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ukarabati wa wadi 5 za *ICU*; kununuliwa kwa mashine 14 za upasuaji

(Diathermy Machines), mashine 2 za utakasishaji vifaa; mashine 1 ya *CT-Scan* yenye uwezo wa "slice" 128; ukarabati wa mashine za *ventilators*, monitors na anaesthesia; kuanzishwa kwa uchunguzi na tiba ya homa sugu ya ini; kukamilika kwa ukarabati wa wadi ya Sewahaji Na. 18 yenye vitanda 13 kwa ajili ya wagonjwa wa kulipia; na kuanzishwa kwa huduma za kuchangia damu katika jamii hatua ambayo imepunguza ukosefu wa damu hospitalini.

**(g) Hospitali ya Rufaa ya Bugando**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ununuzi na usimikaji wa vifaa tiba. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ukarabati wa kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la saratani, na ujenzi wa kliniki wa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na kununuliwa na kusimikwa *CT-Scan Simulator*.

**(h) Hospitali ya Rufaa ya KCMC**

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha tiba za saratani awamu ya kwanza kati ya nne; kukamilika kwa ujenzi wa wodi mpya kwa ajili ya wagonjwa walioungua moto na kemikali zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 24 kwa wakati mmoja; na kununuliwa na kusimikwa mashine 4 za kusafisha figo.

**(i) Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa wodi na kununua vifaa tiba. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni ununuzi wa mashine ya kupima usugu wa vimelea vya kifua kikuu kwa dawa daraja la pili hivyo kupunguza muda wa uchunguzi wa kifua kikuu hadi chini ya siku 90.

**(j) Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kutoa mchango wa Serikali kwa Shirika la GAVI linalohusika na ununuzi wa chanjo. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ununuzi wa chanjo ambazo hutolewa kwenye vituo vya kutolea huduma kwa ajili ya kukinga magonjwa mbalimbali hususan kwa watoto na akina mama; kuendelea na hatua mbalimbali za udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza kwa kuhamasisha kampeni ya usafi wa mazingira ambapo ilinunua magari, pikipiki 70 na trekta ya kuzolea taka kwa ajili ya zawadi ya Halmashauri zitakazofanya vizuri katika usafi wa mazingira; na kuandaa mwongozo wa maji na usafi wa mazingira katika vituo vya kutolea huduma za afya.

#### 3.2.2.3.3 Maji Safi na Majitaka

**(a) Ujenzi wa Mfumo wa Maji taka katika Jiji la Dar es Salaam**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya kuboresha huduma ya maji taka kwa Jiji la Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa usanifu wa ujenzi wa miundombinu ya

kuondosha majitaka na ujenzi wa mitambo mipya ya kusafisha majitaka itakayojengwa maeneo ya Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach.

**(b) Miradi ya Maji ya Kitaifa**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha miundombinu ya usambazaji maji nchini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa usambazaji wa maji katika vijiji vya Mihuga, Masimbani, Kweikonje, Mandamazingara, Mkange, Kwan'gandu, Pongwe Kiona, Kifuleta, na Kwaruhombo katika awamu ya pili ya mradi wa Chalinze. Kukamilika kwa shughuli za ukarabati miundombinu ya maji, ununuzi wa pampu za maji, mabomba na kugharamia umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kusukuma maji katika miradi ya maji ya Makonde, Wanging'ombe na Handeni Trunk Main.

**(c) Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Huduma za Maji Mijini**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni Ujenzi wa miradi 7 ya kuboresha huduma ya maji katika mikoa ifikapo Desemba 2018. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya maji katika miji ya Sumbawanga, Kigoma, Lindi, Musoma, Bukoba, Tabora na Arusha; na Miradi katika miji hiyo ipo katika hatua mbalimbali za kiutekelezaji na mingine inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha.

**(d) Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Huduma za Maji Vijijini**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga miundombinu ya maji na vituo vipya 631 vya maji vijijini katika mkoa wa Tabora; kujenga miundombinu ya usambazaji maji Njombe vijijini, Urambo, Singida vijijini, Mbulu, Babati, Iramba na Kilosa; na kujenga miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya mkoa wa Morogoro. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa miradi mipya 1,160 ya maji katika vijiji 1,206 yenye vituo vya kuchotea maji 28,499 katika Halmashauri 148; na kusajiliwa kwa jumuiya 909 za watumia maji. Kuboreshwa kwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi milioni 21.9 sawa na asilimia 72.

**(e) Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Kahama – Nzega – Igunga –Tabora – Sikonge**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji kutoka ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama, Nzenga na Tabora umekamilika ifikapo mwaka 2019. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa usanifu wa ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya miradi ya maji kwa miji ya Tabora, Igunga na Nzega; na kukamilika kwa upimaji na usanifu katika vijiji 32 pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga.

### (f) Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha miradi 4 ya kuboresha huduma ya maji kwa jiji la Dar es Salaam kupitia Mpango Maalum ifikapo mwaka 2018. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa usanifu wa bwawa na barabara kutoka Kidunda hadi Ngerengere (km 75); malipo ya fidia kiasi cha Shilingi bilioni 7.85 kwa wananchi 2,603 kupisha mradi katika maeneo ya vijiji vya Kwanyagongo, Kwatupa, Kariakoo, Bwira chini, Bwira juu, Vikonge na Mikoroshini; kupimwa kwa viwanja 1,000 kwa ajili ya makazi na kugawiwa kwa wakazi watakaopisha mradi wa ujenzi wa bwawa hili; na kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya shule, zahanati na ofisi ya kijiji pamoja na baraba ya kuingia kwenye viwanja.

### (g) Mradi wa Maji Same - Mwanga – Korogwe

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha maji na miundombinu ya usambazaji maji katika miji ya Same, Mwanga, Korogwe pamoja na vijiji 38 vilivyopo kando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa asilimia 15.8 ya ujenzi wa chanzo, mtambo wa kusafisha maji na tanki kubwa la kuhifadhi maji kwa ajili ya usambazaji.

### (h) Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kupeleka Mtwara-Mikindani

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha mradi wa kutoa maji katika mto Ruvuma kwenda Mtwara Mjini (Mikindani) ifikapo mwaka 2020. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa usanifu wa mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara - Mikindani na vijiji 26 pamoja na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu.

**(i) Mradi wa Uendelezaji na Utunzaji wa Rasilimali za Maji Pamoja na Ubora wa Maji:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kutambua, kutunza, kuendeleza na kulinda vyanzo vya maji nchini dhidi ya uchafuzi kila mwaka. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kuendelea kwa ujenzi wa ofisi za Mabonde ya Maji za Kigoma, Tabora na Kahama ambapo umefikia wastani wa asilimia 97; kutambuliwa kwa maeneo mapya 272 ambapo maeneo 9 yamewekewa mipaka; na kujengwa kwa jumla ya vituo 12 na kukarabati vituo 23.

**(j) Mradi wa Maji wa Ruvu Chini – Pwani**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha miradi 4 ya kuboresha huduma ya maji kwa jiji la Dar es Salaam kupitia Mpango Maalum ifikapo mwaka 2018: Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ulazaji wa bomba la kusafirisha maji kutoka mtambo wa Ruvu Chini (Bagamoyo) hadi Dar es Salaam (km 55.38) ambapo upanuzi huu umeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 180 hadi lita milioni 270 kwa siku.

**(k) Mradi wa Maji wa Ruvu Juu – Pwani:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika jiji la Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa upanuzi wa chanzo cha maji eneo la Ruvu Darajani; kukamilika kwa ulazaji wa mabomba makuu yenye urefu wa kilomita 40.01 kutoka Mlandizi hadi Kimara; na kukamilika kwa ujenzi wa tanki jipya la Kibamba. Mradi huu upo katika hatua za majaribio ambapo umeongeza uwezo wa uzalishaji wa maji kutoka lita za ujazo milioni 82 hadi milioni 196 kwa siku na kunufaisha wakazi wa maeneo ya Mlandizi, Kibaha, Kibamba, Kiluvya, Kinyerezi, Mbezi, Kimara, Changanyikeni, Segerea, Vingunguti, Airport, Ukonga, Kibangu, Makuburi na Kipawa.

**(l) Mradi wa Visima Virefu vya Kimbiji – Dar es Salaam na Mpera – Pwani:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika jiji la Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa uchimbaji wa visima sita (6) na kufanya idadi ya visima vilivyokamilika kuwa 15 kati ya visima 20 vya uzalishaji maji; na kukamilika kwa uchimbaji wa visima saba (7) vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi katika mwamba wa Kimbiji na Mpera maeneo, Mkuranga, Mwasonga, Kibada, Buyuni, Changani na Nzasa – Chanika.

### 3.2.2.3.4 Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

**(a) Programu ya Kukuza fursa za Ajira na kuwezesha Kiuchumi:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kubaini ajira zenye tija kwa wananchi ili kuiwezesha serikali kutunga sera, sheria na miongozo katika kukuza na kuboresha ajira nchini hususan kwa watu wenye ulemavu. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya Shilingi 1,469,358,000 kwa vikundi vya vijana 297 vyenye wanachama 1,485 kutoka katika Halmashauri 66 za Mikoa ya Tanzania. Vile vile, katika vikundi hivyo vipo vikundi 3 vya watu wenye ulemavu kutoka kwenye Halmashauri za Korogwe, Ulanga na Meru, kutolewa kwa mafunzo ya ujasiliamali kwa vijana 3,222 na mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana 8,838. Kuhuisha Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 ili kutoa fursa zaidi katika kukuza ajira kwa vijana na kuandaa Kanuni za Sheria ya Baraza la Taifa la Vijana.

**(b) Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuratibu programu ya kukuza ujuzi na stadi za kazi katika viwanda, kilimo-biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA na madini hususan mafuta na gesi. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kutoa mafunzo kwa vijana 1,000 kati ya 3,000 katika ushonaji wa nguo kupitia viwanda vya Tooku-DSM na Mazava Morogoro ambapo vijana 950 wameajiriwa; vijana 100 kati ya 1000 wameanza mafunzo ya kutengeneza bidhaa za ngozi kwenye Chuo cha DIT – Mwanza. Kuanzia mwezi Machi, 2017 vijana 4,300 wataanza mafunzo ya kurasimisha

ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa elimu yatakayoendeshwa na VETA katika fani za utalii, ujenzi, ufundi umeme na ufundi makenika; kutoa mafunzo ya uanagenzi kwa vijana 4,600; kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu 4,000; kutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 13,400 waliopo makazini na kuimarisha mfumo wa taarifa za soko la ajira na vituo vya huduma za ajira pamoja na kukamilika kwa miongozo ya mafunzo kwa vitendo na uanagenzi (Internship and Apprenticeship Training Frameworks).

**3.2.2.3.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**(a) Mradi wa Kuimarisha Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kufungwa mitambo mipya ya kupoozea studio tano (5) za Redio zilizopo katika jengo la utangazaji barabara ya Nyerere na kufanyiwa majaribio; kupatikana kwa mzabuni wa kufunga vifaa vya mtambo wa kurusha matangazo ya redio na televisheni kwa njia ya Satelaiti (Satellite Uplink) ambaye ameanza kazi na kuagiza vifaa vipya kutoka nchini Israeli; mitambo ya redio imefungwa mkoani Geita na kuwezesha usikivu wa matangazo ya fm kwenye masafa 87.7 MHz (TBC Taifa) na 89 MHz (TBC fm) Geita Mjini, Bukombe, Chato na Kahama.

**(b) Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukarabati jengo la ofisi ya programu. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwea ukarabati wa Jengo la Makumbusho ya Jeshi linalotumiwa kwa sasa kama ofisi za programu ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika; na kukamilika kwa maandalizi ya Mpango Mkakati wa uendeshaji wa programu.

**(c) Mradi wa Eneo Changamani la Michezo la Taifa:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuimarisha miundombinu mbalimbali ya uendeshaji wa eneo Changamani la Michezo. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa taratibu za manunuzi ya matengenezo ya mifumo ya umeme na maji; vifaa vya TEHAMA; vipuli vya jenereta; na ununuzi na matengenezo ya viyoyozi.

**(d) Mradi wa Ukarabati wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuimarisha miundombinu ya kufundishia katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika maeneo ya teknolojia ya sauti, muziki ubunifu, pamoja na uzalishaji wa picha jongevu. Vile vile, TaSUBa imepkea msaada wa vifaa vingine vya kufundishia ikijumuisha kompyuta, ala za muziki na vyombo vya sauti kutoka Serikali ya Denmark.

**(e) Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Maonyesho ya Sanaa:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa ukumbi wa wazi wa maonyesho ya sanaa. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya kukaa watazamaji; kukamilika kwa ujenzi wa ofisi na ukumbi mdogo wa mikutano na mafunzo; kukamilika kwa ujenzi wa vyumba vya wasanii kwa ajili ya kujiandaa wakati wa maonyesho; kukamilika kwa ujenzi wa ofisi za wasimamizi/waendeshaji wa mitambo ya ukumbi; kukamilika kwa ujenzi wa nguzo, paa, ujenzi wa miundombinu ya umeme na maji safi na maji taka.

### 3.2.2.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

Uchumi wa viwanda unahitaji miundombinu ya kutosha, uhakika na bei nafuu. Unahitaji pia mfumo thabiti wa sera na mfumo wa kodi kuhakikisha utabirifu wa mazingira ya uendeshaji biashara. Maamuzi ya uwekezaji hayawezi kuwa ya haraka na uhakika kwani muda ni nyenzo muhimu katika ushindani. Lakini pia unahitaji msingi thabiti wa mfumo na miundo-taasisi. Kwa kuzingatia haya hatua zifutazo zimezingatiwa:-

#### 3.2.2.4.1 Miundombinu

**A. Reli**

**(a) Kubadilisha mataruma ya reli kwa kuweka reli nzito**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kufanya malipo ya awali ya mikataba ya kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi kati ya Lulanguru na Tabora (km 61); kubadilisha km 283 za reli ya kati sehemu ya Dar es Salaam - Kilosa na Tabora-Isaka (km 130); malipo ya awali ya kununulia vipuri vya mtambo wa kuzalisha kokoto wa Tura; ununuzi wa mtambo wa kukagua na kupima njia ya reli; na shughuli za uzalishaji wa mataruma katika Karakana ya Pugu. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa tathmini na usanifu (field assessment and design) ambapo makabrasha ya zabuni yameandaliwa kwa ajili ya kuwapata makandarasi wa kufanya kazi hiyo; ukarabati wa njia ya reli kwa kutandika reli ya ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni ya Mpiji na soga kilometa 12 unaendelea; kazi ya kufunga vipuri kwenye mitambo ya mgodi wa kokoto wa Tura imekamilika; na kiwanda cha kunyoosha mataruma ya reli yaliyopondeka kilichopo Pugu DSM kimeboreshwa na sasa kina uwezo wa kuzalisha hadi mataruma 400 kwa siku kwa *shift* moja.

**(b) Ukarabati na Ununuzi wa Vichwa vya Treni na Mabehewa**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na uzalishaji upya wa injini za treni katika karakana ya Morogoro; ukarabati wa viberenge na treni za kufanya ukaguzi wa reli; na kukamilisha ununuzi wa mabehewa 22 ya mizigo. Hatua iliyofikiwa ni: uundaji wa mabehewa 7 ya abiria na mabehewa ya mizigo 120 na vichwa viwili (2) vya treni.

**(c) Ukarabati na Uboreshaji wa Matawi ya Reli ya Kati:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kutandika reli katika njia ya reli ya Kaliua – Mpanda (km 185) na kujenga daraja moja na makalavati matatu (km 154, km 162, na km 174); na ukarabati wa stesheni na ujenzi wa jengo la kuhifadhia mizigo katika stesheni ya Mpanda. Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa ukarabati njia ya reli ya Mpanda eneo la kutoka stesheni ya Ugalla River hadi stesheni ya Katumba yenye umbali wa kilometa 15 kwa kuondoa reli za ratili 45 na 50 kwa yadi na kuweka reli za ratili 60 kwa yadi.

**(d) Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli:**

Mradi unalenga kukarabati miundombinu na mawasiliano katika njia kuu ya reli ya kati ili kuboresha ufanisi. Katika mwaka 2016/17, zimetengwa Shilingi bilioni 70.7 fedha za ndani na bilioni 11 fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu unaohusisha:-

(i) Ujenzi wa daraja na matengenezo ili kuzuia tatizo la mafuriko katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya stesheni za Godegode na Gulwe. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na kazi ya kudhibiti eneo linaloathirika mara kwa mara na mafuriko kati ya Kilosa – Gulwe na kujenga daraja na matengenezo ya stesheni za Kilosa na Gulwe;

(ii) Ujenzi wa madaraja 10 kati ya 38 yaliyo katika hali mbaya katika njia ya Tabora – Kigoma. Utekelezaji upo katika hatua ya kumpata mkandarasi;

(iii) Usanifu na kuanza ujenzi wa madaraja na makalavati 38 yenye uwezo wa tani 25 yaliyo katika hali mbaya kati ya Dar es Salaam – Isaka. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa tathmini, usanifu (Field survey and design) na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumwajiri mkandarasi kati ya Dar na Kilosa na kuwasilishwa Benki ya Dunia. Tangazo la kuwaalika wazabuni litatolewa mara baada ya Benki ya Dunia kutoa kibali;

(iv) Kujenga daraja katika eneo la Godegode. Katika utekelezaji wa mradi huu imeamuliwa kuwa usanifu wa suluhisho la kudumu utafanyika kupitia mkandarasi wa SGR, hivyo imeamuliwa kusitisha mpango wa awali na RAHCO wanajenga kalvati la muda la chuma;

(v) Kuboresha mfumo wa mawasiliano (awamu ya kwanza) kati ya Dar es Salaam – Dodoma, Tabora – Kigoma, Tabora- Mwanza na Kaliua – Mpanda. Tathmini ya zabuni inaendelea kufanyika;

(vi) Kuweka mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia mizigo katika reli (Electronic cargo tracking system). Mfumo umejengwa kutoka Dar-Morogoro na majaribio ya utendaji wa mfumo (commissioning) uliowekwa yamekamilika ili kujiridhisha na viwango vya ujenzi. Kazi ya kusambaza mfumo huo kwenye njia nyingine za mtandao wa reli inaendelea; na

(vii) Ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika eneo la Godegode - Gulwe na Msagai

(km 384). Maandalizi ya makabrasha ya zabuni ya kumpata mshauri mwelekezi yamekamilika. Hata hivyo, mradi huu imeamuliwa kuwa usanifu wa suluhisho la kudumu ufanyike kupitia mkandarasi wa SGR.

**(e) Ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha usanifu wa kina wa ujenzi wa njia ya reli kati ya Tanga – Arusha; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli kwa kiwango cha standard gauge kati ya Arusha – Musoma, pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu; kuweka mawe 27,070 ya mipaka katika njia na stesheni za reli; na kupima viwanja vya reli na kuweka alama na uzio katika maeneo hayo. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali sehemu ya Tanga – Arusha; na kwa sehemu ya Arusha – Musoma, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali ipo katika hatua za mwisho.

**(f) Mradi wa Reli Mtwara – Mbamba Bay na Mchuchuma – Liganga;** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali; na kumpata mtalaam Elekezi atakayesimamia upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa reli; taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kumwajiri Mshauri wa Uwekezaji (Transaction Advisor) atakayesaidia upatikanaji wa fedha zinaendelea.

**(g) Usafiri wa Treni Dar es Salaam**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli zikiwemo za maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo; na ujenzi wa mchepuo wa njia ya reli kutoka "Ilala block post" hadi Stesheni ili kuepusha mwingiliano wa treni ya abiria kutoka Stesheni kwenda Ubungo na ile ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia mpya za reli unaofanywa na kampuni ya GIBB kutoka Afrika ya Kusini; na ujenzi wa mchepuo wa njia ya reli kutoka "Ilala block post" hadi Stesheni. Kazi hii ipo chini ya mradi wa Tanzania Intermodal Rail Project (TIRP) ambapo usanifu wa kina unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha.

**B. Miundombinu ya Barabara na Madaraja**

**(a) Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuanza ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi yenye urefu wa kilomita 50. Mradi huu uko katika maandalizi ya awali ya kuanza ujenzi ambapo mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) umesainiwa. Mkandarasi ameanza maandalizi (mobilization) ya ujenzi wa barabara hiyo.

**(b) Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 359):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tabora – Sikonge – Ipole (Sehemu ya Tabora – Usesula, km 30); na kulipa fidia sehemu ya Mpanda – Koga – Ipole. Hatua iliyofikiwa ni: kujenga tuta la barabara km 3.5; tabaka la chini la msingi km 7.58; makalvati makubwa 2; Makalvati madogo 6 ambapo kiujumla ujenzi umefikia asilimia 27.5; na Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Tabora (Usesula) – Sikonge – Ipole – Koga – Mpanda ambazo zilikuwa zimetangazwa zimesitishwa kwa muda ili kukamilisha mapitio ya usanifu.

**(c) Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa (km 528):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kulipa sehemu ya madai ya makandarasi waliojenga barabara za Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya; ujenzi wa barabara ya Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya umekamilika na malipo ya madai ya makandarasi husika yamelipwa. Kwa upande wa sehemu ya Itigi – Mkiwa - Noranga (km 50) taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea.

**(d) Kuanza ujenzi wa sehemu za Chunya – Makongolosi na Itigi – Mkiwa (km 36):** Lengo lilikuwa ni kuanza ujenzi wa sehemu za Chunya – Makongolosi na Itigi – Mkiwa (km 36). Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36) umekamilika. malipo ya madai yamekamilika kwa sehemu za Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya. Aidha, tarataibu za kuwapata makandarasi wa ujenzi kwa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 43) na Mkiwa – Itigi – Noranga (km 56.9) zinaendelea.

**(e) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7**): Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu za Tabora – Nyahua na Manyoni – Itigi – Chaya; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya na sehemu ya Tabora – Nyahua imekamilika kwa asilimia 95 ambapo km 78.33 zimekamilika kwa kiwango cha lami; kutangazwa kwa zabuni za kupata mkandarasi wa ujenzi na Mhandisi Msimamizi wa sehemu ya Nyahua – Chaya. Hata hivyo hatua hiyo ilisimamishwa baada ya nchi ya Kuwait kuonyesha nia ya kufadhili mradi huu. Taratibu za kusaini mkopo zinaendelea kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait.

**(f) Barabara ya Dodoma – Babati (km 261):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Dodoma – Mayamaya, Mayamaya – Mela na Mela – Bonga. Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi sehemu ya Dodoma – Mayamaya(km 43.65) na Bonga – Babati (km 19.2)

umekamilika. Mayamaya – Mela (km 99.35) ujenzi wa tabaka la lami km 79.5 na makalavati makubwa 5 na madogo 10 umekamilika kwa asilimia 82.23. Mela – Bonga (km 88.80) ujenzi wa tabaka la lami km 67.5 na makalavati madogo 37 umekamilika kwa asilimia 75.81.

**(g) Barabara ya Iringa – Dodoma (km 260):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni**:** Kulipa sehemu za madai ya makandarasi wa barabara ya Migori – Fufu *Escarpment*, Iringa-Migori na Fufu *Escarpment* – Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Iringa *bypass*. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa mradi na sehemu ya madai ya makandarasi wa barabara ya Migori – Fufu *Escarpment* na Iringa-Migori amelipwa.

**(h) Barabara ya Masasi - Songea – Mbambabay (km 868.7):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa sehemu za (Mangaka – Nakapanya, Nakapanya – Tunduru, Mangaka – Mtambaswala, na Tunduru – Matemanga); na kuanza ujenzi wa sehemu za Mbinga – Mbambabay na Masasi – Newala – Mtwara. Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa sehemu za Mangaka – Nakapanya, Nakapanya – Tunduru, Mangaka – Mtambaswala, na Tunduru – Matemnanga umekamilika; kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi kati ya Serikali na mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Masasi – Newala – Mtwara (km 209); sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) mkandarasi yuko kwenye kipindi cha maandalizi ya ujenzi; na kwa upande wa barabara ya Mbinga – Mbamba bay (km 67), Mhandisi Mshauri anaendelea na mapitio ya usanifu wa kina kabla ya kutangaza zabuni za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**(i) Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo - Mto wa Mbu (km 338):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Sanzate na kuanza ujenzi Mto wa Mbu – Loliondo. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya tuta la barabara km 34.4 na ujenzi wa daraja moja na makalavati 33 na kuanza kwa maandalizi ya kuanza ujenzi wa tabaka la lami kwa sehemu ya barabara ya Makutano – Sanzate (km 50). Kutangazwa kwa zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Natta – Mugumu ( km 30); Loliondo (Sale Junction) – Wasso (km 50).

**(j) Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (Km 491):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Ndono – Urambo na Kaliua – Kazilambwa; na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Uvinza – Malagarasi na Urambo – Kaliua. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Ndono – Urambo (km 51.98). Kwa barabara ya Kaliua – Kazilambwa (km 56), utekelezaji kufikia asilimia 90.4;

ujenzi wa makalavati makubwa kumi (10) na madogo 74 umekamilika. Kwa upande wa barabara ya Urambo – Kaliua, taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea ambapo mkataba unatarajiwa kusainiwa hivi karibuni. Kuhusu sehemu ya Uvinza – Malagarasi, zabuni zitatangazwa baada ya kusaini makubaliano na mfadhili (ABU – DHABI na OPEC).

**(k) Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17) na Bulamba – Kisorya (km 51):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukarabati wa barabara ya Nyangunge – Simiyu/Mara Boarder; kulipa madai ya mkandarasi wa Simiyu/Mara boarder – Musoma; kuendelea na kazi za ujenzi Kisesa – Usagara bypass na barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba); kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bulamba, Musoma – Makojo – Busekela, Makutano – Sirari na barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Mwanza. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border; kulipwa kwa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border; kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kisesa - Usagara (km 17); kwa upansde wa barabara ya Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba) kazi za kusafisha eneo la mradi zinaendelea na makalavati mawili (2) yamejengwa; na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Musoma - Makojo - Busekela (92km) zimekamilika.

**(l) Barabara ya Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 310):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu na Nyakanazi – Kibondo; na kukamilisha mapitio ya usanifu; na kuanza maandalizi ya ujenzi sehemu ya Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 210). Hatua iliyofikiwa ni: kwa Kidahwe – Kasulu, ujenzi wa tuta la barabara kwa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50) unaendelea ambapo km 6.92 zimejengwa; ujenzi wa makalvati madogo nane (8) na kubwa moja (1) umekamilika; kazi ya ujenzi wa sehemu ya Nyakanazi – Kibondo inaendelea ambapo km 9.2 za eneo la ujenzi limesafishwa na km 4 za tuta la barabara zimekamilika; na kuhusu maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 210), Mhandisi Mshauri anaendelea na mapitio ya usanifu wa kina ili uendane na viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**(m) Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang'ombe – Sanya Juu (Km 173), Arusha – Moshi – Holili (Km 140), KIA - Mererani (26), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (Km 16.0) na Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (Km 10.8):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kulipia sehemu ya malipo ya mwisho ya makandarasi wa barabara za Rombo Mkuu – Tarakea, Marangu – Rombo Mkuu, Ujenzi wa

barabara ya Kwa Sadala – Masama - Machame Jct, Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia na Mwika – Kilacha; Ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa za barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.10) na njia mbili kwa sehemu ya Arusha *Bypass* (km 42.41); na kuendelea na ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani; na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Sanya Juu – Kamwanga. Hatua iliyofikiwa ni: kulipwa kwa sehemu ya malipo ya mwisho ya makandarasi wa barabara za Rombo Mkuu – Tarakea na Marangu – Rombo Mkuu; kukamilika usanifu wa kina kwa barabara ya Kwa Sadala – Masama - Machame *junction* na barabara ya Kiborloni – Kiharara – Tsuduni– Kidia (km 10.8); kuendelea na kazi za ujenzi wa mradi wa barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.10) na njia nne kwa sehemu ya Arusha ambapo ujenzi umefikia asilimia 46.64; kuendelea na ujenzi wa barabara ya KIA – Mererani (26km) ambapo km 14 za tabaka la lami zimekamilika; na kuanza kwa maandalizi ya awali (mobilization) ya ujenzi wa barabara ya Sanya Juu – Kamwanga (km 32.2).

**(n) Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero (km 60):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kulipa malipo ya mwisho ya madai ya mkandarasi wa sehemu ya Isaka – Ushirombo pamoja na mkandarasi wa Rusumo *One Stop Border Post*; kuendelea na ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga; maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero; na maandalizi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari huku yakitembea (Weigh in Motion Scale) sehemu ya Nyakanazi (Kagera). Hatua iliyofikiwa ni: madai ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa sehemu ya Isaka – Ushirombo (km 132) yamelipwa; malipo ya mkandarasi wa Rusumo *International Bridge* na *One Stop Border Post* yamelipwa; kwa upande wa barabara za Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero, Mhandisi Mshauri anaendelea na mapitio ya usanifu wa kina ili uendane na viwango vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**(o) Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kassanga Port; na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya. Hatua iliyofikiwa ni: kazi za ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kassanga Port (112 km) zinaendelea ambapo km 75 za tabaka la lami zimekamilika; na kuendelea na mapitio ya Usanifu wa Kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ya ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50).

**(p) Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Hatua iliyofikiwa ni: kusainiwa kwa mkataba

wa Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usimamizi wa kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara (km 103.3); kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina; na kutangazwa kwa zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Kidatu – Ifakara.

**(q) Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 346.6):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuendelea na kazi za ujenzi sehemu za Sumbawanga – Kanazi (Km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kizi – Sitalike – Mpanda (km 95); na kuanza ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Mishamo (km 100). Hatua iliyofikiwa ni: Kazi za ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga – Kanazi (Km 75) zinaendelea ambapo km 53.3 za lami zimekamilika; sehemu ya Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6) km 64.4 za lami zimekamilika; sehemu ya Sitalike – Mpanda (km 36.9) imekamilika; na kusainiwa kwa mkataba wa Ujenzi wa barabara ya Mpanda – Mishamo (km 100); katika sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 30) umesainiwa ambapo mkandarasi yupo kwenye kipindi cha maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi.

**(r) Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.8)**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha malipo ya mwisho ya mkandarasi wa barabara ya Bariadi – Lamadi na kuendelea na ujenzi sehemu ya Mwigumbi – Maswa. Hatua iliyofikiwa ni: mradi wa barabara ya Bariadi – Lamadi (km 71.8) umekamilika na kufunguliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Januari, 2017; sehemu ya madai ya mwisho ya mkandarasi yamelipwa; kazi za ujenzi wa barabara ya Mwigumbi – Maswa (km 50.3) zinaendelea ambapo mkandarasi amekamilisha ujenzi wa km 23.28 za tuta la barabara na makalavati makubwa 4 na madogo 23; na maandalizi kwa ajili ya kutangaza zabuni ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7) yanaendelea.

**(s) Barabara za Mikoa:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: ukarabati wa jumla ya kilomita 632.05 kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilomita 23.25 kwa kiwango cha lami; na ujenzi wa madaraja 15. Hatua iliyofikiwa ni: kujengwa kwa kilometa 19 kwa kiwango cha lami na kukarabatiwa kwa kilometa 122.22 kwa kiwango cha changarawe.

**(t) Barabara za Kupunguza Msongamano Jiji la Dar es Salaam (km 111.85):** Mradi unalenga kujenga, kupanua na kukarabati barabara za jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Katika mwaka 2016/17, Shilingi bilioni 38.9 zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha ujenzi wa barabara za Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley –Jangwani/Twiga Jct (km 2.7); kumamilisha ujenzi wa barabara Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo Maziwa – External (km 2.25)

sehemu ya Tabata Dampo-Kigogo (km 1.65) na kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa eneo la Ubungo Maziwa – External; na kuendelea na ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 9), Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20 sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7) na Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6).

Hatua iliyofikiwa ni:

(i) Kukamilika kwa barabara za: Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Jct (km 2.7); Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo Maziwa – External (km 2.25) sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) na kulipwa kwa Sehemu ya madai ya Mkandarasi; Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 3 kutokea External); Mbezi (Morogoro Road) –Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Sehemu ya Kifuru – Kinyerezi (km 4); Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20) sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7); na Tangi Bovu – Goba (km 9).

(ii) Kuendelea na ujenzi kwa barabara za: Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14); Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20) sehemu ya Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba; na Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6).

**(u) *Flyover* ya TAZARA:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa *Flyover* ya TAZARA: Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi umeanza kwa kusafisha eneo la mradi kwa ajili ya kambi ya ujenzi, kuhamisha miundombinu ya maji na kulipa fidia kwa mali na wananchi na kujenga barabara. Kwa ujumla mradi umekamilika kwa asilimia 40.9.

**(v) *Flyover* ya Ubungo:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kufanya malipo ya awali ya mkandarasi wa ujenzi. Hatua iliyofikiwa ni: kundelea na ujenzi wa *flyover*. Hatua iliyofikiwa ni: kusainiwa kwa mkataba na mkandarasi wa ujenzi wa "*Ubungo Interchange*" na ujenzi ulizinduliwa na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Joseph Pombe Magufuli Machi 2017.

**(w) Maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela na Kawawa/Morocco:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kufanya maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco. Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea kwa majadiliano ya awali ya mkataba na Mhandisi Mshauri.

**(x) Barabara ya TAZARA – Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (km 6):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA kuwa njia 6. Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**(y) Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200) Sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144) kwa kiwango cha "Expressway" na mradi huu utahusisha ukarabati (overlay) kwa kiwango cha lami sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24). Katika mwaka 2016/17, zimetengwa Shilingi bilioni 12.77 kwa ajili ya: kukamilisha upembuzi yakinifu na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze km 144; na ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24). Hatua iliyofikiwa ni: Mtaalam Mwelekezi (Transaction Advisor) amewasilisha taarifa ya mwisho ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali pamoja na nyaraka za zabuni kulingana na taratibu za miradi ya PPP za kumpata mbia (Concessionaire). Aidha, kilometa mbili (2) za sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24 zimekarabatiwa.

**(z) Madaraja ya Barabara kuu:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa madaraja mbalimbali Nchini. Madaraja hayo ni: Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, Daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge, Daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto – Inyonga, Daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga – Manonga, Daraja la Ruhekei katika barabara ya Mbinga – Mbamba Bay, Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Momba kwenye barabara ya Sitalike – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo (Rukwa/Mbeya Border), Daraja la Simiyu kwenye barabara Mwanza – Musoma, Daraja la Wami barabara ya Chalinze – Segera, Daraja la Lukuledi II kwenye barabara Matama – Kitangali – Newala, Daraja Jipya la Selander na Daraja la Mlalakuwa. Hatua ziliyofikiwa ni pamoja na:

(i) kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Kilombero na Mbutu;
(ii) kuendelea na ujenzi madaraja ya Ruhuhu na Sibiti; na
(iii) madaraja ambayo yapo kwenye hatua za awali za utekelezaji: Simiyu (usanifu wa awali unaendelea); Ruhekei II (upembuzi yakinifu umekamilika); Selander (kuanza usanifu wa kina); Wami na Momba (kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza kwa taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi); na Mlalakuwa (maandalizi ya ujenzi yameanza).

**(aa) Daraja la Mwalimu Nyerere – Kigamboni:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha sehemu ya malipo ya mkandarasi wa ujenzi wa daraja na kuanza ujenzi wa barabara za maingilio. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa daraja na lilifunguliwa na Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19 Aprili 2016.

**C. Usafiri wa Majini**

**(a) Ununuzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu:** Mradi unalenga kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika mwaka 2016/17, Shilingi bilioni 50.5 fedha za ndani zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi; ambapo Shilingi bilioni 21 ni kwa ajili ya malipo ya awali (asilimia 50) ya kununua meli moja mpya katika ziwa Victoria; Shilingi bilioni 20 ni kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa meli ya MV Victoria, Shilingi bilioni 5.9 ni kwa ajili ya ukarabati meli ya MV Liemba katika ziwa Tanganyika; na Shilingi bilioni 3.6 ni kwa ajili ya ukarabati wa meli ya MV Butiama kwa ziwa Victoria. Taratibu za ununuzi wa meli mpya na ukarabati wa meli kwa ziwa Victoria unaendelea. Kwa upande wa matengenezo ya meli ya Mv. Liemba, mjenzi amepatikana ambaye ni M/S LEDA SHIPYARD na taratibu za kusaini mkataba zinaendelea.

**(b) Ujenzi wa maegesho ya vivuko**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: ujenzi wa maegesho na majengo ya abiria ya kivuko cha Dar es Salaam – Bagamoyo (Pwani); upanuzi wa Maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bwina ya Kivuko cha Chato – Nkome; na ujenzi wa maegesho ya Lindi – Kitunda. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za kusaini mkandarasi wa kujenga maegesho.

**(c) Ununuzi wa vivuko vipya:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ununuzi wa vivuko viwili (2) vitakavyofanya kazi kati ya Kigamboni – Magogoni na Kigongo – Busisi; ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA; na ununuzi wa boti za abiria katika vivuko vya Kilambo – Namoto na Mkongo – Utete. Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi kivuko eneo la Bandari *Dockyard*; kuendelea na taratibu za kusaini mkataba wa ununuzi wa kivuko kipya cha Kigongo – Busisi. Vifaa vya karakana za TEMESA, na boti za abiria kwa ajili ya vivuko vya Kilambo – Namoto na Mkongo – Utete hazitanunuliwa kutokana na uhaba wa fedha.

**(d) Ukarabati wa Vivuko:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II (Tanga), MV Sengerema, MV Mwanza, MV Geita, MV Kome, MV Nyerere, MV Misungwi na MV Ilagala. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa kivuko cha MV Pangani II; na kununuliwa kwa Engine moja (1) kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha MV Sengerema.

## D. Bandari

**(a) Ujenzi wa gati Na. 13 na 14, Bandari ya Dar es Salaam:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kujenga gati Na. 13 na Na. 14 katika bandari ya Dar es Salaam ili kuhudumia mizigo mingi kwa ufanisi zaidi. Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mtaalamu Mwelekezi atakayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa njia bora ya kuhamisha KOJ na usanifu wa ujenzi wa gati jipya la mafuta pamoja na kituo cha kuhifadhia mafuta (tank farm).

**(b) Uboreshaji wa gati Na. 1 – 7, Bandari ya Dar es Salaam:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1 – 7. Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa mkandarasi *China Habour Engineering and Construction (CRCC)* atakayefanya kazi hiyo.

**(c) Kina cha Bahari na Kupanua Lango la Kuingilia Meli:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuongeza kina cha Bahari na kupanua lango la kuingilia meli. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

**(d) Bandari Kavu ya Ruvu (Ruvu Dry Port):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam kuhudumia mizigo na kupunguza msongamano wa mizigo na malori bandarini . Hatua iliyofikiwa ni kutwaa eneo lenye ukubwa wa ekari 2000 kwa ajili ya Bandari Kavu, na kuanza ujenzi.

**(e) Ujenzi wa Bandari ya Mwambani – Tanga:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kuzingatia ujenzi wa reli mpya (Tanga – Arusha – Musoma). Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na maandalizi ya makabrasha kwa ajili ya marejeo ya upembuzi yakinifu ili zabuni iweze kutangazwa kabla ya Juni 2017. Aidha, maandalizi ya kujenga gati la Chongoleani (Tanga) kwa ajili ya kupokelea mafuta kutoka Uganda yanaendelea kwa kufanya upembuzi yakinifu.

**(f) Ujenzi wa bandari ya Mtwara:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuanza ujenzi wa gati moja (1) lenye urefu wa mita 350 kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko (Multi-Purpose Terminal). Hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa mkandarasi wa kazi ya ujenzi ambaye ni kampuni ya China Railway Construction (CRCC); na kuwekwa kwa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi kuanza tarehe 4 Machi, 2017 na Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Ujenzi wa gati hili utakamilika ndani ya miezi 21.

**(g) Ziwa Viktoria (Bandari za Maziwa Makuu):** Katika mwaka 2016/17,

shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: ujenzi wa Dhow Wharves ya Mwigobero; upimaji na utoaji fidia kwenye gati la Kyamkwikwi, Lushamba, na Ntama; ujenzi wa gati la Chato, uongezaji kina katika Bandari ya Nansio na Mwanza South na Ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu.

**(h) Ziwa Tanganyika (Bandari za Maziwa Makuu):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni uboreshaji wa maegesho ya meli (gati) za kuhudumia abiria pamoja na mizigo katika miji ya Lagosa, Sibwesa, pamoja na Kibirizi; upembuzi yakinifu katika bandari ya Karema pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara kuelekea katika bandari ya Kipili. Hatua iliyofikiwa ni ujenzi katika Gati ya Kalya/Sibwesa umefikia asilimia 50; na kuendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Karema.

**(i) Ziwa Nyasa (Bandari za Maziwa Makuu):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati la Mbamba Bay, ujenzi wa gati la Ndumbi na ujenzi wa sakafu (pavement) katika bandari ya Kiwira kwa ajili ya maegesho ya vifaa, mizigo na magari. Hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa gati la Ndumbi, umepangwa kuanza Mei 2017.

### E. Usafiri wa Anga

**(a) Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Julius Nyerere**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 65.

**(b) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa maegesho ya ndege, ukarabati na upanuzi wa barabara za viungio; ukarabati wa jengo la abiria; usimikaji wa taa za kuongozea ndege; na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka. Hatua iliyofikiwa ni: ukarabati wa maegesho ya ndege na barabara za viungio umefikia asilimia 80; usimikaji wa taa za kuongozea ndege asilimia 90; na ukarabati wa jengo la abiria asilimia 40.

**(c) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na majadiliano ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya marejeo ya usanifu wa kina.

**(d) Kiwanja cha Ndege Mwanza**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na kuendelea

na kazi za kurefusha na kujenga barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo terminal), maegesho ya ndege na viungio vyake, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua. Hatua iliyofikiwa ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo na maegesho yake pamoja kazi za kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege umeanza.

**(e) Kiwanja cha Ndege Kigoma:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka); usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio; na ujenzi wa jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Hatua iliyofikiwa ni kutangazwa upya kwa zabuni baada ya gharama za awali kuwa juu.

**(f) Kiwanja cha Ndege Tabora:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa jengo la abiria na barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari; ukarabati wa njia ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, maegesho ya ndege; na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kufanya majadiliano na hatimaye kusaini mkataba wa kazi.

**(g) Kiwanja cha Ndege Mtwara:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha usanifu na Mpango Kabambe (Concept Design & Master Plan) na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege; na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na kazi ya kufanya usanifu na kuandaa mpango kabambe; kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege; na kukamilika kwa maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya ukarabati wa uwanja.

**(h) Kiwanja cha Ndege Sumbawanga:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na kulipa fidia. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi.

**(i) Kiwanja cha Ndege Geita:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwanja na kuanza ujenzi. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi za usanifu na kuanza kazi za ujenzi.

**(j) Kiwanja cha Ndege Shinyanga**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; na kulipa fidia. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za kufanya majadiliano na hatimaye kusaini mkataba wa kazi.

## F. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**(a) Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kufunga alama za majina ya mitaa na namba za nyumba kwa Kata 100 za Mikoa ya Dar-es-Salaam, Mwanza, Zanzibar na Mbeya; kuhamasisha na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu mradi na faida za matumizi ya anuani za makazi na simbo za posta; kuendesha programu za kujengea uwezo watumishi kuhusu masuala ya matumizi ya anuani za makazi; na kuwezesha mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta pamoja na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta na ufuatiliaji wa utendaji kazi wa mfumo wa Taifa anuani za makazi na simbo za posta. Hatua iliyofikiwa ni: kuwekwa kwa majina kwa mitaa na barabara ambayo haikuwa na majina katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Visiwani Zanzibar; kufanyika kwa uhamasishaji wa wananchi na kupewa elimu kuhusu faida za matumizi ya anuani za makazi na simbo za posta katika Manispaa ya Dodoma na Halmashauri ya Chamwino; Kazi ya kujenga uwezo na uelewa kwa watumishi imefanyika katika halmashauri za mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora; na kutokana na mtirirko mdogo wa fedha, kazi ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta pamoja na maandalizi ya mkakati wa utekelezaji wake haikufanyika.

**(b) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni tathmini ya hali ya miundombinu ya mkongo na mifumo yake ili kubaini fursa za kufanya upanuzi wa miundombinu siku za usoni; tathmini ya athari za kimazingira katika maeneo ambayo awamu za III, IV na V ya mradi wa Mkongo zitatekelezwa; usambazaji wa mitandao ya mkongo katika miji; kuendelea na uunganishaji wa mkongo wa Taifa kwa watumiaji wa mwisho; utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi na umuhimu wa Mkongo wa Taifa; na kuwezesha zoezi la kuhuisha kanuni, taratibu, miongozo, viwango na vigezo ya huduma na vifaa vya TEHAMA. Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambao unatekelezwa kwa awamu tano (5) ambapo awamu ya I na II zikiwa na jumla ya kilomita 7,560 zimekamilika na zinatumika; ufungaji wa mitambo ya IP/MPLS kwa ajili ya upanuzi wa mkongo katika mikoa 24 ya Tanzania umekamilika; tathmini ya athari za kimazingira imefanyika; usambazaji wa mitandao umekamilika na inatumika katika miji ya Dar es salaam (Kilomita 300), Mwanza (Kilomita 36), Arusha (Kilomita 58), Tanga (kilomita 43.28), Moshi (kilomita 35.08), Mbeya (kilomita 6.9),

Shinyanga (kilomita 2.3), Musoma (kilomita 2.1) na Biharamulo (kilomita 0.2), Morogoro (kilomita 18) na Dodoma ( Kilomita 42); juhudi za utafutaji wa fedha wa kazi hii unaendelea. Awamu ya V ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa utahusisha ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha watumiaji wa mwisho "Last Mile Broadband Connectivity"; utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Mkongo umefanyika nchi nzima kwa kupitia radio, TV, warsha, makongamano n.k; na muongozo wa utumiaji wa huduma na vifaa vya TEHAMA umeandaliwa.

## G. Nishati

### (a) Miradi ya Uzalishaji Umeme

(i) **Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi I (MW 185):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuandaa eneo la ujenzi wa mitambo ikiwa ni pamoja na kujenga msingi katika eneo litakapowekwa mitambo hiyo; kusanifu ujenzi wa mitambo; na kusimika mitambo. Hatua iliyofikiwa ni kusafishwa kwa eneo la kujenga mitambo ya kufua umeme; kukamilishwa kwa matengenezo ya mitambo ya gesi (Gas Turbines) katika kampuni ya GE nchini Marekani; kukamilishwa kwa malipo kwa kampuni za GE (100%) na Citec ya Norway (90%); na kusafishwa kwa eneo la kujenga mitambo ya kufua umeme.

(ii) **Mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II (MW 240):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ununuzi wa vifaa na mitambo ya kuzalisha umeme na kufunga mitambo. Gharama zote za mradi zimekamilika ambapo hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu na misingi kwa ajili ya kusimika mitambo sita (6); kukamilika kwa ujenzi wa ofisi ya TANESCO na mkandarasi wa mradi Kampuni ya Sumitomo Mitsui Corporation na TOSHIBA; kuendelea na utengenezaji wa mitambo nchini Japan, Korea Kusini na Singapore; kuwasili kwa transfoma nne (4) kati ya nane (8) na mitambo mitatu (3) kati ya sita (6) kuwasili nchini; na kazi ya kufunga mitambo imeanza Aprili 2017.

(iii) **Uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe Kiwira (MW 200) – Mbeya:** katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kufanya uthamini kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaolazimika kupisha eneo la mradi; kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina; na kuanza utekelezaji wa mradi. Hatua iliyofikiwa ni kuanza kwa majadiliano baina ya Tanzania na Serikali ya Urusi ambayo imeonesha nia ya kufadhili utekelezaji wa mradi.

(iv) **Kufua umeme kwa kutumia maji (MW 80) – Rusumo**: Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi mbapo Tanzania itapata MW 26.6. Gharama za ujenzi wa mtambo wa kufua umeme ni Dola za Marekani 340 ambapo mchango wa Serikali ya Tanzania ni Dola za Marekani milioni 113 ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuanza ulipaji fidia kwa wananchi wataoisha mradi; kusafisha njia (route clearence) ya usafirishaji wa umeme na eneo la ujenzi wa mitambo ya kufua umeme. Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa wakandarasi wa ujenzi wa kituo cha kufua umeme ambao ni Kampuni za COCO Group Jingal Water (China) na Hydropower Construction Company (Canada), wakandarasi hao watahusika na kazi za "Civil and Hydro – mechanical"; na Kampuni ANDRITZ HYDRO GmbH na ANDRITZ HYDRO Pvt Ltd (Austria) watahusika na kazi za Electro – mechanical. Vile vile, malipo ya awali kwa wakandarasi kiasi cha Dola za Marekani milioni 16.3 yamefanyika na utekelezaji wa mradi unaendelea. Aidha, uzinduzi wa mradi ulifanywa na Mawaziri wa Nishati wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi tarehe 30 Machi, 2017.

(v) **Kufua umeme kwa kutumia maji (MW 45) – Malagalasi:** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuajiri mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuutangaza mradi kwa njia ya ushindani; kufanya usanifu wa mitambo (technical design); kufanya upimaji wa eneo utakapojengwa mtambo na njia ya usafirishaji wa umeme; na kuajiri makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi. Utekelezaji wa mradi huu unasubiri kupatikana kwa fedha

(vi) **Kufua umeme kwa kutumia maji (MW 87) – Kakono**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuajiri mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuutangaza mradi kwa njia ya ushindani; kufanya usanifu wa mitambo (technical design); kuandaa hati za zabuni (tender/ bidding documents); Upembuzi yakinifu (feasibility study) wa eneo utakapojengwa mtambo na njia ya usafirishaji wa umeme; na kuajiri makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi. Hatua iliyofikiwa ni kuwasisha maombi ya mkopo kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika ambao wameonesha nia ya kufadhili mradi huu; mshauri mwelekezi kampuni ya SP STUDIO PIETRANGELA ya Italia amepetikana kwa ajili ya usimamizi wa mradi; na kukamilika kwa taratibu za kubadilisha umiliki wa eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta 1100 kutoka kwa wamiliki wa sasa (NARCO na Kagera Sugar) kwenda TANESCO.

(vii) **Uendelezaji wa Nishati ya Joto Ardhi (Geothermal) – (MW 100) – Mbeya:** Mradi huu unahusu utumiaji wa joto ardhi kwenye mlima wa Volcano wa Ngozi Mkoani Mbeya kwa ajili ya kuzalisha umeme wa MW 100. Mradi

unatekelezwa na Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB/CIF) na Kamisheni ya Afrika. Hatua iliyofikiwa kamilika kwa utafiti wa kina (Detail surface study) wa uendelezaji wa joto ardhi katika maeneo ya Ziwa Ngozi (Mbeya). Utafiti huo umeweza kuainisha sehemu tatu (3) za kuchoronga visima vya majaribio.

**(b) Miradi ya Usambazaji Umeme**

(i) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo kV 220 Makambako – Songea (km 250):** Lengo la mradi ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme ikujumuisha njia za usamabazaji za umeme wenye msongo wa kV 33 na 0.4; na kuendelea na ujenzi wa njia kubwa ya kusafirisha umeme. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa km 365 kati ya km 580 za msongo katika maeneo ya mkoa wa Ruvuma sawa na asilimia 62.9; kwa upande wa Makambako hadi Njombe km 118 kati ya km 393 zimekamilika sawa na asilimi 30; na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Songea kV 33/11 umefikia asilimia 52.

(ii) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 *North West Grid* (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi km 1,148):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha upembuzi yakinifu na usanifu wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 ili kuwiana na mahitaji ya sasa ya kujenga njia hiyo kwa kiwango cha kV 400; na kupima mkuza wa njia ya umeme kutoka Mbeya hadi Sumbawanga (km 340) na kulipa fidia ya mali zitakazoathiriwa na mradi kwenye njia ya Mbeya - Sumbawanga. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kukamilisha upembuzi yakinifu kutoka kV 220 kwenda kV 400; na kusainiwa kwa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na EDCF ya Korea kwa ajili ya kutekeleza mradi

(iii) **Mradi wa Msongo wa kV 400 *North - East Grid* (Dar – Tanga – Arusha km 682):** katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kulipa fidia kwa ajili ya wananchi wataopisha mradi; kupata mshauri mwekezi kwa jili ya kusimamia ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa tathmini ya fidia kwa wananchi watakapoisha mradi na kuendelea na mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi.

(iv) **Kusambaza umeme Vijijini na Makao Mkuu ya Wilaya (REA Turnkey Phase III)**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kuandaa mahitaji na usanifu wa mradi; kutafuta makandarasi watakaotekeleza mradi; kukamilisha maandalizi ya awamu ya III ya programu

ya REA (REA Turnkey Phase III); kuanza utekelezaji wa mradi; kukamilisha miradi inayotekelezwa chini ya REA II; na kufanya tathmini ya utekelezaji wa REA I na II. Hatua iliyofikiwa ni: ujenzi wa vitu sita (6) ya kuongeza nguvu ya umeme kutoka msongo wa kV 11 hadi 33 katika miji ya Kasulu, Kibondo, Kigoma, Mbinga, Ngara na Tunduru; ujenzi wa njia ya ksambaza umeme wa msongo wa kV 33 wenye urefu wa km 17,740; ujenzi wa vituo vidogo vya kupoza na kusambaza umeme 4,100; ujenzi wa njia ndogo za kusambaza umeme zenye urefu wa km 10,970; kuunganishwa kwa wateja 153,821 sawa na asilimia 62 ya lengo la awali la kuunganisha wateja 250,000 waliokusudiwa kwa mradi wa REA II; na kukamilika kwa kazi za kuunganisha umeme kwenye makao makuu ya wilaya 13 za Busega, Buhigwe, Chemba, Itilima, Kakonko, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele, Momba, Nanyumbu, Nyasa na Uvinza. Kwa REA III kazi zilizofanyika ni: uandaaji wa orodha ya vijiji ambavyo havijapatiwa umeme; kusainiwa kwa mikataba na kuanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa *Densification* unaohusisha mikoa ya Arusha, Iringa, Mara, Mbeya, Pwani na Tanga; kukamilika kwa taratibu za kupata wakandarasi wa kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyoko kwenye mkuza wa njia ya kusafirisha umeme wa *Backbone Transmission Investment Project* kutka Iringa hadi Shinyanga; na kukamilika kwa uchambuzi wa maombi 300 ya kusambaza umeme wa nishati jadididfu kwa vijiji vilivyo nje ya Gridi ya Taifa.

(v) **Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa - Shinyanga (km 670):** Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha kazi za ujenzi wa mradi ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupozea umeme (kV 400/220). Mradi huu umekamilika.

(vi) **Msongo wa kV 400 wa Somangafungu – Kinyerezi:** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka eneo la Somanga Fungu (Lindi) hadi Kinyerezi (Dar es Salaam) na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme eneo la Somanga Fungu. Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha ulipaji fidia kwa wananchi wataoathirika na mradi; kuajiri Mtaalamu Mshauri wa kutayarisha usanifu wa kiufundi (detailed design); na kuajiri Msimamizi wa mradi. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni: kusainiwa kwa mkataba baina ya TANESCO na Mtaalam Mshauri kampuni ya Byucksan Power Ltd ya Korea Kusini ili kudurusu upembuzi yakinifu na kusimamia ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme; na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi ambapo waathirika 2,305 kati ya 3,901 sawa na asilimia 59.1 wamelipwa.

(vii) **Msongo wa kV 220 wa *North - West* kutoka Geita – Nyakanazi**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kupata mkandarasi; na kuanza ujenzi wa mradi. Utekelezaji wa mradi huu unasubiri kupatikana kwa fedha. Kazi zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na: upimaji wa njia kuu ya usafirishaji umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; tathmni ya athari ya kijamii na mazingira; na usanifu wa mradi.

(viii) **Msongo wa kV 220 Bulyanhulu – Geita**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 Bulyanhulu – Geita. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa uchambuzi wa zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi na kufanyika kwa tathmini ya mali za wananachi watakaopisha mradi.

(ix) **Kujenga Miundombinu ya Usambazaji Gesi Asilia (CNG & Piped Natural Gas Distribution Networks) katika Mikoa ya Lindi na Mtwara**: Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: kukamilisha upembuzi yakinifu wa tathmini ya athari za kijamii na kimazingira (esia); kukamilisha usanifu wa kina wa kihandisi; na kuandaa zabuni ya kumpata mwekezaji. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ukamilishaji wa Mpango Kabambe.

**(c) Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) – Tanga (Tanzania):** Katika mwaka 2016/17 mradi ulilenga kufanya maandalizi ya Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya awali (MoU); kutolewa kwa vivutio vya kodi; kufanyika kwa majadiliano ya *Inter-Govermental Agreement* (IGA); kufanyika kwa tathmini ya njia ya bomba (Survey); kufanyika kwa tathmini ya mahitaji ya njia ya bomba (infrastructure requirements); kufanyika tathmini ya masuala ya kijamii na mazingira (environmental and societal survey); kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa gati ya kupokelea mafuta – Chongoleani, Tanga; na kutangazwa kwa zabuni za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya uchunguzi wa udongo (Geophysical and Geotechnical survey). Gharama za mradi ni Dola za Marekani bilioni 3.5. Wadau wakuu katika Mradi huu ni Kampuni ya CNOOC (China), TOTAL (Ufaransa), TULLOW (Uingereza) na Serikali za Tanzania na Uganda. Kazi za *Geophysical and Geotechnical survey* zinaendelea kutekelezwa.

#### 3.2.2.4.2 Mradi wa Kuwezesha Kumilikisha Ardhi

Mradi unalenga kupima ardhi na kutoa hatimiliki katika ngazi ya vijiji, miji na majiji.

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kutoa hati ya hakimiliki za kimila 100,000 katika wilaya tatu (3) za mfano za Kilombero, Ulanga na Malinyi; kubaini mipaka ya vijiji na kutatua migogoro katika vijiji 75; kuandaa na kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji katika vijiji 75; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 100; kuandaa Mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji 100; kupima vipande 150,000 vya ardhi; kuboresha masijala za ardhi katika wilaya 3 za mfano; kukarabati masijala za ardhi za vijiji 75; na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa maandalizi ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi; kusimikwa kwa alama za msingi 54 za upimaji katika wilaya za Ulanga (16), Kilombero (26), Malinyi (10) na Mufindi (2); kupimwa kwa mipaka ya vijiji 52 katika Wilaya za Kilombero (30), Ulanga (19) na Malinyi (16); kuandaliwa kwa Mipango ya Matumizi ya ardhi kwa vijiji 8 kati ya vijiji 18 katika Wilaya za Kilombero (4) na Ulanga (4); na kukusanywa kwa taarifa za awali (baseline data) za vijiji 37 juu ya umiliki wa ardhi, matumizi ya ardhi, migogoro ya ardhi, ufahamu ya sheria ya ardhi kwa ajili ya maandalizi ya Mipango Kabambe ya Miji ya Ifakara, Malinyi na Mahenge.

#### 3.2.2.4.3 Huduma za Fedha, Utalii, Biashara na Masoko

Upatikanaji wa huduma za fedha, biashara na masoko ni nyenzo muhimu kuhakikisha kazi ya uwekezaji na ukuaji wa shughuli za viwanda, kwa mantiki hii hatua zifuatazo zimepewa msukumo wa pekee katika mpango wa 2016/17:

**(a) Ukuzaji wa Mtaji wa Benki ya Wanawake Tanzania**

Benki inatoa huduma za fedha katika Mikoa nane ambayo ni Mwanza, Dodoma, Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Dar es Salaam na Pwani. Hadi sasa, benki imetoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi 9,323,240,000.00 zilizotolewa kwa wajasiriamali 6,267 na kufanya wajasiriamali waliopata mikopo kuongezeka kutoka wajasiriamali 79,983 Desemba, 2015 hadi kufikia wajasiriamali 86,250 Desemba, 2016 ambapo wanawake ni asilimia 73. Idadi ya akaunti imeongezeka kutoka akaunti 27,253 Septemba 2016 hadi kufika akaunti 27,376. Aidha, benki imeanzisha huduma ya kuwawezesha wateja kumiliki ardhi ambapo jumla ya viwanja 47 vimetolewa. Benki imefungua vituo 14 vya kutolea mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali wanawake katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya na Dar es Salaam, idadi ya vituo hivi imeongezeka kutoka vituo 238 Juni 2016 hadi kufikia vituo 252.

**(b) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake**

Serikali imeendelea kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu. Mafanikio ni pamoja na: Serikali kutoa shilingi milioni 156 ambazo ni fedha za mzunguko kwa vikundi 61 vya wanawake wajasiriamali katika Halmashauri sita (6) za Kisarawe, Gairo, Masasi, Busokelo, Mtwara Vijijini na Manispaa ya Iringa; kutolewa kwa mafunzo kuhusu faida za

kujiunga katika vikundi yaliyotolewa kwa wanufaika wapatao 450 katika Halmashauri za wilaya ya Njombe na Ludewa; kuendelea kwa Halmashauri kuchangia asilimia 5 ya mapato yao ya ndani ambapo Halmashauri 128 sawa na asilimia 70.3 ya Halmashauri zote nchini, zimechangia kiasi cha shilingi 6,222,164,982.00 kufikia Septemba, 2016 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 2.7 ya mapato ya Halmashauri ya ndani.

**(c) Benki ya Rasilimali Tanzania**

Benki ya Rasilimali Tanzania inalenga kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wawekezaji katika sekta ya kilimo, viwanda, biashara, usafiri, utalii na uchimbaji madini. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na utoaji wa mikopo wa jumla ya Shilingi bilioni 5.056 katika sekta za Kilimo – usindikaji wa mazao (bilioni 1.625); ujenzi (bilioni 0.957); Elimu (milioni 52.34); Uvuvi (milioni 12.132); Utalii – hoteli na migahawa (milioni 885.025); sekta ya uzalishaji (milioni 495.062); na uchimbaji wa madini (milioni 36.127). Pia benki imetoa mikopo kwa watu binafsi yenye thamani ya Shilingi milioni 139.538; real estates Shilingi milioni 850.732; na sekta nyingine zilipatiwa mkopo wa Shilingi milioni 3.289.

**(d) Benki ya Maendeleo ya Kilimo**

Serikali imekwishatoa zaidi ya shilingi bilioni 60 kwa benki hii ikiwa ni sehemu ya mchango wa Serikali katika kukuza mtaji ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2016/17 shughuli zilizofanyika ni pamoja na benki kuongezewa ujuzi na Tanzania Merchantile Exchange – TMX katika kuandaa mipango ya kuwawezesha wakulima kuunganishwa na masoko ya uhakika; kupata jengo la kufungua ofisi mkoani Dodoma; kufikia makubaliano na MIVARF na IFAD ya kuiwezesha TADB Kusimamia fedha za dhamana kwa mabenki kutoa mikopo (MIVARF – Dola za Kimarekani milioni 20 na mfuko wa Fedha za Ubunifu Vijijini – Rural Innovation Fund zinazotolewa na IFAD) ambapo MIVARF tayari imetoa jumla ya Shilingi milioni 578.3 kwa ajili ya gharama za usimamizi. Pia, benki imejenga uwezo kwa vikundi 336 vya wakulima wadogo vyenye jumla ya wanachama 44,400 katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga. Vikundi 19 kati ya hivyo vimefanikiwa kutimiza masharti na maandalizi ya msingi ya kuweza kukopa. Vikundi vilivyobaki vinaendelea kupatiwa mafunzo ili viweze kufikia hali ya kuweza kukopesheka.

**(e) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara**

Mradi unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ambapo shughuli zilizofanyika ni pamoja na Serikali kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa AGOA ambao utaisaidia Tanzania kufaidika zaidi na fursa zilizopo kwenye AGOA na soko la Marekani kwa ujumla. Mkakati huu umejikita katika sekta nne za kipaumbele ambazo usindikaji wa bidhaa za kilimo, ngozi na bidhaa zake, nguo na mavazi na bidhaa za kazi za mikono; kukamilika kwa Mpango Kazi wa utekelezaji wa

makubaliano ya FOCAC VI ambao unajumuisha miradi ya viwanda, nishati, miundombinu, fedha, kilimo, elimu na TEHAMA; Uanzishwaji wa kamati ya kitaifa ya Uwezeshaji biashara; usajili wa kampuni na majina ya biashara kwa njia ya mtandao ikiwa ni pamoja na kuwezesha malipo kufanyika kwa njia ya mtandao. Mafanikio katika maboresho ya mazingira ya uwekezaji na biashara ni: kupunguza kwa kiasi kikubwa muda wa kusajili makampuni na majina ya biashara ndani ya masaa 1-2 na hivyo kupunguza gharama kwa wateja; kuanzishwa kwa utaratibu wa ukaguzi wa bidhaa chini ya mfumo wa Pre-shipment Verification of Conformity to Standards Programme (PVoC) kupitia mawakala wake waliopo Japan (3), Dubai (1) na Uingereza (1) kwa lengo la kuepuka uingizaji wa bidhaa hafifu.

Aidha, Serikali kupitia Mamlaka za Uwekezaji zillingia makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji na mauzo ya bidhaa katika masoko ya China na Morocco; kupitia kongamano la biashara na mkutano wa pamoja kati ya Tanzania na Rwanda ilikubaliwa kuondolewa kwa vikwazo vya kibiashara visivyokuwa vya kiushuru (NTBs) ambapo Rwanda iliridhia kuondoa vikwazo hivyo kwenye mchele kutoka Tanzania, pia kupitia majadiliano mbalimbali jumla ya NTBs 8 ziliondolewa; Serikali inaendelea kufanya mapitio ya ushuru wa pamoja wa Jumuiya ya Afrika Masharika (EAC Common External Tarrif), mkakati wa viwanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na mpango kazi wa utekelezaji wa mkakati huo.

**(f) Uendelezaji wa Shughuli za Masoko**

Mradi wa ujenzi soko la kimataifa la Makambako ulijumuisha kulipa fidia kwa wananchi 220 watakaondoka katika eneo la mradi. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kufanyika kwa tathmini; kukamilika kwa mfumo maalum wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko kwa haraka na kwa wakati; na kuwezesha wajasiriamali 28 kutoka mikoa ya Mbeya, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, na Zanzibar kushiriki katika kuonesha bidhaa zao katika maonyesho ya nanenane.

**(g) Utalii**

Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii, kupanua wigo wa vivutio vipya vya utalii na kuimarisha huduma ya usafiri wa anga. Vile vile, Serikali inafanya juhudi kubwa za kudhibiti ujangili na biashara haramu ya wanyamapori. Kutokana na jitihada hizi za Serikali, idadi ya watalii iliongezeka kutoka 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,284,279 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 12 na kuliingizia Taifa Dola za Marekani bilioni 2.

### 3.2.2.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango

Changamoto ya utekelezaji duni wa mipango na miradi imeanishwa na kujaribu kupatiwa ufumbuzi, hususan, kuhusiana na maeneo yafuatayo:-

#### 3.2.2.5.1 Utawala Bora, Utoaji Haki na Huduma za Kisheria

**(a) Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: usajili na utambuzi wa watu ambapo wananchi 388,990 walisajiliwa na kuchukuliwa alama za kibailojia; kutengenezwa kwa vitambulisho 72,925 na kugawiwa kwa wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani pamoja na Zanzibar; kuongezwa kwa vitendea kazi katika ofisi za wilaya zote za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na Wilaya ya Arusha mjini; na kusajili na kuwatambua watu 8,559,671 ambapo 8,551,259 ni raia wa Tanzania ikijumuisha mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar na 8,412 ni wageni wakaazi.

**(b) Mfuko wa Mahakama**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa Mahakama Kuu, kanda za Kigoma na Mara; ukarabati wa majengo ya Makahama Kuu, kanda ya Mbeya; ujenzi wa mahakama za wilaya za Kilindi, Chato, Bariadi, Kasulu, na Kondoa; ujenzi wa mahakama za mwanzo Longido, Terati (Manyara), Machame (Hai), Njombe Mjini, Makongolosi (Chunya), Ulyankulu (Tabora) na Gairo - (Mvomero), Mtowisa (Sumbawanga) na Mangaka (Mtwara). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa ujenzi wa mahakama ya hakimu mkazi na Hakimu wa Wilaya Kibaha.

**(c) Telejustice (E–Justice)**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kukamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi; kuanza utekelezaji awamu ya kwanza ya mradi huo katika mkoa wa Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa maandalizi ya hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi.

**(d) Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni ujenzi wa jengo la ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kukamilika kwa michoro ya jengo.

### 3.2.2.6 Maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa

#### 3.2.2.6.1 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**a) Mradi wa kujenga, kukarabati na kununua majengo kwa ajili ya Balozi za Tanzania**

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kuboresha huduma kwa kujenga, kukarabati na kununua majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi hususani za ofisi, makazi na kitega uchumi. Katika mwaka 2016/17, Shilingi bilioni

8.0 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambalo ni sehemu ya Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Julius Nyerere; kukamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa 9, makazi ya Balozi na mkuu wa utawala ubalozi wa Tanzania Maputo, Msumbiji; kukarabati makazi ya Balozi na watumishi yaliyopo Stockholm, Sweden; kukarabati majengo 2 yanayomilikiwa na Serikali yaliyopo Khartoum, Sudan; na kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Afrika Mashariki na balozi za Tanzania. Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kuendelea na ukarabati wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Maputo; na kuendelea na utaratibu wa kumpata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi na Afisa Ubalozi Stockholm, Sweden.

#### b) Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani

Serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma mipakani kwa kuendelea na mradi wa ujenzi wa vituo vya Tunduma/Nakonde, Kasumulu/Songwe na Mtambaswala. Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa kituo cha Tunduma/Nakonde ni: utiaji wa saini wa Mkataba wa Makubaliano ya Kurahisisha Biashara (Simplified Trade Regime – STR) kati ya Tanzania na Zambia na kuanza ujenzi; na kuanza kwa maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kutenga eneo la ujenzi wa kituo cha Kasumulu/Songwe. Aidha, Tanzania na Malawi zimekubaliana kuanzisha kituo cha pamoja cha mpakani – OSBP na kuingia makubaliano ya kuanzisha mkataba wa mfumo wa kurahisisha biashara (Simplified Trade Regime - STR).

#### 3.2.2.6.2 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (MKURABITA)

Katika mwaka 2016/17, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni: kukamilika kwa mwongozo wa utekelezaji wa Miradi ya Majaribio ya Urasimishaji kwa kutumia dhana ya Mfuko wa Dhamana katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri 2 za Mkoa wa Songwe; kuanzishwa kwa kituo cha urasimishaji (One Stop Formalization Center) katika Mkoa wa Morogoro ili kuwezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi na gharama nafuu; na kukamilika kwa utafiti wa uanzishwaji wa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya kwa mfumo wa dhamana kwa ajili ya kuziwezesha halmashauri kukopa kwa ajili ya urasimishaji.

## 3.3. Ushiriki wa Sekta Binafsi

### 3.3.1. Usaidizi wa Serikali katika Miradi ya Sekta Binafsi

Maendeleo ni jukumu la msingi la Serikali ambapo inaweza kulitekeleza jukumu hili yenyewe moja kwa moja au kwa kutumia wadau wengine, ikiwa ni pamoja na sekta binafsi. Serikali imeendelea kutambua na kuthamini mchango mkubwa wa sekta

binafsi katika utekelezaji wa jukumu lake la maendeleo. Kwa kuzingatia hili na ili kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

(i) Kuweka sera, sheria na taratibu zinazowezesha ushiriki wa sekta binafsi, ama moja kwa moja au kwa ubia na sekta ya umma, hata katika maeneo ambayo hapo awali yalikuwa ni fursa ya sekta ya umma pekee;

(ii) Katika kuipunguzia usumbufu sekta binafsi katika upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji, Serikali, licha ya kupima na kutenga ardhi ya uwekezaji, imetenga maeneo mahsusi ya uwekezaji (EPZ, SEZ na kuanzisha benki ya ardhi chini ya TIC), ambayo husaidia kuweka miundombinu msingi na kuikodisha kwa wawekezaji kwa gharama nafuu;

(iii) Kujenga miundombinu wezeshi mfano barabara, umeme, maji, reli na kuifikisha katika maeneo na shughuli za wawekezaji;

(iv) Kuboresha sera, sheria, na taratibu zilizokuwa ni kikwazo kwa wawekezaji na wafanyabiashara;

(v) Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu na kuhakikisha kuwepo kwa amani na usalama;

(vi) Kuanzisha mifuko maalum ya kuchochea ushiriki wa wawekezaji binafsi mfano SAGCOT *Catalytic Fund* na *PPP Facilitation Fund* na sasa inapendekezwa kuanzishwa mfuko wa maandalizi ya miradi;

(vii) Kuboresha huduma kwa wawekezaji, ikiwa ni pamoja na kuanzisha "one stop centre" chini ya TIC, bandari ya Dar es Salaam na vituo vya utoaji huduma ya pamoja mipakani (one stop border post); na

(viii) Kwa maksudi ya kuboresha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu na ya muda mrefu, Serikali imeaanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na kuendelea kuimarisha mtaji Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB).

### 3.3.2. Miradi Inayotekelezwa na Sekta Binafsi

Sekta binafsi imeendelea kufanya uwekezaji katika sekta za kilimo, mawasiliano, ujenzi wa majengo, miundombinu, nishati, huduma za fedha, uzalishaji bidhaa, maliasili, utalii, uchukuzi, matangazo, kompyuta, na huduma. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kusajiliwa kwa miradi 345 na Kituo cha Uwekezaji Tanzania yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 5,919.44 inayotarajiwa kutoa jumla ya ajira 49,711 ambapo miradi 103 ni ya ndani, 137 ni miradi ya nje na miradi 105 ni ya ubia. Sekta ya uzalishaji bidhaa iliongoza kwa kuwa na miradi mingi ambapo jumla ya miradi 178 ilisajiliwa na kutoa jumla ya ajira 12,455. Baadhi ya miradi mikubwa imeanza kutekelezwa ambayo ni pamoja na ujenzi wa kijiji cha viwanda (industrial parks) unaofadhiliwa na Kampuni ya *Star City* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Watanzania na Wasingapore imeendeleza eneo la Hekta 4,000 kwa kuanza kuweka miundombinu kwa ajili ya viwanda katika eneo la Kingolwira, mkoa wa Morogoro. Mradi huu unaonesha ni jinsi gani sekta binafsi

inavyowekeza katika ujenzi wa viwanda; ujenzi wa kiwanda cha vigae *Tywford Tiles* ambacho kinauwezo wa kuajiri wafanyakazi 2,000; ujenzi wa kiwanda cha *Goodwill Ceramic* chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 1,000; na kuanza kwa uzalishaji katika kiwanda cha *Steel Industries Ltd* kilichopo Mlandizi, Pwani chenye uwezo wa kuajiri wafanyakazi 500.

#### 3.3.3. Miradi ya Ubia na Serikali

Katika mwaka 2016/17, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 5 kwa ajili ya Mfuko wa fedha wa miradi ya ubia (PPP Facilitation Fund) kuratibu uandaaji wa taarifa za upembuzi yakinifu na kujenga uwezo kwa wadau wanaohusika na uibuaji wa miradi. Hii inahusisha miradi ya Dar – Chalinze Expressway, Kiwanda cha Kutengeneza Madawa Muhimu na Vifaa Tiba, Mradi wa Mwendokasi – DART Phase I na Mradi wa Kufua Umeme Kinyerezi III. Hatua iliyofikiwa ni: kupatikana kwa Mtaalam Mwelekezi (Transaction Advisor) na kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa miradi ya Dar – Chalinze Expressway; kuendelea na taratibu za kumpata Mtaalam Mwelekezi (Transaction Advisor) atayefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa mradi wa kiwanda cha kutengeneza madawa muhimu na vifaa tiba; kupatikana kwa mkandarasi wa muda wa kuendesha huduma ya usafiri wa mradi wa mwendokasi – DART Phase I; kuendelea na majadiliano ya umiliki kati ya Serikali na wabia wengine watakaoshiriki katika uwekezaji wa mradi wa kufua umeme Kinyerezi III; na kutoa elimu ya PPP kwa wadau.

### 3.4. Miradi Iliyofuatiliwa na Changamoto za Utekelezaji na Kinga

#### 3.4.1 Miradi Iliyofuatiliwa

Katika mwaka 2016/17 Tume ya Mipango kwa kushirikiana na sekta ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 42 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Tabora, Mwanza, Pwani, Lindi na Mtwara. Miradi ya viwanda iliyofuatiliwa ilijumuisha ifuatayo:

#### (a) Kiwanda cha Nyama – Chobo Investment Limited

Kiwanda hiki kilianzishwa mwaka 2008 na kupata usajili rasmi mwaka 2011 na kipo mkoa wa Mwanza katika Wilaya ya Misungwi. Kiwanda kinajihusisha na uchakataji wa bidhaa mbalimbali za nyama na samaki.



*Mashine ya kisasa ya kuchinja ng'ombe katika kiwanda cha nyama cha Chobo – Misungwi Mwanza.*

Kiwanda kimeajiri wafanyakazi zaidi ya 90 na kinachinja ng'ombe 70 hadi 100 kwa wiki ikilinganishwa na uwezo halisi wa kuajiri wafanyakazi 150 na kuchinja zaidi ya ng'ombe 500 kwa siku. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: kutopatikana kwa mifugo inayokidhi viwango hususan uzito unaohitajika; Kutokuwa na maeneo ya kunenepeshea na kulishia mifugo; kuwa na mtaji kazi (working capital) mdogo wa kukidhi uendeshaji wa kiwanda; kukosa mtaji wa kukamilisha kiwanda hususan ujenzi wa maabara, jengo la utawala, kununua magari na kuanzisha kituo cha kunenepesha mifugo; kutokuwa na miundominu ya maji hivyo kukosa maji ya uhakika na kuongeza gharama za uzalishaji; na mwingiliano na mgongano wa kimamlaka na utendaji kwa taasisi nyingi za Serikali zinazoshabihiana mfano TBS, TFDA, Idara ya Afya, OSHA, FIRE na NEMC zinasababisha urasimu katika kupata vibali na ufuatiliaji.

### (b) Kiwanda cha S & Y

Kiwanda hiki kilianzishwa mwaka 2014 na kuanza uzalishaji mwaka 2015, kipo mkoa wa Dodoma na kinashughulika na uchakataji wa mazao ya nyama ya ng'ombe. Kiwanda kinamilikiwa na raia wa kigeni na kimeajiri wafanyakazi 70, na kinazalisha mazao ya nyama ya ng'ombe na kufungwa kwa ajili ya soko la nje pekee; na kinauwezo wa kuchinja na kuchakata ng'ombe 20 kwa siku. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: Kutopatikana kwa ng'ombe wa kutosha na wanaokidhi vigezo; Ukosefu wa miundombinu na huduma wezeshi; Uwepo wa tozo nyingi na vibali vingi katika biashara ya nyama; na Tatizo la wafanyakazi kuacha kazi baada ya muda mfupi (labour turnover).

### (c) Kiwanda cha Tanzania Meat Company (TMC)

Kiwanda kipo mkoa wa Dodoma na kilianzishwa na Serikali mwaka 2004 na mwaka 2008 Serikali iliuza sehemu ya umiliki wake kwa sekta binafsi (kampuni ya NICOL)

kwa asilimia 51. Kiwanda kina malengo ya kuvutia wawekezaji kuwekeza katika ujenzi wa maeneo ya kupozea nyama (*Cold rooms*) na kuwezesha kuchinja ngómbe zaidi ya 200 na mbuzi zaidi ya 1,500 kwa siku; kuuza kwenye soko la nchi za Falme za Kiarabu (UAE); na kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa kwa wananchi.



*Sehemu ya Kuhifadhia nyama Tanzania Meat Company (TMC)*

Kiwanda kimepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kukuza masoko ya wawekezaji wadogo wanaojihusisha na biashara ya nyama; kutangaza biashara ya nyama katika masoko ya Kimataifa; na kutoa ajira za moja kwa moja kwa watu 160 na zaidi ya 100 kwa wawekezaji wa makampuni ya kusafirisha nyama. Pamoja na mafanikio hayo, kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: upatikanaji wa maligafi (ng'ombe na mbuzi); uwepo wa kodi nyingi ambazo zimekuwa zikiongezeka mara kwa mara; na kusitishwa kwa uwekezaji toka China ambao ulihitaji kupata bidhaa za nyama na ngozi kwa wakati mmoja.

**(d) Kiwanda cha Nyama – Alpha Choice**

Kiwanda kipo katika Wilaya ya Magu mkoani Mwanza na kina uwezo wa kuchinja na kuchakata nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo kiasi cha tani 20 kwa siku kwa ajili ya soko la ndani. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 65. Kiwanda kina lengo la kuongeza maeneo ya kufugia na kunenepeshea mifugo ambapo tayari ekari 250 zimepatikana katika Wilaya ya Chato na kuongeza uzalishaji na kuuza bidhaa za nyama katika masoko ya nje. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: upatikanaji wa mifugo yenye ubora; na kuwepo kwa utitiri wa kodi na tozo ambazo zinaongeza gharama za uendeshaji;

## (e) Kiwanda cha Arusha Meat Company

Kiwanda hiki kinamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha kupitia Kampuni ya Maendeleo ya Jiji (CDC). Kampuni hii inajihusisha na uchinjaji wa wanyama pamoja na uendeshaji wa machinjio. Machinjio huchinja kwa wastani ng'ombe 120 na mbuzi 120 kwa siku za kawaida na ng'ombe 300 na mbuzi 500 wakati wa siku za sikukuu. Vile vile, Kampuni hii imekuwa ikitoa mafunzo ya uchinjaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za nyama ambapo mpaka sasa jumla ya vijana 120 wamepatiwa mafunzo na kuhitimu. Changamoto zinazoikabili kampuni hii ni: uwezo mdogo wa kuzalisha na kusindika nyama kibiashara; ukosefu wa mashine kama vile ya kutenganisha nyama na mifupa (deboning), kuzalisha vifungo, gundi pamoja na chakula cha mifugo kwa kutumia kwato na pembe; uduni wa miundombinu na mashine zilizopo kutokidhi haja; uwepo wa machinjio ndogo ndogo ndani ya Halmashauri za Jiji la Arusha ambazo zinasababisha wafanyabiashara wengine kutumia machinjio hizo; kiwanda kutokuwa na mitambo ya kuzalisha biogas; na kukosekana kwa mitambo ya kukausha damu.

## (f) Kiwanda cha Maziwa cha Tanga Fresh

Kiwanda kinamilikiwa na kampuni ya Kiholanzi na kina uwezo wa kuzalisha lita 50,000 za maziwa kwa siku. Kiwanda kinategemea malighafi kutoka kwa wakulima wadogo na wa kati katika Mkoa wa Tanga. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazao: uhakika wa upatikanaji wa maziwa kutoka kwa wakulima hususan kipindi cha kiangazi; uwepo wa kampuni ndogo ndogo zinazozalisha bidhaa za maziwa hivyo kupelekea ushindani wa bei ya maziwa kutoka kwa wakulima; kiwango cha chini cha ubora wa maziwa kutoka kwa wakulima; na ukosefu wa mtaji.




*Ujenzi wa jengo jipya wa Kiwanda cha Tanga Fresh ukiendelea, Januari 2017*

**(g) Kiwanda cha Kuchakata Ngozi cha *SAK International***

Kiwanda kipo katika Hamashauri ya Jiji la Arusha na kinamilikiwa na kampuni ya *SAK International.* Kiwanda kinachakata ngozi kwa ajili ya soko la ndani na kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi na kimeajiri wafanyakazi 30. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: upatikanaji ngozi bora unaosababishwa na upigaji chapa wanyama na uchunaji mbovu; na kushuka kwa soko la ngozi.

**(h) Kiwanda cha Kuchakata Ngozi cha Salex**

Kiwanda kipo katika Jiji la Arusha na kinamilikiwa na *Salex Company Limited*. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata ngozi za ng'ombe 400, mbuzi 6,000 na kondoo 3,000 kwa siku na kimeajiri wafanyakazi 38. Kiwanda hiki kwa kiasi kikubwa kinazalisha bidhaa kwa ajili ya soko la nje. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto za: upatikanaji ngozi bora unaosababishwa na upigaji chapa wanyama na uchunaji mbovu; na usafirishaji haramu wa ngozi ghafi nje ya nchi.

**(i) Eneo la Viwanda Vidogo – SIDO, Mwanza**

SIDO Mkoa wa Mwanza imejikita katika kutekeleza jukumu la kulea na kuendeleza viwanda vidogo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya viwanda vidogo na vya kati kutoka 750 mwaka 2012 hadi kufikia viwanda 1,500 mwaka 2016; ujenzi wa majengo 10 katika eneo la SIDO Nyakato *Industrial Estate* lenye viwanda vidogo 17 ambavyo vinafanya kazi na vimeajiri watu 200; kuvipa mikopo vikundi vya wajasiriamali kupitia *National Entrepreneurship Development Fund* (NEDF) na *Regional Revolving Fund* (RRF); na kusaidia usajili wa Jumuiya ya Mafundi kwa Kanda ya Ziwa (Lake Zone Artisants Association – LAZOA) ambayo inajumuisha vikundi 80 kutoka Mwanza, Mara, Shinyanga na Kagera. Changamoto zilizopo ni: kukosekana kwa *Foundry*; upatikanaji wa rasilimali fedha na maeneo ya kutosha ya kuendeleza viwanda; na tozo nyingi kwa wafanyabiashara wadogo.

**(j) SIDO Mkoa wa Arusha**

SIDO Mkoa wa Arusha imejikita katika kutekeleza jukumu la kulea na kuendeleza viwanda vidogo ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiriamali, masoko na fedha, kuongeza tija katika uzalishaji – Kaizen na teknolojia mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo; kutekeleza programu ya kuwaendeleza wabunifu wadogo (incubation program) na kuwawezesha wajasiriamali wadogo kushiriki katika maonesho mbalimbali ya viwanda, biashara na bidhaa. Mafanikio ya SIDO Arusha ni kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kwa lengo la kuimarisha viwanda vidogo pamoja na kuongeza tija viwandani kupitia mafunzo ya Kaizen; kutoa mafunzo ya kusindika ngozi kwa kushirikiana na *World Vision*; kutekeleza mradi wa utengenezaji wa mizinga ya nyuki ya kisasa kwa ushirikiano wa *World Vision*; na kuandika maandiko mbalimbali ya biashara (Business Plan) kwa ajili ya kuuza kwa wahisani. Kupitia jitihada hizo Umoja wa Ulaya umeridhia kufadhili mradi wa ujenzi wa kituo cha

kuchakata ngozi – Oldonyosambu. SIDO Arusha inakabiliwa na changamoto: uchakavu wa miundombinu na mashine; ukosefu wa rasilimali fedha na upungufu wa rasilimali watu; uvamizi wa eneo la shirika; tozo na kodi; na ukosefu wa mitaji kwa wahitimu wa mafunzo.

**(k) Eneo la Viwanda Kisarawe (Kisarawe Industrial Park)**

Mradi una eneo lenye ukubwa wa ekari 3,000 kwa ajili ya viwanda na makazi na lipo karibu na njia ya Reli ya Kati (m 50) na TAZARA (km 3). Mafanikio kadhaa yamepatikana ikiwemo kupimwa kwa jumla ya viwanja 291; na kuanzishwa kwa tovuti maalum kwa ajili ya kulitangaza eneo la Viwanda la Kisarawe. Mradi unakabiliwa na changamoto zifuatazo: miundombinu hafifu ya maji, gesi asilia, umeme, barabara na reli; upatikanaji hafifu wa rasilimali fedha kutoka Serikalini kwa ajili kuendeleza eneo; na mpango wa matumizi ya ardhi na mpango kabambe wa kisarawe uliopitwa na wakati.

**(l) Kiwanda cha Saruji Tanga**

Kiwanda kinazalisha saruji na malighafi ya kuzalisha saruji (clinker) ambapo kwa mwaka 2016 kiwanda kilizalisha saruji tani 80,000 na malighafi ya saruji (clinker) tani 40,000. Kiwanda kimekamilisha ujenzi wa tanuru (Kiln) la pili; kumiliki kikamilifu kampuni ya usambazaji wa saruji katika Afrika Mashariki; kuwekeza katika mashirika ya jamii; na kuimarika kwa ubora wa bidhaa za kiwanda. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika; maandalizi ya makaa ya mawe kwa ajili ya kuzalisha nishati; na ukosefu wa reli na barabara za uhakika katika eneo la kiwanda.

**(m) *Lake Tannery Trading Company***

Kiwanda kinajihusisha na usindikaji wa ngozi kwa kiwango cha *wet blue leather na finished leather*. Kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 40 na kina uwezo wa kusindika vipande vya ngozi ya ng’ombe 400 na mbuzi 2,500 sawa na futi za mraba 30,000 kwa siku. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto za zifuatazo: upatikanaji wa ngozi bora; ukosefu wa maji ya kutosha; kodi na ushuru mkubwa; ukosefu wa nguvu kazi yenye ujuzi wa kutosha katika sekta ya ngozi; na gharama kubwa ya madawa na kemikali mbalimbali za ngozi.

**(n) Kiwanda cha kuchakata Juisi cha Mwandege**

Kiwanda kipo Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani na kinasindika matunda (embe, machungwa na nanasi) na kutengeneza juisi na soda. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha chupa 24,000 za soda na chupa 28,000 za juisi kwa saa sawa na tani 250 za juisi na soda kwa siku. Kiwanda kinatarajia kujenga mitambo mingine itayoongeza uzalishaji kufikia tani 350 kwa siku ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi hususan nchi za Afrika Mashariki. Kiwanda kina eneo lenye ukubwa wa ekari 62 na

kimeajiri jumla ya wafanyakazi 800 wakiwemo vibarua 300.




*Uzalishaji wa soda na Juisi katika kiwanda cha Azam*

Kiwanda kinakabiliwa na changamoto zifuatazo: ukosefu wa malighafi ikiwemo sukari ya viwandani hapa nchini; uwezo mdogo wa kiwanda kununua matunda yote yanayozalishwa na wakulima; ukosefu wa ardhi ya kutosha kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda; na gharama kubwa za uzalishaji kutokana na kutumia umeme wa jenereta.

### 3.4.2 Changamoto za utekelezaji na Kinga

Changamoto za jumla katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 ni pamoja na:

(i) **Upatikanaji wa fedha za ulipaji fidia kwa maeneo ya uwekezaji**: Baadhi ya miradi ya maendeleo inahitaji ardhi iliyo wazi ili utekelezaji uweze kuanza. Hivyo, fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi zinapochelewa kupatikana kunapelekea utekekelezaji wa miradi kuchelewa kuanza.

(ii) **Uwezo mdogo wa uandaaji wa miradi inayouzika kwenye taasisi za fedha:** Miradi mingi hushindwa kukidhi vigezo vya kukopa mfano kutokuwa na andiko la mradi na taarifa ya upembuzi yakinifu, hivyo Serikali kulazimika kuigharamia kwa mapato yake ya ndani.

(iii) **Ukosefu wa miundombinu wezeshi kama vile nishati, maji na barabara:** Miundombinu katika maeneo ya mradi ni muhimu sana hususan katika kuwezesha usafirishaji wa vifaa vya ujenzi hadi katika eneo la mradi na malighafi za uzalishaji kiwandani. Miradi katika maeneo mengi ndani ya mikoa na Halmashauri huwa vigumu kutekelezwa kutokana na miundombinu duni.

(iv) **Upatikanaji wa malighafi za kutosha na zenye ubora:** Viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika kuzalisha bidhaa nyingine za viwandani ni

muhimu katika kuchochea uwekezaji hususan katika viwanda. Kukosekana kwa viwanda vya aina hiyo kumekuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(v) **Ukosefu wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji:** Upatikanaji wa mitaji ni muhimu katika kuchochea uwekezaji, ufinyu wa mitaji ya Umma na Sekta binafsi nchini kumekuwa kikwazo cha kuwekeza katika miradi mikubwa yenye matokeo makuwa katika uchumi wa Taifa. Mfano uwekezaji katika miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga imeshindikana kutekelezwa kwa miaka mingi kutokana na ukosefu wa mitaji.

(vi) **Wingi wa kodi na tozo hususan maeneo ya viwanda:** Mazingira ya Uwekezaji yanaweza kuwa kikwazo au kivutio kwa wawekezaji. Wingi wa kodi na tozo mbalimbali nchini katika ngazi za Wizara na Halmashauri zimekuwa kikwazo kwa wawekezaji. Wingi wa kodi na tozo hizo husababisha usumbufu kwa wawekezaji, hivyo kutovutiwa kuwekeza nchini na hatimaye kuwekeza katika nchi nyingine zenye taratibu nzuri za kodi.

(vii) **Matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati**: Baadhi ya mashine na mitambo ya uzalishaji katika viwanda mbalimbali nchini ambavyo vilianzishwa miaka mingi iliyopita bado vinatumia teknoloji iliyopitwa na wakati. Hii inasababisha kushindwa kushindana na viwanda vya nje vinavyozalisha bidhaa zinazofanana kutokana gharama za uzalishaji kuwa juu ikilinganishwa na viwanda vya nje vinavyotumia teknolojia ya kisasa.

(viii) **Wadau muhimu wanaoshughulikia miradi ya maendeleo kufanya kazi *in silos*:** wadau muhimu kufanya kazi kwa pamoja katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni muhimu ili kuharakisha utekelezaji hususan kwa miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja ikijumuisha mihimili yote ya Serikali na sekta binafsi.

Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hizo ikiwemo: kuwianisha mapato na matumizi kwa kuhakikisha kuwa mgawo wa fedha unaendana na upatikanaji wa mapato; kuendelea kupunguza matumizi yasiyo ya lazima; kuelekeza fedha katika miradi ya maendeleo; na kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara nchini ikijumuisha kupambana na rushwa na mianya yote ya ubadhirifu.

# SURA YA NNE

# VIPAUMBELE VYA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18

## 4.1 Utangulizi

Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2017/18 imegawanyika katika maeneo matano yafuatayo: miradi itakayopewa msukumo wa juu ikiwemo ya kielelezo; viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; kufungamanisha maendeleo ya uchumi na rasilimali watu; kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango. Miradi ipo katika maeneo ya kipaumbele yanayoendana na azma ya kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, ya kutumia kimkakati rasilimali za Taifa kujenga uchumi wa viwanda na kuchochea maendeleo ya watu. Hivyo, kwa kiasi kikubwa, miradi iliyobainishwa katika Mpango wa mwaka 2017/18 ni muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya mwaka 2016/17.

## 4.2 Misingi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2017/18

Katika kipindi cha muda wa kati (2017/18 - 2019/20), misingi ya mpango na bajeti ni pamoja na:-

(i) Amani, usalama, utulivu na utangamano wa ndani na nchi jirani vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa;
(ii) Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, mfumuko wa bei, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika;
(iii) Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
(iv) Bei za mafuta katika soko la dunia zitaendelea kuimarika;
(v) Hali ya hewa nchini na katika nchi jirani kuwa nzuri;
(vi) Mahusiano na nchi jirani, kikanda na kimataifa kuendelea kuwa mazuri; na
(vii) Kuwepo kwa sheria na taratibu wezeshi kwa uwekezaji.

## 4.3 Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla

Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2016;
(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja;
(iii) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani (ikijumuisha ya Serikali kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa) kufikia asilimia 16.5 ya Pato la Taifa;
(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18;
(v) Matumizi ya Serikali kufikia asilimia 24.9 ya Pato la Taifa;

(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) ya asilimia 3.8 ya Pato la Taifa;

(vii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(viii) Kuhakikisha utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania.

## 4.4 Miradi ya Kipaumbele

### 4.4.1 Miradi ya Kielelezo

Hii miradi mikakati iliyobainishwa kwa utekelezaji katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21. Miradi hii ni ile iliyobainishwa kwa kuzingatia ukubwa wake na matokeo yake makubwa katika ukuzaji wa uchumi, ubadilishaji wa mfumo wa uchumi, kujenga uwezo endelevu wa ujenzi wa uchumi wa viwanda na kuchochea maendeleo ya watu. Miradi hii inajumuisha ile ya kielelezo.

#### 4.4.1.1 Ujenzi wa Reli ya Kati

Mradi huu utahusisha ujenzi wa Reli ya Kati kutoka Dar – Tabora - Kigoma (km1,251) kwa *Standard Gauge* na matawi yake ya: Tabora – Isaka – Mwanza (km 379); Isaka – Rusumo (km 371); Kaliua – Mpanda - Karema (km 321); Keza – Ruvubu (km 36); na Uvinza – Kalelema kuelekea Musongati (km 203). Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 900 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kuendelea na ujenzi wa reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 205); kukamilisha taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa maeneo ya Morogoro hadi Makutupora (Km 336), Makutupora hadi Tabora (Km 294), Tabora hadi Isaka (Km 133) na Isaka hadi Mwanza (Km 249); kupata eneo la ardhi kati ya Mpiji na Soga (Pwani) lenye ukubwa wa hekta 1,000 kwa ajili ya kuunganishia na kuanzishia treni ndefu; ulipaji wa fidia wa ardhi ekari 500 eneo la Buhongwa (Mwanza) kwa ajili ya kuunganishia na kupokelea treni ndefu (Marshalling yard); kupata ardhi eneo la Hekta 516 Ihumwa (Dodoma) kwa ajili ya kituo kikubwa cha treni za mizigo na makasha; na kumpata Mtaalam wa fidia na utwaaji ardhi.

#### 4.4.1.2 Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania

Mradi unahusisha uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya, kulipa madeni muhimu pamoja na mtaji wa kuanzia wa kuiwezesha ATCL kuendesha shughuli zake. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege 3 ambapo ndege mbili (2) ni aina ya CS 300 zenye uwezo wa kubeba abiria 127 na ndege kubwa moja (1) ya masafa marefu aina ya Boeing 787 yenye uwezo wa kubeba abiria 262.

#### 4.4.1.3 Makaa ya Mawe Mchuchuma

Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma unatekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (hisa asilimia 20) na kampuni ya *Sichuang Hongda Group Limited - SHGL* (hisa asilimia 80) ya China kupitia kampuni ya ubia ya Tanzania - China *International Mineral Resources Limited (TCIMRL).* Mradi unalenga kujenga mgodi wa kuchimba makaa ya mawe kiwango cha tani milioni 3 kwa mwaka. Makaa hayo yatatumika kuzalisha MW 600 za umeme, ambapo MW 250 zitatumika katika mgodi wa chuma - Liganga, na MW 350 zitaingizwa katika Gridi ya Taifa. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya kV 220 kutoka Mchuchuma hadi Liganga. Gharama za mradi hadi kukamilika ni Dola za Kimarekani bilioni 1.2 ambazo zitatolewa na kampuni ya SHGL. Katika mwaka 2017/18, Shilingi milioni 100 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na kusimamia ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi utakaofanywa na wawekezaji; kusimamia ununuzi wa mitambo na mashine; kuwezesha kupokea vifaa vya miradi bandarini na kusafirishwa hadi eneo la mradi; kusimamia ujenzi wa mgodi wa makaa ya mawe na kituo cha kufua umeme; kutoa mafunzo kwa wafanyakazi; na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

#### 4.4.1.4 Chuma Liganga

Mradi wa kuzalisha chuma Liganga unatekelezwa na kampuni ya Tanzania – China *International Mineral Resources Limited*, ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa yenye hisa asilimia 20 na kampuni ya Sichuang Hongda Group Company Limited (SHGL) kutoka China yenye hisa asilimia 80. Mradi utahusisha ujenzi wa mgodi na kiwanda cha kuzalisha chuma, kiwanda hiki kitazalisha tani milioni 1 za chuma kwa mwaka pamoja na ujenzi wa kinu cha kuyeyusha chuma na kutenganisha chuma na madini ya Vanadium na Titanium. Gharama za mradi ni Dola za Kimarekani bilioni 1.7 fedha ambazo zitatolewa na Kampuni ya SHGL. Katika mwaka 2017/18, Shilingi milioni 100 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia utakaofanywa na wawekezaji kwa watakaotakiwa kuhama ili kupisha shughuli za mradi; kusimamia ununuzi wa mitambo na mashine; kuwezesha kuipokea mizigo bandarini na kuipeleka kwenye eneo la mradi; kuthaminisha mali za wananchi na ulipaji wa fidia kwa msongo wa umeme wa Mchuchuma - Liganga; kusimamia ujenzi wa mgodi wa chuma, kiwanda cha chuma na msongo wa umeme wa Mchuchuma - Liganga, mafunzo kwa wafanyakazi na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

#### 4.4.1.5 Shamba la Kilimo cha Miwa na Uzalishaji Sukari Mkulazi

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PPF itaendelea na hatua za kuwekeza kwa ajili ya kilimo cha miwa kwa mashamba ya Mkulazi na Mbigiri na ujenzi wa kiwanda cha sukari. Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya

NSSF na PPF kupitia kampuni ya umiliki ya Mkulazi Holding Company ambapo kila mfuko unamiliki hisa ya asilimia 50. Mradi unahusisha uwekezaji katika eneo la Mkulazi Ngerengere mkoani Morogoro lenye ukubwa wa hekta 63,227 kwa ajili ya kilimo cha miwa na kuanzisha kiwanda cha sukari kinachotarajiwa kuzalisha tani za sukari 200,000 kwa mwaka kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha ajira kwa watu zaidi ya 100,000. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu yanaendelea kwa mwaka 2017/18.

#### 4.4.1.6 Ujenzi wa Mitambo ya Kusindika Gesi Kimiminika, Lindi

Mradi unalenga kuendeleza gesi asilia inayozalishwa katika kina kirefu baharini kwa kuichakata gesi hiyo na kuigeuza kuwa kimiminika kwa lengo la kuisafirisha nje ya nchi ikiwa imesindikwa na pia gesi hiyo iweze kutumika ndani ya nchi. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na makampuni ya mafuta ya kimataifa na wadau wengine. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 13 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kufanya uhakiki wa thamani za mali ili kuwalipa fidia wananchi watakaopisha mradi; kuandaa michoro ya maeneo na mpango kazi wa kuwahamishia waathiriwa wa mradi; kuendesha majadiliano ya makubaliano na Serikali (Host Government Agreement) kuhusu mfumo wa uendelezaji mradi; na kuandaa wataalam wazawa kwa ajili ya kuajiriwa na kuendesha shughuli za mradi.

#### 4.4.1.7 Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi

Mradi unalenga kuendeleza kanda ya Bagamoyo, Kigoma, Ruvuma na Mtwara ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Miradi itakayohusika ni pamoja na:-

a. **Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo:** Mradi unahusisha uendelezaji wa eneo la Bagamoyo kama moja ya maeneo maalum ya uwekezaji kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalaum ya Uwekezaji. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 9.414 zimetengwa kwa ajili ya majadiliano na kuratibu usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani ya mradi awamu ya kwanza; kuratibu uboreshaji wa makazi holela ya maeneo ya makazi ya Kiromo, Mlingotini na Zinga; na kuratibu ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya umeme na maji kufikia eneo la mradi (offsite infrastructure). Wawekezaji wanategemea kuanza kazi ya ujenzi wa bandari mara tu baada ya makubaliano kuridhiwa na Serikali.
b. **Eneo Maalum la Uwekezaji la Mtwara**: Mradi unahusisha uendelezaji wa eneo maalum la uwekezaji katika Mkoa wa Mtwara kama moja ya maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Maeneo Maalaum ya Uwekezaji. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 80 zimetengwa kwa ajili ya kulipia fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi.
c. **Maeneo Maalum ya Uwekezaji ya Kigoma na Ruvuma**: Kwa mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 13.87 fedha za ndani zimetengwa katika maeneo haya

ya SEZ kwa ajili ya kumalizia malipo ya fidia katika maeneo ya mradi yaliyofanyiwa uthamini ya Kigoma na Ruvuma; kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani katika maeneo ya mradi wa Kigoma; kupima viwanja (survey) na gharama za usajili wa hati miliki katika maeneo ya mradi wa Kigoma; na kuendelea kutangaza miradi kitaifa na kimataifa na kuendeleza shughuli zote za maenedeleo ya SEZ ya Ruvuma.

#### 4.4.1.8 Kusomesha kwa wingi kwenye fani na ujuzi adimu na maalum kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na watu na kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu

Mradi unahusisha kusomesha kwa wingi vijana kwenye fani na ujuzi maalum na adimu kuendana na mahitaji ya maendeleo ya viwanda tarajiwa na ustawi wa watu. Katika mwaka 2017/18 Serikali itaendelea kusomesha kwa wingi vijana kwenye fani na ujuzi maalum na adimu kuendana na mahitaji ya maendeleo ya viwanda tarajiwa na ustawi wa watu ikijumuisha. Aidha mradi huu unajumuisha miradi ya:

(i) **Mradi wa Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kukarabati hosteli za wanafunzi, ofisi za watumishi, maabara, nyumba za watumishi, mifumo ya maji, uwanja wa michezo; kuweka lift kwenye jengo jipya; kuanza ujenzi wa kituo mahiri cha magonjwa ya moyo na mishipa ya damu; kuanza ujenzi wa majengo ya kufundishia, mabweni, maabara na nyumba za watumishi wa hospitali ya Mloganzila; na kuongeza na kuboresha miundombinu ya mawasiliano na elimu kwa watumishi.

(ii) **Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa – Dodoma:** katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 1 fedha za ndani kwa ajili ya: ununuzi wa vifaa na vifaa tiba; kuongeza wataalam wa fani za afya na kuwajengea uwezo waliopo; kuanzisha maabara ya kisasa (Cath Lab) kwa ajili ya matibabu ya magonjwa ya moyo na uchunguzi wa vinasaba; kuanzisha huduma ya matibabu ya magonjwa ya figo, njia ya mkojo (Dialysis) na upandikizaji wa figo (Rental Transplant).

#### 4.4.1.9 Uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini

Mradi utahusisha ujenzi wa kituo cha kisasa cha biashara na huduma. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya: kuhakikisha upatikanaji wa hati miliki ya eneo lote la mradi; kuingia ubia na sekta binafsi katika kuendeleza na kuendesha mradi; na kulipia fidia wananchi watatu waliosahaulika kufanyiwa uthamini wa mali zao na kuwezesha upatikanji wa Mshauri Mwelekezi.

### 4.4.2 Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

#### 4.4.2.1 Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha

Mradi wa uchimbaji Magadi Soda unatekelezwa na Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC katika bonde la Engaruka - Monduli (Arusha). Mradi unahusisha ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka yatakayotumika viwandani kuzalisha madawa, vioo na sabuni. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa faida za kiuchumi za mradi; kufanya utafiti wa mazingira; kusimamia ulipaji fidia kupitia fedha za wawekezaji kwa wananchi watakaopisha mradi; kusimamia umilikishwaji wa ardhi; kusaini mkataba wa ubia na kuunda kampuni ya ubia; miundombinu ya kusambaza maji kwa ajili ya matumizi ya kiwanda na jamii; kulipia ada za leseni za madini na tozo ya ardhi; na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

#### 4.4.2.2 Mradi wa kufufua Kiwanda cha General Tyre - Arusha

Kiwanda cha General Tyre Arusha kilianzishwa kwa ajili ya kuzalisha magurudumu kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali za kiuendeshaji, mtaji na soko, uzalishaji wa magurudumu ulisimama mwaka 2009. Kwa kuzingatia umuhimu wa kiwanda hicho, taratibu za kukifufua zimeanza ambapo katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 70 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuainisha njia muafaka ya kutumia eneo la kiwanda na kubainisha aina ya uwekezaji unaofaa katika eneo kilipokuwa kiwanda cha matairi Arusha.

#### 4.4.2.3 Viwanda vya Nguo Eneo la Viwanda – TAMCO Kibaha

Viwanda vya nguo kwa muda mrefu vimekuwa vikikabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu muhimu ya uzalishaji. Katika kutanzua changamoto hiyo, katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 10.94 fedha za ndani kwa ajili ya: kuandaa na kujenga mfumo wa barabara za ndani katika mradi wa nguo na mavazi wenye eneo la ekari 95; kujenga tanki la kuhifadhia maji safi na miundombinu yake; kujenga mabwawa ya maji taka; na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

#### 4.4.2.4 Mradi wa Kuunganisha Matrekta, TAMCO, Kibaha

Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kugharamia uingizaji wa vifaa bandarini na kuipeleka kwenye maeneo ya mradi; kuajiri wafanyakazi; kufanya mafunzo; kuanzisha vituo katika maeneo mengine 8 nchini; na kulipia tozo ya ardhi, kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

#### 4.4.2.5 Kuendeleza kusindika Nyama Dodoma na Kibaha - Pwani

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 190 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi wa viwanda vya kusindika nyama Dodoma na Kibaha – Pwani**.** Shughuli hizo ni pamoja na: kuendelea na kuboresha

taarifa ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa machinjio ya kisasa; na kufungasha nyama kwenye makopo; kutafuta eneo linalofaa kwa ajili ya mradi wa machinjio ya kisasa; kuendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya mradi wa nyama; kuunda kampuni kwa ajili ya mradi huo na kusimamia na kutathimini shughuli za mradi.

#### 4.4.2.6 Kuendeleza Kongane (Clusters) za Viwanda vya Ngozi

Mradi unalenga kutatua changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya viwanda vya ngozi katika eneo la hekta 107 Zuzu mkoani Dodoma ili kuongeza ufanisi kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu duni, ukosefu wa mitaji, masoko na teknolojia duni. Wasindikaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi watapatikana vifuasi na huduma nyingine muhimu kwa urahisi katika eneo moja. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa kongane la sekta ya ngozi na bidhaa za ngozi; kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa Mpango wa Biashara; kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan); kuandaa "Layout Plan and Detailed Design"; kufanya tathmini ya athari ya mazingira (Strategic Environmental Assessment - SEA); ujenzi wa miundombinu ya usafishaji taka; uwekaji wa mfumo wa umeme; ujenzi wa barabara ndani ya kongane; kuandaa Hadidu za Rejea za kuwapata Wataalamu Waelekezi; kusimamia na kuratibu shughuli zote za mradi; na kuanza ujenzi wa baadhi ya majengo ya kufanyia shughuli za viwanda (industrial sheds).

#### 4.4.2.7 Miradi ya Uendelezaji Teknolojia na Ubunifu

**(a) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC)**

Kituo hiki kina jukumu la kuendeleza na kusambaza teknolojia zilizoboreshwa na endelevu kwa ajili ya kilimo na maendeleo vijijini, na kupitia uendelezaji na matumizi ya teknolojia sahihi katika kilimo kwa kutumia mitambo ya kisasa, vifaa vya usambazaji wa maji, vifaa vya ujenzi, usafiri vijijini na nishati. Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 500.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kujenga uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kufanyia majaribio zana za kilimo nchini; kutafiti na kuendeleza teknolojia mbalimbali za kilimo na ufundi vijijini; kujenga maabara kwa ajili ya majaribio ya zana za kilimo nchini; kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya majaribio ya zana za kilimo nchini; kufanya tafiti ya mahitaji ya zana za kilimo na teknolojia za vijijini; na kushirikiana na wajasiliamali na wabunifu katika kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa zana za kilimo.

**(b) Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO)**

TEMDO ni Shirika lenye jukumu la kuhamasisha ubunifu/uundaji wa teknolojia za viwanda, maendeleo ya teknolojia na kuhamasisha kampuni kushindana katika utoaji wa huduma bora za kiufundi. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kuboresha na kutengeneza mitambo ya kusindika

mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mafuta; kubuni, kuendeleza na kuboresha teknolojia za kuteketeza taka ngumu na hatarishi zitokanazo na utoaji wa huduma za afya na huduma za uthibiti kwa lengo la kulinda afya na mazingira; kubuni na kuendeleza mashine na vifaa vya mtambo wa kuzalisha saruji ya moto na bidhaa zake; kubuni na kuendeleza teknolojia ya kuzalisha bidhaa za marumaru kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini; na kubuni na kuendeleza teknolojia ya kutengeneza mitungi ya gesi asilia na vifaa vya matumizi ya gesi asilia (majiko, taa, n.k) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, shughuli za kibiashara na viwandani.

Vile vile, fedha hiyo itatumika kufanya utafiti kuhusu aina ya vifaa vya pikipiki vinavyoweza kutengenezwa nchini; kubuni, kufanya majaribio na kutengeneza utaratibu wa kuunda (manufacturing process) vipuri vya pikipiki hapa nchini; kuendeleza, kufanya majaribio na kuboresha chasili cha mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji; kuendeleza, kufanya majaribio na kuboresha teknolojia ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya upepo; kuendeleza, kufanya majaribio na kuboresha teknolojia ya kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya mvuke unaotengenezwa kwa kutumia mabaki ya mimea na taka za mijini; kuboresha mtambo wa kutengeneza kuni mbadala na mkaa mbadala (biomass briquettes).

Shughuli zingine zitakazofanyika ni kubuni, kuendeleza na kufanya majaribio ya mashine ya kukausha mabaki ya mimea na taka za mijini kwa ajili ya kutengeneza kuni na mkaa mbadala; kubuni, kuendeleza na kufanya majaribio ya mtambo wa kutengeneza mkaa mbadala unaotokana na vumbi la makaa ya mawe; na kuanzisha kituo cha uendelezaji wa shughuli za utengenezaji wa bidhaa na teknolojia za viwandani in Tanzania, na upatikanaji na usimikaji wa mashine mbalimbali na vifaa vya kisasa vya karakana na ofisi ya usanifu na kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo.

**(c) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)**

Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 3.0 zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha na kuhakiki maabara za TIRDO; kuanzisha na kuhakiki maabara ya vipimo vya mafuta na gesi (petrochemical laboratory) ambayo kwa sasa haipo nchini; kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira, kemia na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani; uhakiki na ununuzi wa vifaa katika maabara ya makaa ya mawe; kutafiti vigezo vya uzalishaji wa chuma cha pua (steel bar production parameter) katika viwanda/mashine za kawaida za chuma (conventional rolling mill); kuanzisha na kuhakiki maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory) ambayo haipo nchini kwa sasa; na kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama "leather boards".

#### 4.4.2.8 Mradi wa Uendelezaji wa Viwanda vya Magereza

Mradi unalenga kuboresha huduma za Jeshi la Magereza ili kupunguza utegemezi kutoka Serikalini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 2.2 fedha za ndani kwa ajili ya kununua trekta na mashine mpya kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya mawese na mise katika kiwanda cha mafuta Kwitanga – Kigoma; Kuboresha Viwanda vya kokoto Maweni - Tanga na Msalato - Dodoma kwa kununua mashine mpya kwa ajili ya kuponda kokoto katika maeneo ya Msalato na Maweni; kuanzisha kiwanda kipya cha useremala katika gereza la Isanga - Dodoma; kuanzisha kiwanda kipya cha uchakataji wa chumvi gereza la Lindi.

#### 4.4.2.9 Madini

##### (a) Kuimarisha Usimamizi wa Shughuli za Madini

Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ofisi za Makao Makuu Dodoma na Kanda ya Mashariki; kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali za madini; na kuimarisha ukaguzi wa migodi nchini.

#### 4.4.2.10 Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO

Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kuendeleza maeneo ya viwanda vidogo (Industrial Estates/Parks) ikijumisha ujenzi wa miundombinu ya viwanda katika mikoa ya Manyara, Mtwara, Dodoma, Kagera, Njombe, Katavi na Simiyu; kujenga mabanda ya viwanda 10 katika mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3) na Geita (4); kujenga ofisi za kutolea huduma katika mikoa mipya ya Simiyu na Geita; kuimarisha kituo cha kuendeleza teknolojia cha Shinyanga; kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo vijijini kwa kuzingatia mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja; na kuendelea kusambaza teknolojia vijijini kwa kutengeneza mashine za kuongeza thamani mazao ya kilimo na misitu. Vile vile, Shilingi bilioni 7.1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF) ambao unatoa mikopo midogo kwa wenye viwanda na wafanyabiashara wadogo. Kiasi hiki kitaongeza wigo wa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wengi zaidi.

#### 4.4.2.11 Kilimo cha Mazao

##### (a) Matumizi Bora ya Ardhi kwa Kilimo

Serikali chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) katika mwaka 2017/18 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.26 fedha za ndani kwa ajili ya Kufanya tathmini ya ubora wa ardhi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji vya mto Wami/Ruvu na Pangani kwa lengo la kuainisha aina ya mazao ya kilimo yanayofaa kulimwa na kutoa miongozo ya matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo katika uzalishaji; kuanzisha

mashamba darasa yatakayoainisha teknolojia mbalimbali za kuhifadhi udongo na maji mashambani kwenye halmashauri sita zilizo katika vyanzo vya mito ya Ruvu na Pangani; kuainisha, mashamba na kuyagawa kwa vikundi vya vijana kwa uzalishaji; kuandaa mpango kina wa matumizi bora ya ardhi, kuwezesha upatikanaji wa Hati za haki miliki za kimila (CCROs) kwa mashamba ya wakulima wanaozunguka mashamba 5 makubwa ya kilimo cha Biashara ya Lukulilo, Mkulazi, Pangani, Kitengule na Bagamoyo; kuainisha makundi athirika katika jamii (wanawake, wanaoishi na virusi vya ukimwi na wazee) kwenye halmashauri 5 kwa lengo la kuwapatia ardhi na nyenzo za uzalishaji na hivyo kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo; kuanzisha Kanzidata za mashamba ya uwekezaji, makundi maalum na kilimo cha kibiashara; kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji ya hekta 10,000 zilizotengwa kwa uwekezaji katika kilimo kwenye halmashauri ya Ludewa na eneo la chini la mto Rufiji; na Kufanya utambuzi wa awali kwenye mikoa tisa (9) ya Rukwa, Katavi, Lindi, Kigoma, Ruvuma, Kagera, Shinyanga, Geita na Tabora kwa lengo la kuainisha mashamba mapya ya kilimo cha kibiashara.

**(b) Kilimo cha Mpunga**

Serikali kuu kwa kushirikiana na Halmashauri za Mvomero, Kilosa na Kilombero itatekeleza mradi wa kuongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga katika maeneo yaliyoelekezwa Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara mradi utatekelezwa katika skimu za Mbogokomtonga, Kigugu (Halmashauri ya Mvomero), Mvumi (Halmashauri ya Kilosa), Msolwa Ujamaa na Njage (Halmashauri ya Kilombero). Katika mwaka 2017/18 zimetemgwa Shilingi bilioni 7.08 fedha za nje kwa ajili ya kufundisha juu ya matumizi ya mbolea, mbegu bora, viuatilifu na zana za kilimo kwa wakulima viongozi 4,800 katika skimu 22 na kuanzisha mashamba darasa 80 (FFS) ya mpunga ili kuongeza uzalishaji kutumia kilimo shadidi; kuwezesha usambazaji wa pembejeo za kilimo (mbegu na mbolea) kwa wakulima 4,800 (SRI trained) kutoka skimu 22 za umwagiliaji; kutoa mafunzo kuhusu teknolojia ya uzalishaji mpunga kwa wataalam wa ugani 50 katika skimu 18 za umwagiliaji; na kuwezesha Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Bora (TOSCI) kukagua mashamba ya mbegu, kuchukua sampuli na kupima ubora wa mbegu; na kuwezesha Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kuzalisha aina mpya za mbegu ya mpunga na kusambaza kwa wakulima wadogo.

**(c) Kilimo cha Mahindi**

Katika mwaka 2017/18 Serikali imetenga Shilingi milioni 467.7 fedha za ndani kwa ajili ya kujenga makaushio (drying platforms) ya kisasa 30 na kusambaza makaratasi 30 ya kukaushia (drying sheets) mazao ya chakula katika Halmashauri za Wilaya za Sikonge, Chemba, Kondoa, Chamwino, Manispaa ya Dodoma na Kiteto kwa lengo la kudhibiti sumu kuvu na madhara yake. Aidha, shilingi milioni 907.55 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maghala/kukarabati na kuweka vifaa katika maghala 33 katika Halmashauri za Iringa, Mlele, Msimbo, Songea na Njombe

kwa ajili ya hifadhi ya mahindi chini ya mpango wa COWABAMA.

**(d) Skimu za Umwagiliaji Mpunga**

Katika mwaka 2017/18, Serikali imetenga Shilingi bilioni 2.91 fedha za nje kwa ajili ya uendelezaji wa zao la mpunga kupitia mradi wa *Expanded Rice Production Project* (ERPP) ambapo shughuli zilizopangwa kufanywa ni: kujenga maghala matano (5) katika skimu za umwagiliaji za Njage na Msolwa Ujama katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, skimu ya Mvumi wilayani Kilosa na skimu ya Kigugu na Mbogo Komtonga katika Halmashauri ya wilaya Mvomero; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika maeneo ya Gidahababieg (Hanang), Lwiche (Kigoma), Igwachanya (Njombe), Ibanda na Muhongo (Sengerema) utafanyika; kukamilisha/kuanza ujenzi katika miradi ya umwagiliaji ya Igenge (Misungwi), Dongobesh na Trau (Mbulu) na Itagata (Manyoni); Kukarabati skimu za umwagiliaji za Kiria na Genge (Mwanga), Kongogo (Bahi), Ngongowele na Segeni (Liwale).

**(e) Tafiti za Kilimo**

Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 1.65 fedha za ndani kwa ajili ya: kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa lengo la kuratibu na kusimamia Utafiti wa Kilimo nchini; Kukarabati na kuvipatia vifaa muhimu vya kufanyia utafiti vituo 7 vya Utafiti (Ukiriguru, Ilonga, Seriani, Tumbi, Naliendele, Uyole na Makutopora) nchini ili viweze kuendesha utafiti kwa mazao ya kipaumbele katika mnyororo wa thamani (CVCs); kukarabati Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za mimea (National Plant Genetic Resource Centre) ili kiweze kutoa huduma bora; kuwezesha Taasisi ya Utafiti wa Chai (TRIT) kuendeleza utafiti wa chai; kutafiti teknolojia za kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani kwa mazao ya kipaumbele; na kuendelea na utafiti wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao kwa mazao ya kipaumbele.

**(f) Mafunzo na Ugani wa Kilimo**

Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 5.02 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kufundisha wanafunzi 2,200 ngazi ya Astashahada na Stashahada; kukarabati Vyuo vya Kilimo Maruku na Mubondo; kuipatia Idara Makao makuu na Vyuo vya Mubondo na Igurusi vitendea kazi; kuandaa mtaala wa Diploma ya Matumizi Bora ya Ardhi (Diploma in Land Use Planning) katika mfumo wa Moduli; na kuboresha (review) mitaala ya Stashahada ya Kilimo (Diploma in General Agriculture), Mboga, Maua na Matunda (Diploma in Horticulture).

**(g) Kuboresha Hifadhi ya Taifa ya Chakula**

Katika kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka NFRA, Serikali katika mwaka 2017/18 imetenga Shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani kwa ajili ya kuiwezesha NFRA kujenga ghala moja kwa ajili ya hifadhi ya mahindi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na kununua, kuhifadhi na kusambaza nafaka kwenye maeneo yenye upungufu wa

chakula. Aidha, shilingi bilioni 1.92 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya Kujenga maghala manne yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 kila moja na kuweka vifaa vya ghala katika mikoa ya Mwanza, Singida, Kigoma na Manyara.

**(h) Mfuko wa Taifa wa Pembejeo**

Katika mwaka 2017/2018, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) imetenga Shilingi bilioni 7.781 fedha za ndani kwa ajili ya kutoa mikopo ya matrekta makubwa mapya 71; kutoa mikopo 80 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo; mikopo minne (4) kwa ajili ya ukarabati wa zana za kilimo; mikopo sita (6) kwa ajili ya miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi; mikopo mitatu (3) kwa ajili ya fedha za kuendeshea shughuli za shamba; mikopo mitatu (3) kwa ajili ya kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji samaki; mikopo mitatu (3) kwa ajili ya zana unganishi; na mikopo mitato (5) kwa ajili ya zana za kusindika na vifungashio vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

### 4.4.2.12 Mifugo

**(a) Kuimarisha Uzalishaji Katika Sekta ya Mifugo**

Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa mitamba na mbegu bora kwenye mashamba matano (5) kwa kununua ng'ombe wazazi 100 na mashine mbalimbali za shamba; kuimarisha vituo vya uhimilishaji vya NAIC Usa River na Sao Hill; kujenga minada ya upili miwili (2) mipakani (Longido na Kirumi) na kukarabati minada ya upili (Nyamatala na Kasesya) ili kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kuchimba malambo matatu (3) katika Wilaya za Hanang, Kilosa na Rufiji; kuimarisha mashamba nne (4) ya kuzalishaji mbegu bora za malisho na kuyapatia vitendea kazi muhimu; kutambua, kutenga na kutangaza kwenye gazeti la Serikali maeneo ya nyanda za malisho kwenye vijiji 10 za Wilaya za Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Hanang, Kilombero, Iramba, Kiteto na Rufiji; na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji mifugo na masoko.

**(b) Miundombinu ya Maji na Maeneo ya Malisho**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 873.3 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kukarabati na kujenga malambo matatu (3) kwa ajili ya mifugo katika Wilaya za Kilosa, Hanang na Rufiji; kupima na kumilikisha maeneo ya ufugaji katika vijiji 10 vya Wilaya za Kilosa, Ngorongoro, Mvomero, Iramba, Kiteto, Rufiji na Hanang; kukarabati mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho pamoja na kuainisha na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**(c) Magonjwa ya Milipuko na Magonjwa ya Kipaumbele**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuzalisha chanjo za mifugo katika kituo cha Kibaha na kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo (Ndigana Kali); kutoa elimu kwa wadau kuhusu umuhimu wa

magonjwa haya katika biashara ya mifugo na mazao yake kitaifa na kimataifa ili kuchukua hatua za tahadhari; na kuendelea na ukarabati wa majosho na kuhimiza utumiaji wa majosho na chanjo.

**(d) Vituo vya Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Mifugo**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) kuratibu utafiti, mafunzo na ugani; kuendeleza kosaafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na wanyama hai; kukarabati Kampasi za Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) Madaba, Kikulula, Morogoro na Mabuki; na kuwezesha LITA kutoa mafunzo ngazi ya cheti na diploma kwa wanafunzi 2,600 kwa mwaka.

**(e) Uwekezaji wenye Tija katika Ranchi za Taifa (NARCO)**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 126.1 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuzalisha jumla ya ndama 4,269; kununua ng'ombe 2,100; kununua ng'ombe wazazi 100 na kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa Ruvu.

#### 4.4.2.13 Uvuvi

**(a) Kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 700 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kujenga na kukarabati miundombinu ya uvuvi katika vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi, mialo, karakana ya kutengenezea maboti (Boatyards) na vituo vya uthibiti wa ubora na viwango; kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa njia ya ushirikishaji jamii za uvuvi; kuiwezesha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA); kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI); kuiwezesha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU).

**(b) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari kubwa ya uvuvi ambayo itawezesha meli zinazovua katika bahari kuu kutia nanga nchini ili kuwezesha Serikali kusimamia kwa ufanisi uvuvi katika bahari kuu.

**(c) Ufugaji wa Viumbe kwenye Maji**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kujenga na kuboresha mabwawa matano katika vituo vya ufugaji samaki katika maji baridi vya Mwamapuli - Tabora, Ruhila - Songea, Kingolwira - Morogoro, Nyigedi - Lindi na Nyamirembe - Chato na kujenga kituo cha ufugaji samaki katika maji chumvi cha Machui – Tanga; kuanisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria; kuwezesha vituo vinne vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Bukoba, Kilimanjaro, Mwanza na Mara; na kuzalisha na kupandikiza

vifaranga vya samaki katika marambo na mabwawa ya asili kumi (10) katika mikoa ya Shinyanga, Tanga, Lindi, Mtwara, Songwe, Manyara, Arusha, Pwani, Simiyu na Mwanza na kwenye skimu tano za umwagiliaji miwa na mpunga (Namtumbo, Kilombero, Lower Moshi, Korogwe na Mvomero) ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

#### 4.4.2.14 Maliasili na Misitu

**(a) Mradi wa Kilombero and *Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management* (KILORWEMP):** Katika mwaka 2017/18, mradi utaendelea kutekeleza usimamizi endelevu wa ikolojia ya ardhi oevu ya Bonde la kilombero na Mto Rufiji kwa kuboresha maisha ya wananchi.

**(b) Mradi wa Kuimarisha Mtandao wa Hifadhi ya Misitu kwa Utunzaji wa Bioanuai Tanzania:** Katika mwaka 2017/18, mradi utaendelea na ujenzi wa ofisi sita za misitu ya Hifadhi za Mazingira Asilia (Chome, Magamba, Minziro, Mkingu na Uzungwa); vituo 15 katika hifadhi hizo; kuandaa na kutekeleza makubaliano ya usimamizi wa pamoja; kuimarisha miundombinu ya utalii ikilojia; na kutangaza vivutio vya utalii katika hifadhi 12 za Mazingira asilia.

**(c) Mradi wa Kuwezesha Jamii Katika Usimamizi Shirikishi wa Misitu na Mabadiliko ya Tabia Nchi:** Katika mwaka 2017/18, mradi utaendelea kuboresha miundombinu ya vyuo vya misitu; kujenga uwezo wa watumishi wa halmashauri za wilaya na Taasisi zisizo za kiserikali katika kutoa huduma za mipango na shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Misitu, Mkakati wa Kupunguza Hewa Ukaa na Ukataji Miti (MKUHUMI), mabadiliko ya tabianchi; na kurekodi vipindi 100 vya redio katika Wilaya za Bagamoyo, Kilombero, Kiteto na Same.

### 4.4.3 Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Watu

Kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21), maendeleo ya watu ndiyo lengo kuu la kuchochea uchumi wa viwanda na mabadiliko ya muundo wa uchumi. Mabadiliko haya ya kiuchumi yanapaswa kupanua wigo na fursa kwa wananchi wa mijini na vijijini kuchagua namna ya kushiriki katika uzalishaji, ajira, na matumizi katika kaya zao. Haya yote yanawezekana kwa kuwekeza katika elimu, ujuzi, na huduma za afya kwa wananchi. Ili kufanikisha malengo ya mpango wa maendeleo, vipaumbele katika sekta za jamii vitazingatia mabadiliko yanayotokea nchini, ikiwemo idadi ya watu na muundo wake, viwango vya umasikini na viashiria mbalimbali vya upatikanaji na ubora wa huduma za elimu, afya, na maji safi na salama.

Hivyo, katika mwaka 2017/18 utatilia mkazo kuimarisha huduma za afya ya msingi ili kupunguza vifo vya watoto wachanga vinavyotokana na uzazi; kuimarisha upatikanaji wa lishe bora na virutubisho ili kupunguza kudumaa kwa watoto;

kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini; kuboresha mazingira ya utoaji elimumsingi na sekondari ili kuongeza ubora na stadi za maisha kwa wahitimu; na kuimarisha miundombinu na huduma katika miji inayokua haraka.

#### 4.4.3.1 Elimu, Sayansi na Teknologia

##### 4.4.3.1.1 Elimumsingi

**(a) Programu Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu**

Programu inalenga kuhakikisha kuwa watoto wanaojiunga na darasa la I – IV na walio nje ya mfumo rasmi wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 39.79 fedha za nje kwa ajili ya kuandaa, kuchapa na kusambaza mitaala pamoja na machapisho yake (Mihtasari na Kiongozi cha Mwalimu) kwa elimu ya awali, darasa la kwanza hadi la sita; kuhuisha mitaala ya stashahada na shahada katika vyuo vya elimu ili kuingiza masuala ya KKK, kuchapa na kuisambaza kwenye vyuo vyote vya ualimu; na kuandaa na kuchapa vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya Elimu ya Awali, darasa la kwanza hadi la sita; ununuzi wa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum (mashine za nukta nundu), vifaa vya upimaji wa kiafya unaoweza kuathiri ujifunzaji, vifaa kwa vituo maalum vya msaada wa kitabibu); na kuimarisha matumizi ya maji safi na vyoo shuleni (School Water Sanitation & Hygiene –SWASH).

**(b) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu**

Programu inalenga kuboresha mazingira ya shule ili elimu inayotolewa ikidhi ubora wa utoaji unaotakiwa. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 120.38 fedha za nje kwa ajili ya: kununua vifaa vya maabara awamu ya pili; kuanza ujenzi wa shule ya kisasa ya sekondari katika mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuongeza miundombinu ya elimu katika makao makuu ya nchi; ujenzi wa vyumba 2,000 vya madarasa kwa shule za msingi na sekondari; ukarabati wa shule 17 kongwe za sekondari; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji na vyoo katika shule za msingi 1,000 na sekondari 2,000 katika mikoa ya Dodoma, Mara, Tabora, Mwanza, Kagera, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Simiyu na Shinyanga; kufanya mapitio ya sheria ya elimu, sura ya 353 na Sheria za taasisi zilizo chini ya Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (P4R).

**(c) Mradi wa Kuchapa Vitabu vya Kiada – Taasisi ya Elimu Tanzania**

Mradi unalenga kuwawezesha wanafunzi kujisomea na kufanya rejea baada ya muda wa masomo. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 40 fedha za ndani kwa ajili ya: kuchapa vitabu vya Kiada kwa darasa la IV na kidato cha kwanza hadi cha VI; kuboresha mtaala wa elimu ya ualimu na kuandaa moduli zake; kuratibu na kuendesha programu za ufundishaji na ujifunzaji kupitia TEHAMA; na kuendesha mafunzo kazini kwa walimu wa elimu msingi na sekondari ili kuboresha utendaji kazi.

#### (d) Mamlaka ya Elimu Tanzania

Mamlaka ya Elimu Tanzania inalenga kutoa ufadhili katika utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 10 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nane (8) za walimu katika shule za sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi; ujenzi wa vyoo 50 katika shule zenye upungufu mkubwa; ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika taasisi 20 za elimu na mafunzo; kutoa mikopo kwa taasisi za elimu kumi (10) kuwezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia; kuendelea na ukarabati wa shule kongwe za sekondari za Serikali nchini; na kuendelea na ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike katika shule za sekondari kwenye mazingira magumu.

### 4.4.3.1.2 Ufundi na Teknolojia

#### (a) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi

Mradi unalenga kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi nchini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 54.80 fedha za ndani na bilioni 5.38 fedha za nje kwa ajili ya: ujenzi wa vyuo vya ufundi Stadi vya Kagera, Chato Chunya, Kilindi na Nyasa; kukamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi vya Namtumbo na Kihonda; kukamilisha ujenzi wa karakana 11 za vyuo vya ufundi stadi vya mikoa ya Lindi (4), Pwani (3) na Manyara (4); ujenzi wa mabweni mawili (2) katika chuo cha ualimu wa ufundi stadi Morogoro; kufuatilia ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vya mikoa ya Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa; na kuendesha na kusimamia mafunzo ya ufundi stadi ya muda mfupi na mrefu katika vyuo vya ufundi stadi 761 nchini vikiwemo 29 vinavyomilikiwa na VETA.

#### (b) Mradi wa upanuzi na ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha

Mradi unalenga kufanya upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani na bilioni 14. 562 fedha za nje kwa ajili ya: ujenzi wa jengo la madarasa na maabara kwa fani za madini na vito, uhandisi wa vifaa vya tiba, uhandisi wa mawasiliano ya anga na teknolojia ya mawasiliano ya habari; kukarabati na kununua vifaa vya karakana za useremala, uhandisi magari, na uhandisi mitambo; kuboresha elimu ya ufundi kwa kugharamia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi 25 (wanataaluma 15 na waendeshaji 10); kuhuisha mitaala 12 ya programu zilizopo za ufundi sanifu; kuendeleza shamba la mafunzo ya kilimo na umwagiliaji la Oljoro; na kununua mashine na mitambo ya kisasa.

#### (c) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo

Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka

2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati na kuboresha miundombinu ya vyuo kumi (10) vya Maendeleo ya Wananchi; kujenga uwezo kwa wakufunzi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu; kununua vifaa, mitambo na mashine za kisasa za kufundishia na kujifunzia; kufuatilia upatikanaji wa hati miliki za ardhi ya vyuo; na kuchambua hali halisi ya rasilimali zilizopo katika vyuo ikiwemo wakufunzi, watumishi wasio Wakufunzi, miundombinu na Vifaa vya kujifunzia na kufundishia.

**(d) Mradi wa Kuimarisha Elimu na Stadi za Kazi ili Kuzalisha Ajira**

Mradi unalenga kujenga mifumo na uwezo katika kutoa mafunzo na stadi za kazi katika ngazi zote. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 57.78 fedha za nje kwa ajili ya: kuandaa mwongozo wa utekelezaji kwa kuhusisha wadau; kukamilisha uundwaji wa Baraza la Kitaifa la kuendeleza na kusimamia Stadi za kazi; kutengeneza mfumo wa namna ya kuunda na kutumia *Students Voucher Scheme* kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na wadau; kuandaa mfumo huishi wa taarifa (Online Information System) kuhusu utoaji wa elimu na mafunzo katika vyuo na taasisi zote za elimu na mafunzo kwa kushirikiana na TCU, NACTE na VETA; na kujenga uwezo wa Taasisi zinazosimamia na kuratibu elimu ya juu, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**(e) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Maktaba ya Mkoa - Dodoma**

Mradi unalenga kuwapatia wananchi fursa ya kupata maarifa na ujuzi kwa kujisomea vitabu. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi milioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa maktaba ya mkoa wa Dodoma.

#### 4.4.3.1.3 Elimu ya Juu

**(a) Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 427.554 zimetengwa kwa ajili ya: kutoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi 124,884 ikijumuisha wanafunzi 29,328 wa mwaka wa kwanza na 93,295 wanaoendelea na masomo na wanafunzi 2,261 watakaopewa ruzuku. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 327.554 zinatokana na mfuko mkuu wa Serikali na Shilingi bilioni 100.319 zinatokana na marejesho kutoka kwa wanufaika wa mikopo.

**(b) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo vya Ualimu**

Mradi unalenga kuimarisha mafunzo ya ualimu. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 15.690 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa na ukarabati wa vyuo sita (6) vya ualimu vya Kleruu, Mpwapwa, Dakawa, Tabora, Butimba na Marangu; na ukarabati wa miundombinu ya maktaba na maabara za TEHAMA katika vyuo vya ualimu 35 ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wakufunzi na wanachuo.

**(c) Ukarabati na Upanuzi wa Vyuo Vikuu**

**(i) Mradi wa Ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 (DIT Teaching Tower) awamu ya pili lenye maabara 6 zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 54 kila moja, kumbi za mihadhara 2 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kila moja, madarasa 6 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 40 kila moja, madarasa 3 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 kila moja pamoja na ofisi 14 za walimu; na kutekeleza miradi 30 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii.

**(ii) Mradi wa Ujenzi na Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa mabweni nane (8) ya wanafunzi, ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara, ujenzi wa jengo la kitaaluma kwa ajili ya programu za sayansi na Teknolojia, kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, kuboresha mifumo ya usambazaji wa maji katika kampasi kuu Mzumbe; ukarabati wa ofisi za watumishi kampasi ya Dar es Salaam; ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kampasi ya Mbeya; na kugharamia mafunzo ya watumishi 36 katika shahada za uzamili na uzamivu.

**(iii) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ili kuzalisha wataalamu wenye weledi na umahiri kwa kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kukarabati hosteli za wanafunzi awamu ya IX, madarasa, karakana ya useremala, jengo la uchapishaji, nyumba za watumishi na barabara za maegesho ya magari; kukamilisha ujenzi wa jengo la madarasa na ofisi (Lands Building) awamu ya tano; na kujenga hosteli za wanafunzi 2,000 awamu ya I, jengo la maabara ya matumizi mbalimbali (Multi Purpose Laboratory), miundombinu mipya ya TEHAMA na mfumo wa maji taka na umeme jua.

**(iv) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani kwa ajili ya kukarabati vyumba sita (6) vya mihadhara na kukamilisha ujenzi wa maabara kampasi ya Solomon Mahlangu; na kujenga wa hosteli (4) za wanafunzi; kukarabati nyumba 60 za

watumishi.

**(v) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam – Kampasi ya Dar es Salaam:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 5.5 fedha za ndani kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kuatamia ubunifu mpya kitakachojumuisha maeneo mbalimbali ya kitaaluma; kukarabati bweni Na. 5 – Kampasi ya J. K. Nyerere Mlimani; kukarabati miundombinu ya maji safi na maji taka; kujenga kituo cha Buyu – Zanzibar (awamu ya II) kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari; kujenga ofisi mpya ya michezo katika viwanja vya michezo vya chuo kikuuu cha Dar es Salaam na kuongeza ghorofa mbili (2) na samani katika mabweni mapya yaliyojengwa; kuongeza vifaa tiba katika kituo cha afya cha chuo kikuu cha Dar es Salaam.

**(vi) Mradi wa Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma:** Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara, madarasa na ofisi katika Kitivo cha Sayansi Asilia na Hisabati; na kujenga ukumbi wa mihadhara katika Kitivo cha Sayansi za Ardhi; kukarabati mabweni, madarasa na majengo mengine ya chuo; na kununua samani za ofisi, makazi, madarasa, maabara na mabweni ya wanafunzi.

**(vii) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kukarabati miundombinu ya chuo na kukamilisha ujenzi wa jengo la maktaba – Kampasi ya Rukwa; kuandaa mpango kabambe wa upanuzi wa chuo; kufanya tathmini ya mali za wananchi waishio katika eneo la hekta 511 la chuo ili kupisha shughuli za upanuzi wa chuo – Kampasi Kuu Mbeya; kuongeza eneo la Kampasi ya Rukwa kutoka hekta 48 hadi 500; na kuanza ujenzi wa kituo cha atamizi za teknolojia (Technology Incubation Centre).

**(viii) Mradi wa Ujenzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST):** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kufanya utafiti na upembuzi yakinifu kwa ajili ya Kampasi ya Tengeru; kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi ya ardhi – Kampasi ya Tengeru; kuandaa michoro ya ujenzi wa jukwaa, vyoo na barabara kwa ajili ya kiwanja cha michezo na mfumo wa maji safi; kujenga mfumo wa uondoaji wa maji taka, mabweni ya wanafunzi, majengo ya ofisi (Kampasi ya Tengeru) kwa ajili ya watumishi 200; vyumba 10 vya madarasa, kumbi 6 za mikutano

na kituo cha afya; na kuanzisha maabara maalum na kununua vifaa vya sayansi ya miamba.

**(ix) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE):** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya: kujenga kituo cha utafiti, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kukarabati miundombinu ya umeme, kupata ardhi kwa ajili ya upanuzi wa chuo, kufanya upanuzi wa maabara za sayansi, vyumba vya nadarasa (awamu ya II) na mfumo wa maji taka; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na kununua vifaa vya maabara na madawa (chemicals).

**(x) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere:** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya chuo hususan madarasa, nyumba za watumishi na ununuzi wa samani.

**(xi) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MUCCOBS):** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.3 fedha za ndani kwa ajili ya kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja; kukarabati kumbi za mihadhara, madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi.

**(xii) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE):** Mradi unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara, ujenzi wa maabara mbili (2) za sayansi, ofisi; uwekaji umeme jua na uchimbaji wa visima vya maji safi.

**(xiii) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Huria: Mradi** unalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kujenga maabara ya sayansi, hostel za wanafunzi, na vyumba vya madarasa – Makao Makuu Bungo Kibaha; kujenga ofisi za watumishi, ukumbi wa mihadhara na vyumba vya maabara ya kompyuta katika vituo vya mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mwanza, Lindi na Manyara; kukarabati vituo vya mikoa ya Morogoro (awamu ya Pili), Songwe, Kilimanjaro, Lindi, Zanzibar na Simiyu pamoja na vituo vya uratibu vya Chato, Kibondo, Kasulu, Nachingwea na Serengeti.

**(d) Mradi wa Kuimarisha Utafiti, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

Mradi unalenga kuboresha uhawilishaji teknolojia na ubunifu. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 10 fedha za ndani na bilioni 3.671 fedha za nje kwa ajili ya kufadhili miradi mipya na inayoendelea ya utafiti katika maeneo ya viwanda, TEHAMA, kilimo, afya, mazingira na maliasili; kuendeleza na kuanzisha atamizi za ubunifu; kudhamini watafiti kutoka Taasisi za utafiti za umma kusoma shahada za uzamivu katika vyuo vya ndani, na kuimarisha mfumo wa kuhawilisha teknolojia kutoka makampuni ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi ili kujenga uwezo wa ndani katika uendelezaji na uhawilishaji wa teknolojia; kudhamini watafiti kutoka Taasisi za utafiti za umma kusoma shahada za uzamivu katika vyuo vya ndani ya nchi pamoja na kuimarisha mfumo wa kuhawilisha teknolojia kutoka makampuni ya uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi ili kujenga uwezo wa ndani katika uendelezaji na uhawilishaji wa teknolojia.

**(e) Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Mionzi ya Nguvu za Atomiki**

Mradi unalenga kudhibiti matumizi salama ya vyanzo vya mionzi, kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia nchini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ukaguzi wa migodi sita (6) mikubwa inayofanya kazi na migodi mingine itayobainika, ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo; kusajili vyanzo vya mionzi 1,045 ili kuvitambua na kuhifadhi mabaki ya mionzi yasilete madhara katika mazingira na viumbe hai; na kufungua vituo vya Kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Nyanda za Juu katika Mkoa wa Mbeya.

### 4.4.3.2 Afya na Maendeleo ya Jamii

#### 4.4.3.2.1 Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa

**(a) Hospitali ya Rufaa Mbeya**: Mradi unalenga kuendelea na ujenzi na ununuzi wa vifaa katika hospitali ya rufaa ya Mbeya. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani kwa ajili ya kukarabati jengo la daraja la kwanza na kukamilisha ujenzi wa jengo la watoto hivyo kuongeza uwezo kwa hospitali kutoka vitanda 477 vya sasa mpaka vitanda 605; kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma za radiolojia.

**(b) Hospitali ya Rufaa Mtwara:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali.

**(c) Hospitali ya Magonjwa ya Kuambukiza Kibong'oto:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na ukarabati wa wodi za wagonjwa na maabara; na kutoa elimu kwa watalaam mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sugu.

**(d) Hospitali ya Mirembe na Isanga:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa uzio

kuzunguka eneo la hospitali; kukarabati wodi za wagonjwa; na kununua vifaa na vifaa tiba.

(e) **Taasisi ya Saratani Ocean Road:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shillingi bilioni 14.5 fedha za ndani kwa ajili ya kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na PET Scan; kuimarisha shughuli za mkoba (outreach); na kuimarisha upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani.

(f) **Hospitali ya Taifa Muhimbili:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 18 fedha za ndani kwa ajili ya kuanzisha huduma za kubadilisha figo; kuanzisha huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusikia pamoja na kununua vifaa vya kusaidia kusikia; kuanza ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (Private Wing); na kununua vifaa, vitendanishi na vifaa tiba.

(g) **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**: Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 3.8 fedha za ndani kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wataalam wa upasuaji wa kubadilisha Nyonga na Goti; kuanza upasuaji wa vivimbe kwenye mishipa ya damu ya ubongo; kununua vifaa na vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya jengo la MOI awamu ya III na kulipa deni la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

(h) **Hospitali ya Bugando:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi milioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya kukarabati jengo la kliniki za wagonjwa wa nje; kukamilisha ujenzi wa kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na kununua mashine ya *Brachytherapy* kwa ajili ya matibabu bora ya saratani.

(i) **Hospitali ya KCMC:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi milioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa wodi na hosteli za wagonjwa wa saratani.

#### 4.4.3.2.2 Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

Mradi unalenga kuboresha hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 236 fedha za ndani na milioni 409.94 fedha za nje kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya.

#### 4.4.3.2.3 Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza

Mradi unalenga kuimarisha huduma za kupambana na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kupitia huduma za chanjo, na afya mipakani. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 36.5 fedha za ndani na bilioni 104.304 fedha za nje kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kwa kununua na kusambaza chanjo

kulingana na mahitaji ya chanjo.

#### 4.4.3.2.4 Mradi wa Kupunguza Vifo vya Uzazi (SMRP)

Mradi unalenga kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 8.6 fedha za ndani kwa ajili ya kuboresha huduma za uchunguzi za uzazi salama kwa kununua mashine 65 za Ultra Sound kwa ajili ya vituo vya afya; kuendelea kuboresha upatikanaji wa damu salama kwa kuongeza vituo vitano (5) vya benki za damu salama katika mikoa yenye takwimu ya vifo vingi vitokananvyo na uzazi vya Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Manyara; na upanuzi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili viweze kutoa huduma za upasuaji wa dharura wakati wa kujifungua.

#### 4.4.3.2.5 Chakula na Lishe

Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi milioni 100 fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa afua za lishe kama ilivyoainishwa katika Mpango Shirikishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (2016/17 – 2020/21). Katika kipindi hiki afua zitakazotekelezwa ni pamoja na: utoaji wa huduma za lishe kwa wakina mama wajawazito, na watoto wadogo; kukuza na kuimarisha usimamizi shirikishi wa matibabu ya utapiamlo; kuendelea kutoa huduma za urutubishaji wa unga, mafuta na uongezaji wa madini jotokatika chumvi kwa mikoa yote nchini; kuendelea kufanya tafiti na kuishauri Serikali na wananchi kwa ujumla juu ya lishe bora na namna ya kuutokomeza utapiamlo; kujenga uwezo wa wataalam wengine kuhusu masuala ya lishe; na kuendelea na ukusanyaji wa takwimu na taarifa za lishe nchini pamoja na utoaji wa kadi alama ya lishe.

### 4.4.3.3 Maji na Usafi wa Mazingira

#### 4.4.3.3.1 Miradi ya Kuboresha Huduma za Maji Vijijini

Mradi unalenga kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini kwa kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya vijiji 10 katika Halmashauri zote nchini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 220 fedha za ndani na bilioni 43.41 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika mikoa kame ya Dodoma (Bahi, Kondoa, Chemba, Mpwapwa na Kongwa), Shinyanga (Kishapu, Shinyanga), Singida (Mkalama, Ikungi, Iramba, Itigi), Tabora (Urambo, Sikonge), Arusha (Longido, Monduli), Pwani (Kisarawe, Kibaha, Mkuranga), Manyara (Simanjiro, Kiteto, Hanang'), Katavi (Mlele), Lindi (Ruangwa, Newala), Mtwara (Tandahimba, Nanyamba, Namtumbo, Newala); Songwe (Ileje, Songwe, Momba, Mbozi), Simiyu (Maswa, Bariadi, Meatu); ujenzi wa mradi wa Same – Mwanga – Korogwe; ujenzi na ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa ya maji vijiji vya Kidete (Kilosa-Morogoro), Sekeididi (Kishapu-Morogoro), Iguluba (Iringa), Habiya (Itilima-

Simiyu), Wegero (Butiama-Mara), Kawa (Nkasi-Rukwa), Mwanjoro (Meatu-Simiyu), Nanja (Monduli-Arusha), Masuguru (Bagamoyo-Pwani) na Matwiga (Chunya-Mbeya); na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji katika Halmashauri za Ismani (Iringa), Hedaru, Sand Dam (Same) Ngorongoro, Muze (Sumbawanga) pamoja na miradi ya pembezoni mwa maziwa makuu (Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika).

#### 4.4.3.3.2 Mradi wa Kuboresha Huduma za Maji, Dar es Salaam

Mradi unalenga kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea na kuanza utekelezaji wa miradi mipya chini ya Mpango Maalum wa kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 27.5 fedha za ndani na bilioni 45 fedha za nje kwa ajili ya: kukarabati miundombinu ya usambazaji maji ili kupunguza upotevu wa maji; kujenga na kukarabati mtandao wa usambazaji maji katika maeneo ya Jiji; ujenzi wa mfumo wa maji kutoka Kibamba kwenda Mloganzila; ujenzi wa bomba kuu la kutoka Ruvu Chini hadi matanki ya Chuo cha Ardhi; upanuzi wa mtambo na ujenzi wa bomba kuu la kusambaza maji na ujenzi wa matanki ya Kimara; kujenga miundombinu ya mfumo wa maji taka katika Jiji; na ujenzi wa dampo la taka ngumu; na kusambaza maji kutoka katika visima virefu vya Kimbiji na Mpera katika maeneo ya Mkuranga, Chamazi, Msongola, Chanika, Gongolamboto, Pugu, Kitunda, Uwanja wa Ndege, Kinyerezi, Vituka, Kiwalani na Vingunguti.

#### 4.4.3.3.3 Mradi wa Maji Ziwa Victoria

Mradi unalenga kuboresha huduma za maji katika maeneo ya Nzega, Igunga, Tabora na Sikonge kutoka Ziwa Victoria. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 12 fedha za ndani na bilioni 20 fedha za nje kwa ajili ya utekeklzaji wa mradi wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda Tabora, Igunga, Nzega, Sikonge, Uyui, Isaka na Kagongwa; Tinde, Malampaka, Sumve, Busega, Bariadi, Langabilili Mwanhunzi, Mwadui, Kishapu, Kolandoto, Malya na Maganzo.

#### 4.4.3.3.4 Miradi ya Kuboresha Huduma za Maji Mijini

Mradi unalenga kukamilisha miradi 6 katika miji mikuu ya mikoa ya Mtwara, Sumbawanga, Lindi, Kigoma, Musoma na Babati. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 98 fedha za ndani na bilioni 102.5 fedha za nje kwa ajili ya:

(a) **Musoma**: kukamilisha ujenzi wa chanzo *(intake)* cha maji; kukamilisha ujenzi wa chujio la kusafisha maji; kulaza bomba kuu la kusafirisha maji; kulaza mabomba ya kusambaza maji na ujenzi wa eneo la kumwaga majitaka (*sluge digester)***.**

(b) **Mtwara na Babati:** uboreshaji wa chujio la majisafi na upanuzi wa mtandao wa majisafi katika Miji hiyo na uboreshaji wa usafi wa mazingira katika Miji ya Mtwara, Babati, Lindi, Kigoma na Sumbawanga.

(c) **Manispaa ya Kigoma/Ujiji:** kukamilisha ujenzi kitekeo cha maji, ujenzi wa *pumping station,* ujenzi wa matanki 6 ya maji yenye jumla ya mita za ujazo 10,500, ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 122.8, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 16.9, na ujenzi wa mabwawa 2 ya kutibu majitaka.

(d) **Lindi:** kukamilisha; ujenzi wa chujio la maji lenye uwezo wa kusafisha maji mita za ujazo 7,500 kwa siku, ujenzi wa matanki mawili maeneo ya Mtanda na *Central* ya maji yenye ukubwa wa mita za ujazo 3,000 na 2,000, ulazaji wa bomba kuu la maji umbali wa kilomita 11.5 na mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 27 na ujenzi wa mabwawa mawili ya kutibu majitaka:

(e) **Sumbawanga:** kukamilisha ujenzi wa chujio la maji na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji kilometa 25. Kukamilisha na kuendelea kupanua miradi ya maji katika miji mikuu ya Mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe, Katavi na Songwe.

(f) **Mpanda:** kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika mji wa Mpanda. Mradi huu utakapokamilika jumla ya wakazi 60,000 watanufaika.

(g) **Bariadi:** kukamilisha ujenzi wa matanki mawili ya maji katika maeneo ya Somanda na Sima (lita 135,000) na (lita 680,000).

(h) Ujenzi wa miradi katika miji midogo na miji mikuu ya wilaya tisa (9) ya Kisarawe, Chunya, Orkesumet, Ilula, Makambako, Korogwe, Tunduma, Mangaka na Omulushaka/Kayanga yenye uhaba mkubwa wa maji pamoja na kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika makao makuu ya Wilaya mpya za Songwe, Tanganyika, Kibiti na Malinyi.

#### 4.4.3.3.5 Miradi Mikubwa ya Maji ya Kitaifa

Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 13 fedha za ndani na bilioni 6.0 fedha za nje kwa ajili ya ukarabati wa mifumo ya maji katika miradi ya kitaifa ya Mugango-Kiabakari, Makonde, Wanging'ombe, Maswa na kupanua mifumo ya usambazaji maji katika miradi ya kitaifa ya Masasi-Nachingwea na Chalinze. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kumalizia mradi wa Chalinze awamu ya pili na utekelezaji wa mradi wa maji wa Chalinze (awamu ya III); kukarabati mfumo wa maji katika maeneo yanayopata huduma kutoka miradi ya kitaifa ya Handeni *Trunk Main* (HTM), Makonde, Maswa, Wanging'ombe na Masasi – Nachingwea.

#### 4.4.3.3.6 Mradi wa Kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mtwara-Mikindani

Mradi unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma za maji katika Manispaa ya Mtwara – Mikindani. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

#### 4.4.3.3.7 Mradi wa Ujenzi wa Mabwawa ya Maji
Mradi unalenga kuboresha huduma za maji katika miji ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Nzega, na Monduli. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 14.893 fedha za ndani na bilioni 3.0 fedha za nje kwa ajili ya kulipa fidia na kuanza ujenzi wa mabwawa makubwa ya Kimkakati ya Kidunda (Morogoro), Farkwa (Dodoma) na Ndembera (Iringa) na kukarabati mabwawa manne ya ukubwa wa kati ambayo ni Nkiniziwa na Itobo (Nzega), Lemioni na Enguikment II (Monduli).

### 4.4.3.4 Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

#### 4.4.3.4.1 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana
Mfuko unalenga kuwawezesha vijana kiuchumi ili waweze kujiajiri na kuwa wajasiliamali. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana vikiwemo vikundi vya wenye ulemavu kulingana na miradi iliyobuniwa na vikundi hivyo; kujenga uwezo wa vijana, maofisa vijana wa halmashauri na viongozi wa SACCOS za vijana kuhusu uanzishaji na usimamizi endelevu wa SACCOS; na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

#### 4.4.3.4.2 Programu ya Kukuza Ujuzi
Programu itaendelea kutekeleza malengo ya kukuza ujuzi na stadi za kazi katika viwanda, kilimo-biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA na madini hususan mafuta na gesi ili nchi ijitosheleze na nguvu kazi yenye ujuzi unaohitajika katika uchumi wa viwanda. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 15 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa kushirikiana na waajiri wa sekta binafsi kwa watu 18,600 wakiwemo watu wenye uelamavu 4,600 kupitia uanagenzi; kutoa mafunzo kwa vitendo baada ya kuhitimu kwa watu 4,000; kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi (RPL) kwa watu 7,500 na kutoa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi waliopo kazini kwa watu 5,000.

### 4.4.3.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

#### 4.4.3.5.1 Mradi wa Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma
Mradi unalenga kujenga kiwanja cha michezo katika mkoa wa Dodoma. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.82 fedha za ndani kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi.

#### 4.4.3.5.2 Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa TBC
Mradi unalenga kuimarisha Shirika la Utangazaji la Tanzania. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 3.0 kwa ajili ya ukarabati wa studio za redio na televisheni za Dodoma na Dar es Salaam; kununua vifaa vya utangazaji wa redio na

televisheni; na kununua vitendea kazi muhimu kwa ajili ya shughuli za utangazaji na ufundi.

#### 4.4.3.5.3 Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika

Programu inalenga kuboresha maeneo ambayo yalitumika katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuhifadhi na kukarabati miundombinu ya vituo viliyotumika katika ukombozi wa Bara la Afrika.

### 4.4.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

#### 4.4.4.1 Miundombinu

**A. Reli**

**(a) Miundombinu ya Reli ya Kati**

Lengo la mradi huu ni kuboresha njia ya reli ya kati kwa kujenga reli mpya pamoja na kukarabati reli reli iliyopo. Katika mwaka 2017/18 Mfuko wa reli umetengewa jumla ya Shilingi bilioni 218.569 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa reli kwa *standard gauge* pamoja ukarabati wa reli iliyopo.

**(b) Ukarabati wa Miundombinu ya Reli ya TAZARA**

Lengo la mradi ni kuboresha usafiri wa treni kwa njia ya TAZARA. Katika mwaka 2017/18 shilingi billioni 26.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Ukarabati na uimarishaji wa miundombinu ya njia kuu ya reli iliyopo; Kununua Traction Motor 90 kwa ajili ya injini 15 zitakazokarabatiwa; Matengenezo na ukarabati wa vichwa vya teni vilivyopo, mitambo, mabehewa ya mizigo na ya abiria; Ukarabati wa majengo ya karakana ya Dar es Salaam, mitambo, vifaa na mashine mbalimbali ikijumuisha karakana ya Mbeya, kiwanda cha kokoto na uzalishaji wa mataruma ya zege cha Kongolo; ukarabati wa mabehewa 21 ya kusafirisha abiria katika treni za mjini Dar es Salaam na treni ya Udzungwa inayo hudumia kati ya stesheni za Mlimba – Kidatu - Makambako; na kufanya upembuzi yakinifu wa kujenga mchepuko wa njia ya reli kati ya Mlowo na Magamba.

**(c) Ujenzi wa reli mpya ya Mtwara – Mbambabay**

Lengo la mradi ni kujenga njia ya reli kati ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kukamilisha usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge) na kumtafuta Transaction Advisor atakayekuwa na jukumu la kuunadi mradi na kutafuta fedha za ujenzi wa reli hiyo kwa njia ya PPP.

**(d) Tanga – Arusha – Musoma na Minjingu - Engaruka**

Mradi unalenga kuboresha na kujenga njia ya reli kati ya Tanga – Arusha na Arusha - Musoma kwa kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli kwa standard gauge kati ya Arusha – Musoma, pamoja na matawi yake kwenda Engaruka na Minjingu pamoja na kuweka uzio kwa ajili ya kulinda miundombinu ya reli ya zamani iliyopo kutoka Tanga – Moshi na Arusha kutokana na kukithiri kwa biashara ya vyuma chakavu.

**(e) Usafiri wa reli jijini Dar es Salaam**.

Lengo la mradi huu ni kuboresha usafiri wa abiria na kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kutumia usafiri wa treni ya abiria. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam, zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu kupitia uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Bagamoyo; kumpata *Transaction Advisor* na kuboresha miundombinu katika stesheni za Ubungo na Pugu.

**B. Barabara na Madaraja**

**a. Barabara zenye kufungua fursa za Kiuchumi**

**(i) Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211):** Mradi unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 8.465 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Lusitu – Mawengi yenye urefu wa km 50.

**(ii) Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 373):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 373) kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa mradi huu umegawanyika katika sehemu mbili; Tabora – Sikonge (Tabora – Usesula – km 30) na Sikonge (Usesula) –– Ipole – Koga – Mpanda (km 343). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 7.729 fedha za ndani na shilingi bilioni 69.273 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kuanza ujenzi wa barabara hii kwa sehemu ya Sikonge (Usesula) –– Ipole – Koga – Mpanda na kuendelea na ujenzi wa Sehemu ya Tabora – Sikonge (Usesula), km 30.

**(iii) Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa (km 528):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Mbeya hadi Makongolosi (km 115) pamoja na barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (Km 413) kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Mbeya – Lwanjilo (km 36); Lwanjilo-Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi

(km 43). Katika mwaka 2017/18, shilingi bilioni 22.038 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kulipa sehemu ya madai ya wakandarasi wa barabara ya Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya; na kuanza ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi na Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9).

**(iv) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35); Tabora – Nyahua (km 85); na Nyahua - Chaya (km 85). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 30.783 fedha za ndani na shilingi bilioni 15.081 zimetengwa kwa ajili ya: kuendelea na ujenzi wa sehemu za Tabora – Nyahua na kuanza ujenzi wa barabara ya Nyahua – Chaya.

**(v) Barabara ya Handeni - Kibereshi - Kibaya– Singida (km 460):** Katika 2017/18 imetengwa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Handeni - Kibereshi - Kijungu - Kibaya - Njoro - Olboloti - Mrijo Chini - Dalai - Bicha - Chambalo - Chemba - Kwa Mtoro – Singida.

**(vi) Barabara ya Dodoma – Babati (km 251.4):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati (km 261) kwa kiwango cha lami. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: Dodoma – Mayamaya (km 43.7), Mayamaya – Mela (km 99.4), Mela – Bonga (km 88.8) na Bonga – Babati (km 19.6) kwa upande wa barabara ya Dodoma - Babati. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 11.739 fedha za ndani na bilioni 104.985 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya makandarasi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya na Bonga – Babati, kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mayamaya – Mela na Mela – Bonga.

**(vii) Barabara ya Iringa – Dodoma (km 267.1):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa (km 260) pamoja na barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass) kwa kiwango cha lami. Mradi huu unagharamiwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni: Iringa – Migori (km 95.2); Migori – Fufu Escapment (km 93.8) na Fufu Escapment – Dodoma (km 70.9). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 4.784 fedha za ndani na shilingi bilioni 8.668 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu za madai ya Wakandarasi wa barabara ya Migori – Fufu Escarpment, Iringa-Migori na Fufu Escarpment – Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Iringa Bypass.

**(viii) Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo - Mto wa Mbu (km 338):** Mradi unalenga kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa kwa sehemu zifuatazo: sehemu ya Loliondo – Mto wa Mbu (km 213) na Makutano – Natta – Mugumu (km 125). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 17.397 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu ya Makutano – Natta (Sanzate) na kuanza ujenzi sehemu ya Natta – Mugumu na Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Loliondo (Waso) – Sale (km 50).

**(ix) Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (Km 353.7):** Mradi unalenga kujenga kwa kiwango cha lami barabara kati ya Kigoma na Tabora (km 443), ujenzi wa daraja la Mto Malagarasi na barabara za maingilio ya daraja (km 48). Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa barabara za Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Uvinza – Malagarasi (km 51.10), Urambo – Kaliua (km 33) na Kazilambwa – Chagu (km 40). Katika mwaka 2017/18, shilingi bilioni 27.858 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya: kulipa madai ya Makandarasi wa daraja la Mto Malagarasi, Tabora – Ndono, Kidahwe – Uvinza na Ndono – Urambo. Pia fedha zilizotengwa zitahusisha kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kaliua – Kazilambwa; na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Uvinza – Malagarasi na Urambo - Kaliua.

**(x) Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 464):** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 20.257 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu za Kidatu – Ifakara (km 68) na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396).

**b. Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(i) Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17) na Bulamba – Kisorya (km 51):** Mradi unalenga kukarabati barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 80), Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na ujenzi kwa kiwango cha lami ya mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17). Mradi huu unahusisha pia ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Nansio – Kisorya – Bunda (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51)), Nyamuswa – Bulamba (km 55), Musoma - Makojo - Busekela (km 92), barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Mwanza na barabara ya Makutano - Sirari (km 83).

Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 30.332 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Nyangunge – Simiyu/Mara Border; kuendelea na kazi za ujenzi katika barabara za Kisesa – Usagara (Mwanza bypass), Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba) na barabara za kupunguza

msongamano katika jiji la Mwanza (Upanuzi wa barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege wa Mwanza); kuanza ujenzi wa barabara za Nyamuswa – Bulamba, Musoma – Makojo – Busekela na kuendelea na ukarabati wa barbara ya Makutano – Sirari.

**(ii) Barabara ya Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 358):** Mradi ulilenga kujenga barabara ya Kidahwe – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 358) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 19.284 zilitengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidahwe – Kasulu (km 50) na Nyakanazi – Kibondo (km 50) pamoja na kukamilisha mapitio ya usanifu wa kina na kuanza maandalizi ya ujenzi sehemu ya Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 258).

**(iii) Barabara ya Marangu – Tarakea – Kamwanga/Bomang'ombe – Sanya Juu (Km 173):** Mradi unalenga kujenga na kukarabati kwa kiwango cha lami barabara za Marangu – Rombo Mkuu ikihusisha Mwika – Kilacha (km 32), Rombo – Mkuu – Tarakea (km 32), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanyajuu – Alerai), Arusha – Moshi – Holili (km 56.5), KIA - Mererani (km 26), Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16.0) na Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8), Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 105) na Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST – km 14).

Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 18.933 fedha za ndani na bilioni 15.00 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipia sehemu ya malipo ya mwisho ya Makandarasi wa barabara za Rombo Mkuu – Tarakea, Marangu – Rombo Mkuu na Mwika – Kilacha; kuanza ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama - Machame Junction (Masama - Machame Junction), Sanya Juu – Kamwanga, Kiborloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia na kuendelea na ujenzi wa njia nne kutoka njia mbili za sasa za barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Arusha (Sakina) – Tengeru (km 14.10), njia mbili kwa sehemu ya Arusha Bypass (km 42.41), Kijenge - Usa River (Nelson Mandela AIST) na barabara ya KIA – Mererani; na kuanza ukarabati wa njia mbili za kuwa nne kwenye barabara ya Arusha – Moshi – Holili/Taveta – Voi sehemu ya Tengeru - Moshi - Himo pamoja na Mizani wa Himo.

**(iv) Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo (km 92) na Nyakasanza – Kobero (km 60):** Mradi unalenga kukarabati barabara za Isaka – Lusahunga, Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero kwa kiwango cha lami. Mradi huu umegawanyika katika sehemu nne ili kuharakisha utekelezaji: Isaka – Ushirombo (km 132), Ushirombo – Lusahunga (km 110), Lusahunga - Rusumo (km 92) na Nyakasanza -Kobero (km 60). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 18.76 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa malipo ya mwisho ya madai ya Mkandarasi wa sehemu ya Isaka – Ushirombo (km 132) pamoja na kuendelea na

ukarabati wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga; maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero na maandalizi ya ujenzi wa mizani ya kupima magari huku yakitembea (Weigh in Motion Scale) sehemu ya Mwendakulima (Kahama).

**(v) Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112):** Mradi unalenga kujenga barabara ya hii pamoja na barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 20.957 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kassanga Port na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya.

**(vi) Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 346.6):** Mradi unalenga kujenga barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Kidahwe (km 438) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 31.0 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya mkandarasi wa barabara ya Kizi – Sitalike – Mpanda (km 95); sehemu ya Sitalike – Mpanda (km 36); kuendelea na kazi za ujenzi sehemu za Sumbawanga – Kanazi (Km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Mpanda – Mishamo (km 100); sehemu ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 30) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Kibaoni – Sitalike (km 71).

**(vii) Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171.8):** Mradi unalenga kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 25.188 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya malipo ya mwisho ya mkandarasi wa barabara ya Bariadi – Lamadi (km 71.8), kuendelea na ujenzi sehemu ya Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7).

### c. Barabara za Mikoa

Mradi unalenga kukarabati na kuboresha barabara zinazounganisha mikoa nchini. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 30 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa km 469.5 kwa kiwango cha changarawe, kujenga km 58.4 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja 12.

### d. Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini (km 156.7)

Mradi unalenga kujenga, kupanua na kukarabati barabara za jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 12.409 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kugharimia barabara hizo kama ifuatavyo:-

(i) Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley –Jangwani/Twiga Jct (km 2.7), kulipa madai ya mkandarasi;

(ii) Tabata Dampo – Kigogo na Ubungo Maziwa – External (km 2.25), kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi;

(iii) Kimara – Kilungule – External/Mandela Road (km 9), kulipa madai ya mkandarasi na kuendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki;
(iv) Mbezi (Morogoro Road) –Malamba Mawili – Kinyerezi – Banana (km 14), kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Mbezi (Morogoro Road) –Malamba Mawili – Kifuru (km 10.8);
(v) Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi Mwisho (km 20), kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Goba – Tegeta (km 13);
(vi) Tangi Bovu – Goba (km 9), kulipa madai ya mkandarasi;
(vii) Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), kuendelea na ujenzi;
(viii) Kibamba – Kisopwa (km 12.0), kulipa madai ya Mkandarasi wa sehemu ya Kibamba-Mlonganzila (km 4) na kuendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki;
(ix) Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7), kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara sehemu ya Kitunda – Moshi Bar (km 3.2);
(x) Ardhi – Makongo, kuendelea na ujenzi;
(xi) Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5), kuendelea na ujenzi;
(xii) New Bagamoyo (Kawawa Junction – Mwenge-Tegeta: km 17), kuanza ujenzi wa sehemu ya Kawawa Junction – Mwenge (km 4.2) na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua;
(xiii) Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1); na
(xiv) Mwai Kibaki (Old Bagamoyo), kuanza upanuzi wa barabara hiyo.

**e. Ujenzi wa Barabara za Juu**

Mradi unalenga kujenga 'Flyover' ya TAZARA ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 46.89 zimetengwa kwa ajili ya: kujenga barabara za juu (Flyover) kwenye makutano ya barabara za Mandela na Nyerere (TAZARA); kujenga 'Interchange' ya Ubungo kwenye makutano ya barabara za Morogoro na Mandela/Sam Nujoma; kujenga kwa utaratibu wa Usanifu na Kujenga (Design and Build) barabara za juu na kuboresha makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya TAZARA – JNIA kuwa njia 6.

**(i) Flyover ya TAZARA:** Mradi unahusisha ujenzi wa 'flyover' katika makutano ya barabara za Mandela na Nyerere ili kukabiliana na msongamano wa magari. Mradi unatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa fedha za Serikali pamoja na fedha za msaada kutoka Serikali ya Japan. Mkataba wa ujenzi wenye thamani shilingi bilioni 87.156 **ulisainiwa** Oktoba, 2015 baina ya Serikali na mkandarasi kampuni ya M/s Sumitomo Mitsui Construction Co. Ltd ya Japan na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi 35. Usimamizi wa mradi utafanywa na kampuni za M/s Oriental Consultants Co. Ltd na Eight – Japan Engineering Consultants Inc zote za Japan; mkataba wa usimamizi wa mradi ulisainiwa Oktoba, 2013 na una thamani ya shilingi

bilioni 6.28. Katika mwaka 2017/18, shilingi bilioni 0.56 fedha za ndani na bilioni 25.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Flyover ya TAZARA.

**(ii) Interchange ya Ubungo:** Mradi unahusisha ujenzi wa barabara za juu (interchange) katika makutano ya barabara za Morogoro na Mandela eneo la ubungo ili kukabiliana na msongamano wa magari. Mradi unatekelezwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa fedha za Serikali pamoja na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 0.32 fedha za ndani na shilingi bilioni 20 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**(iii) Maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela na Kawawa/Morocco:** Mradi unahusisha maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni/Nyerere, Mwenge, Tabata/Mandela na Kawawa/Morroco kwa utaratibu wa usanifu na kujenga (design and Build). Mradi unalenga kuimarisha uchukuzi Dar-es-Salaam na kupunguza msongamano wa magari. Ujenzi wa flyovers kwa awamu unatarajia kuanza baada ya kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi (upembuzi yakinifu na usanifu wa kina) na kupatikana kwa fedha za ujenzi. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 1 zimetengwa kwa ajili ya maboresho ya makutano ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco.

**f. Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200) Sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144)**

Mradi unalenga kujenga barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 144) kwa kwango cha "Expressway". Mradi huu unahusisha ukarabati wa sehemu ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24) na ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6). Mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi - Public Private Partinership (PPP). Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 12.771 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mshauri Mwelekezi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze; kulipa fidia kwa waathirika wa mradi; kuendelea na ukarabati wa barabara ya Mlandizi – Chalinze; na kuanza ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere.

**g. Madaraja Makubwa**

**(i) Ujenzi wa Madaraja Makubwa:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 36.30 zimetengwa kwa ajili ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa madaraja mbalimbali nchini. Madaraja hayo ni: Daraja la Kirumi (Mara), Daraja la Sibiti (Singida) kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, Daraja la Kilombero (Morogoro) kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge, Daraja la Kavuu (Katavi) kwenye barabara

ya Majimoto – Inyonga, Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Momba kwenye barabara ya Sitalike – Kilyamatundu/Kamsamba – Mlowo (Rukwa/Songwe Border), Daraja la Simiyu (Mwanza) kwenye barabara Mwanza – Musoma, Daraja Jipya la Wami (Pwani) barabara ya Chalinze – Segera, Daraja Jipya la Selander (Dar es Salaam), Daraja la Mlalakuwa (Dar es Salaam), Daraja la Sukuma (Mwanza), Daraja la Kigongo/Busisi (Mwanza), Daraja la Mara (Mara), Daraja la Bwawa la Mtera (Dodoma/Iringa) na Daraja la Magara (Manyara).

**(ii) Daraja la Mwalimu Nyerere – Kigamboni:** Mradi unalenga kujenga daraja la Mwalimu Nyerere - Kigamboni pamoja na barabara za maingilio ya daraja (approach roads) kwa ajili ya kuunganisha eneo la Vijibweni (kwa upande wa Kigamboni) na Kurasini katika bahari ya Hindi. Barabara za maingilio ya daraja ni pamoja na Mjimwema – Vijibweni (km 10), Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mjimwema (km 1.6). Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 2.23 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara unganishi.

**h. Miundombinu ya Mabasi yaendayo Haraka - BRT**

Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi milioni 100 fedha za ndani na bilioni 25.00 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwa awamu ya II, III na IV ambapo utahusisha barabara zifuatazo: **Awamu ya II ya BRT** itahusisha barabara za Kilwa, Sehemu ya barabara ya Kawawa kutoka Magomeni hadi Chang'ombe na Barabara ya Chang'ombe zenye urefu wa km 20.3. Awamu hii itahusisha ujenzi wa Barabara za juu (flyovers) katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu. Awamu ya III ya BRT itahusisha barabara za Nyerere, Azikiwe, Bibi Titi, Uhuru kutoka katikati ya jiji hadi Gongo la Mboto (km 23.6). Awamu ya IV itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Sam Nujoma, na barabara ya Bagamoyo kutoka katikati ya Jiji hadi Tegeta.

**C. Usafiri wa Majini**

**Ununuzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu:** Mradi unalenga kuboresha usafiri wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu kwa kuendelea kukarabati na kununua meli mpya katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 24.49 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa meli moja mpya katika ziwa Victoria na pia kukarabati meli za M.V. Victoria, Liemba,Umoja, Serengeti na Butiama katika ziwa Victoria na Tanganyika.

**D. Bandari**

**(i) Bandari ya Dar es Salaam**

(a) **Gati 1 – 7 na Gati 12 – 14:** Katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na uwezo mdogo wa bandari kuhudumia shehena, kwa mwaka 2017/18 shilingi bilioni 187.12 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi

na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam kwa kuimarisha na kuongeza kina cha gati Na. 1 – 7; kujenga gati jipya la RoRo; kufanya utafiti wa kuhamisha gati la mafuta lililopo Kurasini (KOJ) ili kupisha ujenzi wa gati Na. 12 - 14; kujenga bandari kavu eneo la Ruvu; kujenga gati jipya la kisasa la kushusia mafuta aina zote na kuboresha mifumo ya kazi ya TPA kutoka katika mifumo ya kawaida na kuingia katika mifumo ya kielektroniki.

**(b) Kuongeza Kina na kupanua lango la kuingilia meli:** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 96.25 zimetengwa kwa ajili ya kupanua, kuchimba na kuongeza kina cha lango la kuingilia na kutokea meli pamoja na eneo la kugeuzia meli.

**(ii) Ujenzi wa Bandari Kavu Ruvu – Pwani:** Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 1.7 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari kavu katika eneo la Ruvu.

**(iii) Gati la Nyamisati:** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 3.0 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha gati la Nyamisati Rufiji katika mwambao wa Bahari ya Hindi.

**(iv) Bandari ya Tanga:** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya mapitio ya upembuzi yakinifu na kupendekeza namna bora ya kutekeleza mradi wa kujenga bandari ya Mwambani kwa njia ya ubia na sekta binafsi (PPP).

(v) **Bandari ya Mtwara:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 87.04 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko (Multi – Purpose Terminal); uboreshaji wa mfumo wa usalama; kuboresha maegesho ya meli; kujenga gati la mafuta shangani na kukarabati eneo la gati namba 3 ili kuongeza eneo la kufanyia kazi na kuhifadhi mizigo. Fedha hizo pia zitatumika kujenga gati katika bandari ya Lindi na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga magati ya Kilwa na Rushungi.

**(vi) Bandari ya Bagamoyo:** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 43.0 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha maandalizi na kuanza ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo kwa kushirikisha wabia pamoja na Sekta Binafsi.

**(vii) Bandari za Maziwa Makuu**

**(a) Ziwa Victoria:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 6.29 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya bandari za ziwa Viktoria. Kazi hizi ni pamoja na: uboreshaji wa mfumo wa usalama; ujenzi wa ofisi na jengo la abiria bandari ya Bukoba na Kyamkwikwi; ukarabati wa miundombinu iliyopo Mwanza *South*; kujenga bandari kubwa na ndogo za Nyamirembe, Chato na Magarine. Vile vile mradi huu utajumuisha ujenzi wa 'Dhow Wharves' ya Mwigobero; uongezaji wa kina katika bandari ya Nansio na Mwanza South; kuboresha sehemu ya kushukia

abiria Mwanza North na ukarabati wa *Link Span* ya bandari ya Mwanza South.

**(b) Ziwa Tanganyika:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 18.50 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha bandari ya Kigoma na kukamilisha upembuzi yakinifu wa namna ya kuboresha bandari ya Karema katika Ziwa Tanganyika. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: uboreshaji wa mfumo wa usalama na maegesho ya meli (gati) na kuhudumia abiria pamoja na mizigo katika vijiji vya Lagosa, Sibwesa, Kabwe na Ujiji; upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya Karema; kujenga ofisi na kuboresha miundombinu ya bandari ya Kasanga pamoja na barabara ya kuelekea katika bandari ya Kipili.

**(c) Ziwa Nyasa:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 15.29 zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa namna ya kuboresha bandari za Mbambabay na Lipuli katika Ziwa Nyasa. Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na:uboreshaji wa mfumo wa usalama; kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa gati za Mbamba Bay, Manda na Matema; Ujenzi wa gati la Ndumbi na ujenzi wa sakafu (pavement) katika bandari ya Kiwira na kuboresha sehemu ya kushukia abiria.

## E. Usafiri wa Anga

**(i) Ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa Julius Nyerere:** Katika mwaka 2017/8 shilingi bilioni 35 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake.

**(ii) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro:** Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 5 za fedha za ndani na bilioni 27.56 fedha za nje kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Uholanzi (ORIO). Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesgo ya ndege, barabara za viungio, jengo la abiria, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege, na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka.

**(iii) Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato:** Lengo la Mradi huu ni ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha kimataifa katika eneo la Msalato, Dodoma. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 2 fedha za nje kutoka benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja.

**(iv) Kiwanja cha Ndege Mwanza:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 18.58 fedha za ndani na shilingi bilioni 5 fedha za nje kutoka Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika (BADEA) zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria na kuendelea na kazi za kurefusha na kujenga barabara ya kuruka na

kutua ndege (runway), ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo terminal), maegesho ya ndege na viungio vyake,mnara wakuongoza ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

(v) **Kiwanja cha Ndege Kigoma:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 1.05 fedha za ndani na shilingi bilioni 6.20 fedha za fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, kujenga uzio, na ujenzi wa jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

(vi) **Kiwanja cha Ndege Tabora:** Katika mwaka 2017/18, shilingi bilioni 2.45 fedha za ndani na shilingi bilioni 8.60 fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka), ukarabati wa njia ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

(vii) **Kiwanja cha Ndege Mtwara:** Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 4.55 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu na Mpango Kabambe (Concept Design & Master Plan) na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Fedha hizi pia zitatumika kulipia madai ya wahandisi washauri pamoja naujenzi wa barabara mchepuo inayoingia kiwanja cha ndege.

(viii) **Kiwanja cha Ndege Sumbawanga:** Mradi unalenga ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga ili kuboresha huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka 201/18 shilingi bilioni 5.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 13.20 fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

(ix) **Kiwanja cha Ndege Shinyanga:** Mradi unalenga ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga ili kuboresha huduma za usafiri wa anga. Katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 13.80 fedha za nje kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa , barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.Kati ya fedha hizo za ndani, shilingi milioni 600 zitatumika kulipa fidia na shilingi bilioni 1.2

ni mchango wa Serikali katika mradi.

**(x) Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa:** Katika mwak 2017/18, mradi huu umetengewa jumla ya shilingi bilioni 17.39 fedha za ndani. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15.27 zitatumika kugharamia ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma na Mara. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 1 kimetengwa kwa ajili ya kugharamia maandalizi ya ujenzi wa viwanja vya ndege nane (8) ambavyo ni Lake Manyara, Moshi, Tanga, Kilwa Masoko, Lindi, Njombe, Singida na Simiyu. Vile vile kiasi cha shilingi bilioni 1.12 kitatumika kukarabati uwanja wa ndege wa Dodoma.

## F. Teknolojia ya habari na Mawasiliano

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano:** Mradi unalenga kuunganisha mikoa na wilaya zote nchini pamoja na nchi za jirani katika mkongo wa Taifa ili kuboresha upatikanaji wa huduma za uhakika za mawasiliano na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya: utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi makao makuu ya Wilaya zote nchini (Awamu ya III-V); ujenzi wa muundombinu wa mawasiliano ya mitandao "Public Key Infrastructure - (PKI)"; ujenzi wa vituo vya kuhifadhi taarifa vya Dodoma na Zanzibar; kuratibu matumizi ya huduma za TEHAMA nchini; kufanya tathimini ya kimazingira sehemu zipitazo mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao; na kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi.

**(b) Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi:** Mradi unalenga kuanzisha utaratibu wa kutumia anuani za makazi na simbo za posta katika kutambua maeneo yote ya mitaa. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 3 kwa ajili ya: kuweka muundombinu katika miji mikuu ya mikoa ya Dodoma, Morogoro, Lindi, Mbeya, Dodoma, Kagera, Mwanza, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Unguja Kusini na Geita; kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa barabara/mitaa zinakuwa na majina yaliyorasimishwa; kudhibiti ujenzi holela ama mipango-miji dhaifu; na kuwa na takwimu ya idadi ya nyumba/majengo na mitaa/barabara katika kila kata; kushirikisha wadau hususan sekta binafsi katika utekelezaji wa mpango; Kutoa elimu kwa watendaji na kuhamasisha utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi; kutoa elimu kwa wananchi na kuhamasisha kuhusu faida na matumizi ya mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi na utunzaji wa muundombinu uliowekwa; kusambaza na kutoa elimu ya Mwongozo wa Anwani za makazi, Mwongozo wa Postikodi na Sheria Ndogo ya Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi; na kufuatilia na kutathmini matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi.

**(c) Mradi wa ujenzi wa Kituo cha vifaa vya TEHAMA:** Katika mwaka 2017/18, mradi umetengewa kiasi cha Shilingi milioni 800 kwa ajili ya: upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kituo cha kutengeneza vifaa vya TEHAMA kutokana na TEHAMA zinazofikia mwisho wa matumizi; maboresho ya kituo cha kutengeneza programu za TEHAMA; ununuzi wa samani za kituo; kulipia gharama za mtandao wa *Internet* wa ukubwa wa 10/10 Mbps; kulipa gharama za eneo katika *National Internet Data Centre*; kulipia gharama za kununulia mitambo ya TEHAMA; mafunzo kwa wataalam wa mitambo na uendeshaji wa kituo; na kulipia gharama za jengo la kituo kwa mwaka.

**G. Nishati**

**(a) Miradi ya Uzalishaji wa Umeme**

**(i) Kuongeza Uwezo wa Uzalishaji Umeme wa Mitambo ya Kinyerezi I (MW 185):** Mradi unalenga upanuzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I kwa kuongeza mitambo itakayozalisha MW 185 zaidi ya kiwango cha umeme sasa cha MW 150. Mradi unagharimiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 60 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: kuendelea na ujenzi wa msingi katika eneo itakapowekwa mitambo; na kuagiza vifaa vitakavyotumika katika ujenzi na kusimika mitambo.

**(ii) Kinyerezi II – MW 240**: Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 10 fedha za nje zilitengwa kwa ajili ya: kukamilisha utengenezaji wa mitambo; kuendelea na ufungaji wa mitambo; na kukamilisha mtambo wa kwanza wa kuzalisha umeme wa MW 30 ifikapo Desemba 2017. Mradi mzima unatarajiwa kukamilika Desemba 2018.

**(iii) Mto Malagarasi MW 45:** Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 2.8 zimetengwa kwa ajili ya kuanza kugharamia utekelezaji wa mradi.

**(iv) Kakono MW 87:** Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 2.05 fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi.

**(v) Rusumo MW 80:** Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 2.8 fedha za nje kimtengwa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi.

**(vi) Mradi wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira (MW 200) – Mbeya: :** Mradi unatarajiwa kutekelezwa na STAMICO chini ya utaratibu wa PPP ukilenga kupanua mgodi wa chini ya ardhi kutoka uwezo wa kuzalisha tani 150,000 hadi tani 300,000 kwa mwaka; kuanzisha

mgodi wa wazi wenye uwezo wa kuzalisha tani 1,200,000 kwa mwaka; kujenga mtambo wa kufua umeme (coal fired power plant) wenye uwezo wa kuzalisha MW 200; na kujenga njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kV 400 kutoka Kiwira hadi Mbeya (km 100). Makadirio ya gharama za utekelezaji wa mradi ni Dola za Marekani milioni 498 na utatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia STAMICO na wawekezaji wa sekta binafsi. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 10 fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya mgodi wa chini ya ardhi na kuhuisha taarifa za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi; kufufua mitambo ya uzalishaji wa MW 6 kama maandalizi ya kutekeleza mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa MW 200; na kuthamini mali zilizopo katika maeneo yatakayopitiwa na mradi.

(vii) **Uendelezaji wa Nishati ya Joto Ardhi (Geothermal) – (MW 100)- Mbeya:** Mradi huu unahusu utumiaji wa joto ardhi kwenye mlima wa Volcano wa Ngozi Mkoani Mbeya kwa ajili ya kuzalisha umeme wa MW 100. Mradi unatekelezwa na Serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (Tanzania Geothermal Development Company Limited - TGDC) kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB/CIF) na Kamisheni ya Afrika. Katika Mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 20.29 fedha za ndani na bilioni 7.70 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya awali ya kuchoronga visima vitatu (3) katika eneo la Ziwa Ngozi (Mbeya) ili kutathmini kiwango cha nishati iliyopo na uwezo wake wa kuzalisha umeme.

**(b) Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

(i) **Mradi wa Umeme wa Msongo kV 220, Makambako – Songea**: Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea, yenye urefu wa kilometa 250; ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupozea umeme; ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa kV 33 zenye urefu wa kilometa 900; na ufungaji wa transfoma 250. Jumla ya wateja wa awali 22,700 wataunganishiwa umeme katika vijiji 250. Mradi unalenga kuunganisha Mikoa ya Ruvuma na Njombe kwenye Gridi ya Taifa. Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA). Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 3 fedha za ndani na bilioni 8 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuendelea na ujenzi wa njia kubwa ya kusafirisha umeme.

(ii) **Mradi wa msongo wa kV 400, North - West:** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 wenye urefu wa

km 1,148 utakaounganisha mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma kwenye gridi ya Taifa. Mradi unatekelezwa kwa awamu tatu: Awamu ya kwanza Mbeya – Sumbawanga (km 340); Awamu ya pili Nyakanazi – Kigoma – Mpanda (km 568); na awamu ya tatu Mpanda – Sumbawanga (km 240). Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 12.3 fedha zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha utaratibu wa upatikanaji wa fedha za kutekeleza sehemu ya mradi kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kwa ufadhili wa EDCF ya Korea Kusini; kukamilisha utafiti wa athari za mazingira kutoka Mpanda hadi Sumbawanga; na kulipa fidia wananchi kwa maeneo ya Nyakanazi hadi Kigoma. Na Kwa sehemu ya Geita hadi Nyakanazi (km 133) shilingi bilioni 7.5za ndani na 1.6 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia na kuaza utekelezaji wa mradi.

(iii) **Mradi wa Msongo wa kV 400, North - East Grid (Dar – Tanga – Arusha)**: Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Dar es Salaam hadi Arusha kupitia Chalinze na Tanga (km 702) pamoja na kujenga vituo vikuu vya kupozea umeme wa msongo wa kV 400/220/33. Mradi unalenga kusafirisha umeme utakaozalishwa eneo la Kinyerezi – Dar es Salaam na kuunganisha na Gridi ya Taifa ili kuboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 19.80 fedha za ndani kwa ajili ya kulipa fidia kwa awamu ya kwanza kwa wananchi watakaopisha mradi kutoka Kinyerezi hadi Chalinze pamoja na mchango wa sehemu ya asilimia 15 ya gharama za mradi.

(iv) **Mradi wa msongo wa kV 220 wa North – West Kutoka Geita – Nyakanazi:** Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 na urefu wa kilometa 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi; ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Geita; na usambazaji wa umeme kwenye vijiji vinavyopitiwa na mradi. Mradi unalenga kuunganisha maeneo ya Magharibi na Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania katika Gridi ya Taifa. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 24.2 fedha za ndani na bilioni 15.4 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kupata mkandarasi na kuanza ujenzi wa mradi.

(v) **Mradi wa msongo wa KV 220 Bulyanhulu – Geita:** Mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilometa 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Bulyanhulu; na usambazaji umeme katika vijiji 10 vilivyopo ndani ya eneo la mradi katika wilaya ya Geita. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Uarabuni (BADEA), *Opec Fund for International Develepment* (OFID) pamoja na Serikali. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 7.0 fedha

za ndani na bilioni 1.0 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na kuanza utekelezaji wa mradi.

**(vi) Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini na Makao Makuu ya Wilaya:** Mradi unasimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na unatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za kusambaza umeme za msongo wa kV 11 na kV 33 zenye urefu wa km 25,000; njia za usambazaji umeme za msongo wa Volti 400 na Volti 230 zenye urefu wa km 38,000; na ufungaji wa vipoza umeme 13,000. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2016/17 na utakapokamilika wateja 340,000 wataunganishiwa umeme. Awamu ya Tatu (REA Phase III) itatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 katika vijiji 7,873 vya wilaya zote za Tanzania Bara. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 469.36 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa njia ya msongo wa kati 33 kV yenye urefu wa km 31,828; ujenzi wa njia za msongo mdogo 0.4 kV yenye urefu wa km 100,421; kufunga transfoma 17,735; na kuunganisha wateja 977,043.

**(vii) Miradi ya Kujenga Miundombinu ya Usambazaji Gesi Asilia (CNG & Piped Natural Gas Distribution Networks) katika Mikoa ya Lindi na Mtwara:** Mradi unahusisha ujenzi wa mtandao wa kusambaza gesi asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa watumiaji wa majumbani, taasisi mbalimbali na viwandani. Mabomba hayo yataunganishwa katika matoleo ya bomba kubwa la kusafirishia gesi asilia kutoka Mnazi Bay (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) hadi Dar es Salaam. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 2 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kijamii na kimazingira, kukamilisha usanifu wa kina wa kihandisi; na kuandaa zabuni ya kumpata mwekezaji.

**(c) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi Kutoka Uganda**

Mradi wa Ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Bandari ya Tanga (Tanzania) ni mojawapo ya miradi mikubwa itakayoendelea kutekelezwa. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 50 kwa ajili ya: kufanya tathmini ya mali na kulipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi; na kuwezesha ushiriki wa Tanzania katika mradi huo.

#### 4.4.4.2 Ardhi

**(a) Programu ya Umilikishaji wa Ardhi**

Programu hii inalenga kumilikisha vipande vya ardhi ili kupunguza migogoro inayotokana na ardhi. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani na bilioni 9.0 fedha za nje kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha vipande 80,000 vya ardhi na kuwapatia Hati za Hakimiliki za Kimila (CCRO's) katika

wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi; kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 40, na kuwezesha utekelezaji wa Programu hii ya mfano katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.

**(b) Programu ya Kupanga na Kupima Ardhi**

Programu hii inalenga kuainisha matumizi sahihi ya ardhi kupunguza migogoro inayotokana na ardhi. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 8.0 fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha Mfuko wa Fidia; kutoa Hati za Kumiliki Ardhi 400,000; kutoa Hatimiliki za Kimila 500,000; na kupima mipaka ya vijiji 500 na kuviandalia mipango ya matumizi ya ardhi na kuimarisha Mfuko wa Fidia wa Ardhi.

**(c) Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Mradi unalenga kuimarisha mipaka sita (6) ya Tanzania na nchi za jirani. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 4.0 kwa ajili ya kuimarisha mipaka 6 ya kimataifa ili kutimiza azimio lililotolewa na Umoja wa Afrika lililozitaka nchi zote za Afrika kuimarisha mipaka yake.

**(d) Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Ardhi kwa Sekta Binafsi**

Katika mwaka 2017/18 zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kama mchango wa Serikali (counter part fund) kwa ajili ya kuratibu ujenzi wa mfumo unganishi wa kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za ardhi; kuimarisha utoaji wa huduma za vituo vyote vya *Continous Operating Reference Station (CORS)*; kuendelea na urasimishaji wa mali kwa kutoa hati miliki katika miji ya Mwanza na Dar es Salaam; na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.

#### 4.4.4.3 Huduma za Fedha, Utalii, Biashara na Masoko

**(a) Huduma za fedha**

**(i) Benki ya Rasilimali Tanzania:**

Katika mwaka 2017/18, Benki ya Rasilimali Tanzania itaendelea kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wawekezaji katika sekta ya viwanda vinavyotumia rasilimali za ndani; miundombinu; Kilimo; kuongeza dhamani kwenye madini; kuwezesha sekta za utoaji wa huduma hususan afya, elimu, upimaji viwanja; ujenzi wa hoteli na nyumba. Aidha, Benki ya Rasilimali Tanzania inatarajia kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 198.94; kukusanya riba ya shilingi bilioni 24.76; kuongeza amana (assets) kufika 842.93; na kukusanya mapato yasiyotokana na riba ya shilingi bilioni 14.26.

**(ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

Malengo ya Benki ni kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula nchini na

kubadilisha dhana ya kilimo kutoka katika kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha biashara kwa kuwawezesha wananchi katika sekta ya kilimo. Katika mwaka 2017/18 Benki ya Maendeleo ya Kilimo imepanga: kushirikiana kwa karibu na Tanzania Merchantile Exchange katika kuhakikisha wakulima wanaunganishwa na masoko ya uhakika; kuanzisha ofisi za kanda ili kuwezesha kutoa mikopo nchi nzima na kuwa na usimamizi wa karibu; kushirikiana na MIVARF kuwezesha taasisi mbalimbali za fedha kutoa mikopo katika sekta ya kilimo; na kuendelea kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima wadogo nchi nzima kwa awamu.

**(iii) Benki ya Wanawake Tanzania**

Katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia Benki ya Wanawake Tanzania, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za Benki ya Wanawake Tanzania katika matawi, vituo vya kutolea mafunzo na mikopo, na kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wanawake katika mikoa ambayo ina huduma za benki. Aidha, Serikali kupitia Benki ya Wanawake Tanzania itafungua vituo vya kutolea mafunzo na mikopo katika mikoa ambayo haina huduma za kibenki.

**(b) Utalii**

**(i) Utalii House Phase II**

Mradi huu unahusu ujenzi wa kitega uchumi katika eneo lililokuwa Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam. Kutokana na makubaliano kati ya Serikali za Tanzania na Marekani, kila nchi itachangia nusu ya gharama, hivyo Serikali ya Marekani ilijenga Utalii House Awamu ya I ambao kwa sasa jengo hilo linatumika. Hivyo, Serikali ya Tanzania inawajibika kujenga Utalii House Awamu ya pili, shughuli zifuatazo: kuitisha zabuni za uchoraji na kumtafuta mkandarasi.

**(ii) Mradi wa Ujenzi wa "Theme Park" katika jiji la Dares Salaam**

Mradi huu utatoa fursa kwa Sekta ya Utalii kuwa na eneo la kitalii ambalo litakuwa na huduma bora kama vile sehemu ya mapumziko/starehe na burudani sehemu ya kumbukumbu ya historia mbalimbali, hoteli zenye hadhi ya nyota za daraja la juu, migahawa ya kisasa, maduka (shoping centres), bustani ya wanyama (zoo), michezo ya golf, pamoja na shughuli mbalimbali za kitalii (climbing walls, skycoaster or tower swing, ches playing area) zitafanyika katika eneo hilo. Aidha mradi huu umekadiriwa kutumia eneo lenye ukubwa wa hekta 10,000 karibu na mwambao wa bahari ya Hindi katika jiji la Dar es Salaam.

**(c) Biashara na Masoko**

**(i) Biashara**

Mradi unalenga kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (bilateral), Kikanda (regional) na Kimataifa (multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji; kukamilisha mapendekezo ya uandikaji wa sheria ya anti dumping and countervailing measures; na kuratibu zoezi la kuridhiwa kwa mkataba wa shirika la biashara duniani (WTO) wa urahisishaji wa biashara (trade facilitation agreement).

**(ii) Uendelezaji wa Shughuli za Masoko**

Mradi unalenga ujenzi wa masoko, mazingira pamoja na vitendea kazi vya masokoni ambapo katika mwaka 2017/18 shilingi bilioni 6.35 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya TBS; Kuboresha Miundombinu ya Uwanja wa Maonesho- DTIF; COSOTA-kuboresha mfumo wa usajili wa kazi na wanachama wanaojishughulisha na kazi za ubunifu kwa njia ya mtandao; na ununuzi – vifaa vya kuhakiki upimaji (i.e. Water Meter Test Bench, Electricity Meter Test Bench, special verification truck, Speed Detector Standard, Gas Meter equipment Standard). Aidha, mradi unalenga kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za maghala; kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mazao; kuimarisha biashara na masoko ya mipakani; kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania; kuimarisha na kuboresha mfumo wa ukuasanyaji wa taarifa za masoko; na kuandaa na kupitia sera, sheria na kanuni mbalimbali katika masoko.

### 4.4.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango

#### 4.4.5.1 Utawala Bora, Utoaji Haki na Huduma za Kisheria

**(a) Makao Makuu Dodoma**

Serikali itaendelea na azma yake ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu kwenda Dodoma. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 200 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Serikali mjini Dodoma. Kikosi kazi cha kitaifa kilichoundwa kuratibu zoezi la kuhamia Dodoma kitaendelea na mazungumzo na baadhi ya makampuni kutoka Switzerland, China na Zimbabwe ambayo yameonesha nia ya kuwekeza pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya mji wa Dodoma.

**(b) Mradi wa Mfuko wa Mahakama**

Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya mahakama na nyumba za majaji

nchini. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 17 fedha za ndani na bilioni 1.12 fedha za nje kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mahakama kuu, mahakama za mwanzo, nyumba za majaji, mahakama ya rufaa, mahakama za wilaya, kuimarisha programu ya kupambana na rushwa na kuboresha hduma za utoaji haki na sheria kwa wananchi.

**(c) Mradi wa Telejustice (E–Justice)**
Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kukamilisha taarifa ya upembuzi yakinifu na kuanza utekelezaji awamu ya kwanza ya mradi katika mkoa wa Dar es Salaam.

**(d) Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa**
Mradi unalenga kuhakikisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya utambuzi, usajili wa watu pamoja na uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi (raia), wageni wakaazi pamoja na wakimbizi waishio nchini kihalali.

**(e) Taasisi ya Uongozi**
Taasisi inalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani kwa ajili ya: kutekeleza Programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali wa kufanya majadiliano ya mikataba yenye thamani kubwa na namna ya kuunda timu madhubuti za majadiliano kupitia mafunzo mbalimbali ikiwemo mafunzo ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi".

**(f) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa**
Mradi unalenga kuimarisha huduma za uhamiaji mikoani. Katika mwaka 2017/18, zimetengwa Shilingi bilioni 4.0 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ofisi za uhamiaji za mikoa katika mikoa ya Geita, Lindi, Manyara na Mtwara.

**(g) Mradi wa Mfuko wa Bunge**
Mradi unalenga kuboresha miundombinu ya ofisi za Bunge Dodoma na Dar es Salaam, na ofisi za Wabunge Majimboni. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 7 fedha za ndani na milioni 200 fedha za nje kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu, jengo la Bunge Dodoma, na ofisi za Bunge Dar es Salaam.

**(h) Kuunganisha mtandao wa Polisi na Mkongo wa Taifa**
Mradi unalenga kuboresha mazingira ya utoaji huduma ya Jeshi la polisi kwa kuunganisha mtandao wa Polisi na Mkongo wa Taifa. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi milioni 237.5 fedha za ndani kwa ajili ya kuunganisha

mikoa 8 (Tanga, Mbeya, Mjini Magharibi, Chakechake, Pwani, Mtwara, Morogoro and Ruvuma) na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

**(i) Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi**

Eneo hili linahusisha uratibu wa fursa za mikopo kwa ajili ya mitaji ili kuhakikisha inapatikana bila urasimu, kwa masharti nafuu na kuwafikia wananchi kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji/shehia. Katika mwaka 2017/18 zimetengwa shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi katika kila kijiji/ shehia.

### 4.4.6 Maeneo Mengine Muhimu kwa ukuaji wa Uchumi na Ustawi wa Taifa

#### 4.4.6.1 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**(a) Mradi wa Majengo kwa Balozi za Tanzania**

Mradi unalenga kuboresha huduma kwa kujenga na kukarabati majengo ya balozi za Tanzania nje ya nchi hususani za ofisi na makazi. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 8.0 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi Kinshasa, DRC; ofisi ya Ubalozi na makazi ya watumishi Kampala, Uganda; kukarabati nyumba za Ubalozi, Lilongwe; ofisi ya Ubalozi na makaza ya watumishi Harare, Zimbabwe; jengo la ofisi ya Ubalozi Berlin, Ujerumani; jengo la ofisi na makazi ya Balozi Beijing, China; jengo la ofisi na makazi ya watumishi Pretoria, Afrika ya Kusini; ofisi ya Ubalozi na makaza ya watumishi Cairo, Misri; miundombinu ya Chuo cha Diplomasia Kurasini, Dar es salaam; ukarabati wa jingo la zamani la ofisi ya Ubalozi Washington DC, pamoja na ujenzi wa nyumba ya makazi ya Balozi Addis Ababa, Ethiopia; Brussels, na Muscat.

**(b) Mradi wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani**

Serikali itaendelea kuboresha utoaji wa huduma mipakani kwa kuendelea na ujenzi wa vituo vya Tunduma/Nakonde, Kasumulu/Songwe na Mtambaswala. Ujenzi wa kituo Tunduma/Nakonde utaboresha utoaji wa huduma katika mpaka wa Tanzania na Zambia. Pia Serikali itaendelea na maandalizi ya awali ya ujenzi wa kituo cha Kasumulu/Songwe.

## 4.5 Ushiriki wa Sekta Binafsi

### 4.5.1 Miradi ya Sekta Binafsi Moja kwa Moja

Katika kuhakikisha kuwa sekta binafsi inashiriki katika uwekezaji wa maeneo mbalimbali ya nchi, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iweze kushiriki katika utekelezaji wa Mpango. Katika mwaka 2017/18, Serikali imepanga kuimarisha miundombinu wezeshi (maji, barabara na umeme) katika kongane 4 mkoani Dodoma kwa ajili ya viwanda vya ngozi na eneo la viwanda vya nguo la TAMCO (Kibaha) pamoja na maeneo mengine ya uwekezaji.

Katika mwaka 2017/18, Baraza la Taifa la Biashara litaendelea kusimamia utekelezaji wa maazimio yenye lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendeshaji biashara nchini ikijumuisha: uandaaji wa sera, mkakati na mpango wa maendeleo wa sekta ya utalii; kuwianisha na kuhuisha sheria, kanuni, taratibu na ada zinazohusika na shughuli za uwekezaji na biashara pamoja na mashirika ya udhibiti; kuanzisha mfumo wa kieletroniki wa taarifa za kibiashara (*One Stop Information Centre*) na mfumo wa utoaji leseni za kielektroniki; kuanzisha Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (Integrated Land Information Management System) pamoja na mfumo wa MKURABITA wa upimaji wa ardhi ili kurahisisha utoaji wa hati miliki za ardhi; na kuboresha mazingira ya biashara yatakayosaidia mashirika ya ndege nchini.

### 4.5.2 Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

Katika mwaka 2017/18, Serikali imetenga Shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya (*PPP Facilitation Fund).* Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na: kuwezesha, kuratibu na kuchambua taarifa za upembuzi yakinifu na kutoa elimu kwa wadau kwa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika mwaka 2017/18, miradi ifuatayo itatekelezwa:-

(i) **DSM – Chalinze Expressway** - kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi kuweza kujenga na kugharamia mradi.

(ii) **Mradi wa kutengeneza madawa muhimu** – kufanya upembuzi yakinifu wa mradi.

(iii) **Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)** – Shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia maeneo yatakayopisha awamu ya pili ya mradi. Shughuli nyingine zitakazofanyika ni pamoja na upembuzi yakinifu awamu ya pili kwa njia ya ubia na kumpata mtoa huduma wa kudumu wa usafiri wa awamu ya kwanza na ya pili.

(iv) **Mradi wa Kinyerezi III** - TANESCO na Kampuni ya *Shanghai Electric Power Company* (SEPC) ya China ziliunda Kampuni ya Ubia inayojulikana kama SHANGTAN kwa ajili ya kuendeleza Mradi wa Kinyerezi III (MW 600). Upembuzi yakinifu wa mradi huo umekamilika. Kazi zitakazo fanyika ni pamoja na: kuendele na majadiliano kuhusu mgawanyo wa hisa katika mradi; na majadiliano kwa ajili ya kusaini mkataba wa utekelezaji yanaendelea.

## 4.6 Uwekezaji wa Mashirika na Taasisi za Umma

Serikali itaendelea kuhamasisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mashirika ya umma kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele hususan viwanda. Mashirika ya Umma yanahusishwa katika uwekezaji wa miradi mikubwa ikiwemo ya miundombinu (bandari, barabara, mawasiliano, reli na ujenzi wa viwanja vya ndege), nishati, na maeneo mengine ya kimkakati (viwanda vya chuma, madini, makaa ya mawe) ambayo yameanishwa kwenye mpango huu kama maeneo ya kipaumbele. Mifuko ya

Hifadhi ya Jamii pia imeitikia wito wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda ambapo miradi itakayotekelezwa katika mwaka 2017/18 imebainishwa katika **Kiambatisho Na. I**.

## SURA YA TANO

## UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2017/18

### 5.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/18 utagharamiwa kwa pamoja na Serikali kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, misaada na mikopo; Sekta Binafsi; na ubia kati ya sekta ya Umma na Binafsi.

### 5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2017/18

Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 11,999.6 sawa na asilimia 38 ya bajeti ya mwaka 2017/18, ya Shilingi bilioni 31,699.7 zimetengwa kwa bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 8,969.8 ni fedha za ndani na bilioni 3,029.8 za nje. Kiasi hiki kinakidhi, azma ya Serikali iliyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21, ya kutenga kati ya asilimia 30 hadi 40 ya bajeti ya mwaka kwa bajeti ya maendeleo.

Fedha hizo zitatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo mapato ya ndani, mapato ya nje, ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na uwekezaji wa sekta binafsi. Sehemu kubwa ya fedha za maendeleo zimeelekezwa kutekeleza miradi ya ujenzi wa reli kwa *Standard Gauge* (bil. 900); mfuko wa reli ( bil. 218.569); kuboresha bandari ya DSM (bil. 187.123); ununuzi wa ndege (bil. 500); Mkongo wa Taifa (bil. 10); Kinyerezi I *extension* (bil.10); Umeme vijijini (bil. 394); ukarabati wa barabara kuu na vijijini (bil. 917.5); Ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za rufaa na hospitali maalum (bil. 35.8); MSD (bil.260); Vitambulisho vya Taifa – NIDA (bil 20); ASDP (bil. 15); Mfuko wa Maji (bil. 158); Ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi na vyuo vikuu (bil.28.5); na Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu – HESLB (bil. 427).

### 5.3 Ugharamiaji wa Mpango

#### 5.3.1 Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kugharamia miradi ya maendeleo kupitia vyanzo vya ndani vya mapato vilivyopo na vyanzo vipya vikiwemo vya Halmashauri. Mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi na vyanzo vingine vya mapato ya ndani vitaendelea kuzingatiwa na Serikali katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Serikali itaendelea kutumia mifuko mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya kisekta kama vile mfuko wa barabara, mfuko wa maji, mfuko wa reli. Vile vile, Serikali itaendelea kukopa ndani ya nchi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ukomo wa kukopa ndani ya nchi usiozidi asilimia 1 ya Pato la Taifa.

### 5.3.2 Vyanzo vya Mapato ya Nje

Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kujielekeza pia kwenye misaada inayotolewa na washirika wa maendeleo. Vile vile, itakopa mikopo ya kibiashara kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu. Katika mchakato wa kukopa fedha nje ya nchi, Serikali itazingatia ukomo wa uhimilivu wa deni la Taifa kulingana na mapendekezo ya Taarifa ya Uchambuzi ya Uhimilivu wa Madeni.

### 5.3.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Katika mwaka 2017/18, Serikali itaendelea kuimarisha *PPP Facilitation Fund* kwa lengo la kugharimia uandaaji wa upembuzi yakinifu kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Matokeo tarajiwa ni ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi katika miradi ya kipaumbele kwa njia ya ubia.

### 5.3.4 Uwekezaji wa Mashirika ya Umma

Mashirika ya Umma yana mchango mkubwa katika kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Kupitia mapato yanayotokana na nyanzo vyao au/na kwa kukopa kutokana na dhamana ya mali zao, mashirika ya umma yanaweza kuongeza mtaji utakaoweza kugharamia utekelezaji wa miradi itakayobainishwa. Katika mwaka 2017/18 Serikali itaendelea kutumia mashirika ya umma katika kugharamia miradi ya maendeleo.

### 5.3.5 Ugharamiaji Kupitia Taasisi za Fedha za Ndani

Taasisi za fedha nchini zitashiriki kufanikisha utekelezaji wa Mpango 2017/18 kwa kutoa mikopo kwa wawekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB), Benki ya Kilimo pamoja na benki za biashara. Katika mwaka 2017/18, Serikali itawezesha TIB kimtaji na kuifanya kuwa chombo imara cha utafutaji wa mikopo ya utekelezaji wa miradi (arranger) na ushirikishaji wa wakopeshaji wengine (syndication). Kupitia mfumo huu, utawezesha Serikali kutumia mapato yake kuvutia uwekezaji mkubwa zaidi (leveraging).

## SURA YA SITA

## UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

### 6.1 Utangulizi

Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo uliopendekezwa unasisitiza upatikanaji wa taarifa za uhakika zitakazotumika kupima mafanikio kwa kutumia viashiria vya kitakwimu na visivyo vya kitakwimu. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/18 utazingatia mfumo na mwongozo utakaotumika katika ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ulioainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Mwongozo wa Mpango na Bajeti 2017/18. Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakuwa na malengo ya utekelezaji kwa kila sekta na kuandaa mpango kazi wa mwaka. Utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo utazingatia pia Mwongozo wa Uandaaji na Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management – Operational Manual) wa Mwaka 2015.

Aidha, katika ngazi ya Kitaifa, mfumo utatumia mbinu jumuishi ambayo itahusisha matokeo taarifa zilizotolewa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na taasisi nyingine za umma na binafsi zinazotekeleza miradi ya kimkakati  kupima matokeo kwa kutumia viashiria vya maendeleo ya jumla. Katika ngazi ya kisekta na maeneo mtambuka, taarifa zitatolewa kwa shabaha za malengo makuu na mageuzi yaliyofikiwa yanayohusiana na malengo ya kisekta na mradi au hatua za kimkakati. Katika ngazi ya miradi, utoaji taarifa umepangiliwa ili kupata taarifa za mafanikio na uapungufu utakaojitokeza, kwa mujibu wa shabaha, muda na gharama za utekelezajikama zilivyobainishwa katika Mipango kazi ya utekelezaji wa mradi.

### 6.2 Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Katika kuhakikisha ufanisi katika ufuatiliaji, tathmini na mrejesho katika utekelezaji wa Mpango, Kamati Maalum itakayosimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo itasaidiwa na Wizara ya Fedha na Mipango na itatoa taarifa kila robo mwaka ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na taasisi nyingine za umma zitahusika katika kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mpango, mapitio ya matumizi ya umma na kisekta ili kuchochea mijadala na kutoa taarifa muhimu kwa ajili ya maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka unaofuata.

Sekta binafsi kama watekezaji wakuu wa Mpango, watawajibika kutoa taarifa zitakazohitajika katika kufanya mapitio ya kisera na kuboresha utekelezaji zitakazowezesha kuondoa vikwazo vya uendelezaji wa biashara na uwekezaji. Wadau

hawa watahitajika kutoa taarifa za uhakika na sahihi katika maeneo yao ya maslahi na kiwango cha uwekezaji watakachowekeza katika biashara zao. Kwa uwekezaji mkubwa, ambao utahitaji uwezeshaji wa sekta ya umma, sekta binafsi itawajibika kuwasilisha mipango yao ya uwekezaji na kuwezesha Serikali kupanga namna ya kusaidia utekelezaji wa miradi hiyo.

## 6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango

Ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo utasaidia kupata taarifa mpya zitakazosaidia kurekebisha mapungufu yanayojitokeza katika utekelezaji na kutoa taarifa kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango ni pamoja na: kuibua changamoto halisi za utekelezaji wa Mpango na mikakati ya kutanzua changamoto hizo; kuibua vyanzo vipya vya mapato ya Serikali na mikakati ya utekelezaji wake; kuainisha maeneo ya uwekezaji na kuyatangaza kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi; na kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kuhamasisha matokeo kwa fedha zinazotumika.

## SURA YA SABA

## VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA KINGA

### 7.1 Utangulizi

Vihatarishi mbalimbali vinaweza kujitokeza katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hatimaye kuathiri utekelezaji wa Mpango mzima. Mpango huu umebainisha vihatarishi na mikakati ya kukabiliana navyo.

### 7.2 Vihatarishi katika Kutekeleza Mpango

#### 7.2.1 Vihatarishi vya Nje

**(a) Mtikisiko wa kiuchumi kikanda na kimataifa:** Mtikisiko wa kiuchumi kikanda na kimataifa unapotokea husababisha kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma za Tanzania katika masoko ya nje hivyo kuchangia kupungua kwa fedha za kigeni, ambazo ni muhimu katika kugharamia miradi ya maendeleo na uendeshaji wa uchumi.

**(b) Matukio asilia/mabadiliko ya tabia ya nchi**: Matukio asilia kama vile matetemeko, mafuriko na ukame huathiri uendelevu wa rasilimali asili na ikolojia. Hali hii endapo itatokea itasababisha kupungua kwa uzalishaji katika sekta za uzalishaji hususan kilimo, mifugo, uvuvi na utalii. Vile vile, mabadiliko ya hali ya hewa yasiyotabirika kama mvua nyingi, ongezeko la joto duniani na ukame huathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli za kiuchumi.

**(c) Siasa mbaya za kimaeneo ikiwemo vita na migogoro**: Hii inaweza pia kuathiri utekelezaji wa Mpango kutokana na kuwa matukio kama hayo yanabadili hali ya mshikamano na soko pamoja na vyanzo vya fedha kwa ajili ya uwekezaji.

**(d) Mabadiliko ya Kiteknolojia:** Teknolojia mpya zimekuwa zikivumbuliwa mara kwa mara hivyo uvumbuzi huu unaweza kuathiri utekelezaji wa mpango huu kwa namna moja ama nyingine.

#### 7.2.2 Vihatarishi vya ndani.

**(a) Upungufu wa rasilimali (fedha na watu):** Kutopatikana kwa rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati pamoja na uwiano sawa na ubora wa rasilimali watu inachangia utekelezaji duni wa mpango.

**(b) Umiliki wa Ardhi na usimamizi wa migogoro:** Muundo wa umiliki wa

ardhi umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuchelewesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutelelezwa na kuzua migogoro wakati wa ulipaji fidia.

**(c) Ukuaji Kasi wa Miji:** Uanzishwaji wa viwanda utaongeza kasi ya ukuaji wa miji ambao utaathiri utoaji wa huduma za kijamii, usalama na kusababisha milipuko ya magonjwa na hivyo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**(d) Ushiriki Mdogo wa Sekta Binafsi:** Ushiriki chanya wa sekta binafsi unahitajika katika uwekezaji na uanzilishi wa viwanda ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kufikia malengo ya mpango. Iwapo sekta binafsi haitojitokeza kwa wingi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, matarajio na malengo ya mpango hayatofikiwa.

**(e) Ongezeko la idadi ya watu:** Ongezeko la idadi ya watu lisiloendana na malengo ya Mpango wa Maendeleo linaathiri utekelezaji wa Mpango husika.

**(f) Uharibifu wa Mazingira:** Shughuli za maendeleo na wananchi kujikimu zinaathiri mazingira ikiwa ni pamoja na uangamizaji wa misitu, uchafuzi wa ardhi na vyanzo vya maji, kuenea kwa hali ya ukame, kukauka kwa vyanzo vya maji, kuharibiwa kwa mfumo wa ikolojia. Haya yakiendelea yataathiri uzalishaji na ufanisi wa sekta zote za uchumi.

## 7.3 Mikakati ya Kukabiliana na Vihatarishi

### 7.3.1 Vihatarishi vya Nje

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuongeza mauzo nje ya nchi ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni, kuainisha aina ya mauzo (bidhaa) na masoko, pamoja na kuweka mkakati mahsusi wa kulinda fursa ya masoko nje ambayo Tanzania inamanufaa zaidi;

(ii) Serikali kuendelea na jitihada za kupunguza utegemezi kwa kuwianisha mapato na matumizi, kuongeza mapato ya ndani na kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;

(iii) Juhudi kubwa zimeelekezwa katika kuwezesha Tanzania kujenga uwezo wa majadiliano na ushiriki katika kuzuia matukio yatokanayo na siasa mbaya pindi yanapotishia kutokea kimataifa na kikanda;

(iv) Kuendelea na maboresho katika mfumo wa sheria;

(v) Kuimarisha usimamizi wa sheria na misingi ya utatuzi wa migogoro; na

(vi) Kuimarisha mifumo ya kutambua mapema majanga na kuchukua tahadhari. Aidha, miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi itaendelea kutafutiwa fedha na kutekelezwa.

### 7.3.2 Viharatishi vya Ndani

(i) Kuweka mazingira wezeshi ya biashara hususan katika sekta ya fedha ili kuongeza ushindani miongoni mwa taasisi za fedha na kuwezesha kushuka kwa viwango vya riba. Aidha, Serikali itaongeza makusanyo ya mapato ya ndani ili kupunguza mikopo ya ndani kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi na kutoa fursa kwa sekta binafsi kukopa zaidi kwa ajili ya uwekezaji;

(ii) Kushirikisha wananchi na wadau katika hatua mbalimbali za utunzaji wa mazingira na kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuimarisha mifumo itakayosaidia miundombinu kuhimili mabadiliko ya tabia nchi;

(iii) Kuendelea kuboresha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji kwa kutoa mafunzo na kuziongezea nguvu idara za ufuatiliaji;

(iv) Kuhakikisha uwepo wa mipango miji inayoendana na kasi ya ukuaji wa miji ili kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii; na

(v) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari, taasisi za elimu, vyama vya wazalishaji, wasambazaji na walaji, itaendelea kutoa elimu ya Mpango na namna bora ya utekelezaji ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na mahusiano mazuri na Washirika wa Maendeleo katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango.

**KIAMBATISHO NA. I**

## MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KUPITIA UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI, MIFUKO YA HIFADHI ZA JAMII NA MASHIRIKA UMMA

### 1. Viwanda

### 1.1 Kagera Tea Company (KTC)

Mradi unalenga upanuzi wa kiwanda cha kisasa cha utengenezaji wa chai mkoani Kagera. Kiasi cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya uwekezaji huu ni Dola za Kimarekani milioni 5.7.

### 1.2 Kagera Sugar Limited

Mradi unalenga kukopesha Dola za kimarekani milioni 20.00 kutoka Mfuko wa PSPF kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda hicho ili kuongeza uzalishaji wa sukari kuweza kukidhi haja ya mahitaji ya sukari.

### 1.3 Ujenzi wa Kiwanda cha kuzalisha Bidhaa za Hospitali

Mfuko wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ina dhamira ya kujenga kiwanda kikubwa kitakachozalisha vifaa mbalimbali vya hospitali kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake. Mradi huu unatarajiwa kufanywa kwa ubia kati ya Hospitali ya Muhimbili na mwekezaji mwenye teknolojia ya kisasa na utaalam wa uzalishaji. Tayari hospitali inamiliki kiwanja eneo la Chamazi katika Wilaya ya Temeke, Mkoani Dar es Salaam na mazungumzo ya awali yameanza kwa lengo la Mfuko kuongeza mtaji ili uzalishaji huo ujikite katika kukidhi mahitaji ya vituo vya kutolea huduma hapa nchini.

### 1.4 Kiwanda cha Uzalishaji wa Gesi ya Oksijeni (oxygen)

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unadhamiria kupitia Taasisi ya Mifupa Muhimbili kuanza kuzalisha oksijeni kwa ajili ya matumizi ya hospitali hii kwa lengo la kupunguza gharama; kuongeza upatikanaji wa dawa; na bidhaa katika vituo vya kutolea huduma na hivyo kuboresha utoaji wa huduma.

### 1.5 Ujenzi wa Kiwanda cha Dawa

Kupitia majadiliano yanayoendelea baina ya umoja wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii (TSSA) na Majeshi chini ya shirika la SUMA JKT, Mfuko umebainisha fursa za uwekezaji katika kufufua uzalishaji wa dawa katika kiwanda cha dawa kinachomilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa. Jeshi liliingia makubaliano na kuyatekeleza baina yake na Kampuni inayomilikiwa na Serikali ya China kwa lengo la kuzalisha dawa kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma vinavyomilikiwa na Jeshi. Kupitia makubaliano hayo, kiwanda kilianzishwa katika kambi ya Mgulani Dar es Salaam na kilifanya kazi kwa kipindi fulani na baadae kusimamisha uzalishaji. Hivyo,

kwa sasa Jeshi lina mpango wa kukifufua kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukidhi mahitaji hata ya vituo vilivyo nje ya umiliki wa jeshi. Jeshi limetenga eneo katika kambi ya Ruvu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambapo lengo ni kujenga kiwanda kikubwa na cha kisasa kwa ajili ya kuzalisha dawa pamoja na bidhaa mbalimbali za hospitalini.

### 1.6 Kiwanda cha *Grape Processing Plant* , Chinangali

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) upo katika mazungumzo ya awali kwa kushirikiana na Mfuko wa GEPF pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kupitia benki ya TIB kuanzisha kiwanda cha "***Grape Processing Plant***". Hatua hii inafuatia kupokelewa kwa taarifa ya upembuzi yakinifu na Mpango wa Biashara kutoka kwa Mtaalam elekezi *M/s Arcquants Services Limited*. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 26.3 na kutengeneza ajira za moja kwa moja kiwandani za watu 40 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa wakulima 296 walio kwenye umoja maalum wa kilimo cha zabibu pamoja na wakulima 900 wasiokuwemo kwenye umoja huo.

### 1.7 Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Dar Es Salaam

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa pamoja imejipanga kuboresha uzalishaji katika kiwanda cha Nguo cha Urafiki kwa kutumia Teknolojia mpya na ya kisasa tofauti na ilivyo sasa ambapo Kiwanda kinatumia Teknolojia ya zamani na isiyokidhi kiwango cha uzalishaji. Kiwanda kinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania yenye hisa asilimia 49 na Serikali ya China yenye hisa asilimia 51 kupitia Kampuni ya *ChangZhou State owned Textile Assets Operations Co. Ltd*. Tathmini ya awali inaonesha kuwa kiwanda kinahitaji kiasi cha Shilingi bilioni 27.3 kubadilisha teknolojia ya mashine zinazotumika, Shilingi bilioni 22.00 kuanzisha uzalishaji wa "Garments" na pia Shilingi milioni 19.6 kufufua kitengo cha utengenezaji wa vipuri.

### 1.8 Kiwanda cha Morogoro Canvas Mill

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa pamoja imejipanga kuboresha uzalishaji katika Kiwanda cha Morogoro *Canvas Mill* kilichopo mkoani Morogoro. Tayari taarifa ya awali ya mshauri mwelekezi inaonesha kwamba hali ya kiwanda na mashine ni nzuri zina uwezo wa kuzalisha kilogramu 9,000 za yan na meta 10,000 za pamba "Fabric greige". Kiwanda kina uwezo wa kutengeneza ajira zisizopungua 700. Mwekezaji wa sasa kwa kushirikiana na Benki ya CRDB wameonyesha utayari ya kumkabidhi mwekezaji mpya kuchukua umiliki wa kiwanda hicho.

### 1.9 Vinu vya Kuchambulia Pamba vya Nyanza Cooperative Union

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa pamoja imejipanga katika kuwekeza katika vinu vya kuchambulia Pamba vya *Nyanza Cooperative Union* vilivyopo Mwanza. Umoja wa *Nyanza Cooperation* upo tayari kwa makubaliano na Mifuko ili kufufua vinu hivyo vya Pamba*. Nyanza Cooperation Union* ina mikataba na wakulima wa pamba wapatao

6,760 ambao baada ya viwanda hivi kusimama uchambuzi wa pamba ya wakulima wamelazimika kuuza pamba yao kwa vinu vya watu binafsi. Vile vile, Nyanza Cooperative Union ina eneo lenye ukubwa wa hekari 1,500 lenye uwezo wa kuzalisha mbegu za Pamba. Tayari Mshauri Mwelekezi tayari ameshatembelea Vinu vya kuchambulia pamba vya Nyamililo, Buyagu, Kasamwa, Magu, Nassa, Ngasamo, Nyambiti, Manawa Bukumbi na Buchosa vilivyoko katika Mikoa ya Mwanza, Geita na Simiyu ili kuona hali halisi na kufanya tathmini ya kina.

### 1.10 Kiwanda cha Sukari – Gereza la Mbigiri Dakawa Morogoro

Mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PPF na Jeshi la Magereza. Mradi unahusisha kilimo cha miwa kwenye shamba lenye ukubwa wa hekari 12,000, uendelezaji wakulima wa pembezoni mwa kiwanda (out growers), na ufufuaji wa kiwanda cha kuzalisha sukari ambacho kinatarajia kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka. Uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2017.

### 1.11 Kiwanda cha Kutengeneza Viatu – Gereza la Karanga Moshi

Mradi unatekelezwa kwa ubia baina ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza (Gereza la Karanga – Moshi). Mradi unahusisha upanuzi wa kiwanda kwa ajili ya kuzalisha viatu na bidhaa za ngozi kwa matumizi ya majeshi ya Tanzania pamoja na raia hususan wanafunzi. Mradi unatarajiwa kuzalisha futi 3,750,000 za ngozi (blue hides), soli 900,000 za aina tofauti na bidhaa za ngozi 48,000,000 kwa mwaka na jozi 4000 za viatu kwa siku. Hati ya makubaliano ya mradi (MoU) imesainiwa Oktoba 2016. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 56.64 na mradi unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja na miezi miwili (miezi 14) na kurudisha fedha ndani ya miaka 4 na vile vile kutengeneza ajira za moja kwa moja za watu 707.

### 1.12 Mradi wa Viuadudu (Biolarvicides), Kibaha

Mradi unahusisha uwekezaji utakaokamilisha uzalishaji wa Majaribio (commissioning & trial runs/production) katika kiwanda cha Viuadudu (Biolarvicides) katika Mji wa Kibaha. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa NSSF umetoa mkopo wa Dola za Kimarekani Milioni 2.1 kama mtaji wa uendeshaji na uzalishaji umeanza Septemba 2016. Mradi huu unaotumia teknolojia kutoka nchini Cuba una lengo la kufikia lita milioni 6 kwa mwaka za viuadudu kwa ajili ya soko la ndani na nje. Mradi huu umekwisha tengeneza ajira za moja kwa moja kwa watu zaidi ya 150.

### 1.13 Viwanda vya Kusindika Nafaka na Ukamuaji wa Mafuta

Mradi huu unahusu ufufuaji na upanuzi wa viwanda vya usagaji nafaka Iringa, ukamuaji mafuta ya alizeti Dodoma na uwekaji wa mashine za usagaji nafaka Mwanza ambavyo vinamilikiwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB).

Mradi unatarajiwa kugharimu Shilingi bilioni 40.67 ambapo utafanywa kwa awamu mbili kwa kuanzia na Shilingi bilioni 13.86 za upanuzi wa kinu cha Iringa na Shilingi bilioni 18.81 kwa ajili ya ujenzi ya kinu cha ukamuaji mafuta ya alizeti Dodoma. Mkopo kwa ajili ya vinu vya Iringa na Dodoma uliidhinishwa Agosti, 2016 na NSSF inatarajiwa kuanza uzalishaji. Miradi inategemea kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zaidi ya 4000.

### 1.14 Pipes Industries Company Limited (PICL)

Mradi unahusisha Kampuni ya utengenezaji wa mabomba ya GRP, HDPE na PVC. Mradi unatarajia kugharimu Dola za Kimarekani milioni 39. Mfuko wa PSPF unangoja taarifa za kina kutoka PICL kabla kuamua kuwekeza.

### 1.15 Kiwanda cha Kutenegenza *Agave Syrup* (Natural Sweetener)

Mradi utashirikisha bodi ya katani na mwekezaji kutoka Marekani kupitia kampuni ya Tierra Group pamoja na Mfuko wa PSPF. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia Dola za Kimarekani milioni 8.5. Hati ya Makubaliano (MoU) imekwisha andaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na PSPF inatarajiwa kusaini makubaliano hayo baada ya uhakiki. Hatua zinazotarajia kutekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu na uwekezaji kuanza Septemba 2017. Mradi unatarijia kutoa ajira ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa watu 200 na kuwanufanisha wakulima zaidi ya 2000.

### 1.16 Uzalishaji wa Wanga Kutokana na Zao la Muhogo na Viazi Vitamu

Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSPF na Kampuni ya CSTC ambao wana mpango wa kuzalisha wanga kwa kutumia muhogo na viazi vitamu mkoani Lindi katika eneo linalokadiriwa kuwa na hekta 7,000 ambapo tayari kampuni ya CSTC imemilikishwa hekta 3,000 katika ukanda wa juu wa makonde na eneo la hekta 1,200 za ziada. Eneo la ujenzi wa kiwanda limekwisha ainishwa (Kijiji cha Mbalala) na tathmini ya kulipa fidia inaendelea. Mradi utagharimu Dola za Kimarekani milioni 15 ambapo PSPF inadhamiria kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 5 kupitia hisa. Mradi utakapokamilika unatarajiwa kutengeneza ajira zaidi ya 1,500.

### 1.17 Tanzania *Pharmaceutical Industries*

Mfuko wa PSPF ulitoa mkopo wa kiasi cha Shilingi bilioni 1.0 na kununua hisa za upendeleo za thamani ya Shilingi bilioni 1.5 kwa TPI ili kukiwezesha kiwanda kuanza uzalishaji wa madawa kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Wawekezaji wengine katika mradi huu ni Barclays na SATF. Mradi unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka 2017/18.

### 1.18 Ufufuaji wa Kiwanda cha Chai cha Mponde kilichopo Lushoto Mkoani Tanga

Mfuko wa LAPF umefikia makubaliano na wanahisa wa Kiwanda cha Mponde juu ya utayari wa kuingia ubia wa kufufua kiwanda (The Agreement of Intent). Gharama za mradi husika zinatarajia kufikia Shilingi bilioni 10 na jumla ya wafanyakazi kati ya 30 na 40 wanatarajiwa kuajiriwa. Mradi utawanufaisha wakulima kati ya 250 mpaka 300 ambao watapata soko la majani ya Chai. Kwa sasa mfuko unasubiria hatma ya kesi iliyopo kati ya Serikali na wamiliki wa kiwanda ili hatua zingine ziendelee.

### 1.19 Mradi wa Kutengeneza Bidhaa za Hospitali na *Intravenous (IV) Fluids*.

Mfuko wa LAPF umeonesha nia ya kuwekeza katika kiwanda cha kutengeneza bidhaa za hospitali na intravenous (IV) fluids. Nyaraka mbalimbali zitakazowezesha kufanyika upembuzi yakinifu ili kutoa mwongozo kwa Mfuko kushiriki katika uwekezaji huu zimekwisha wasilishwa yanasubiria kufanyiwa maamuzi.

### 1.20 Mradi wa Machinjio na Usafirishaji wa Nyama wa Nguru Ranch Mkoani Morogoro.

Mfuko wa LAPF upo kwenye mawasiliano na wamiliki wa kiwanda, kwa nia ya kutambua kiasi kinachohitajika kwenye uwekezaji, aina ya uwekezaji na mipango ya upanuzi. Upembuzi ambao uliokwishafanyika unaonyesha kuwa kiwanda kina faida mbalimbali mojawapo ni ununuzi wa mifugo kutoka kwa wafugaji wa Mkoa wa Morogoro na kutoa mafunzo ya ufugaji bora kwa wafugaji ili waweze kupata mifugo yenye ubora unaotakiwa kwenye kiwanda. Kiwanda hicho kina mpango wa kuweka mazalio ya samaki wa kuuza kutokana na maji na malighafi inayobaki baada ya kuchinja ng'ombe na mbuzi. Kiwanda hicho kinatarajiwa kutoa ajira ya moja kwa moja zaidi ya 300.

### 1.21 Kiwanda cha Kilimajaro Machine Tools, Kilimanjaro (KMTC).

Mfuko wa GEPF una lengo la kuwekeza katika mradi wa ujenzi na ufufuaji wa kinu (foundry) cha vipuri katika kiwanda cha *Kilimajaro Machine Tools* cha Mkoani Kilimanjaro. Gharama za mradi zinakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 10.3. Mfuko umekwishakamilisha kupitia andiko la mradi na kuwasilisha mapendekezo yake kwenye uongozi wa NDC Oktoba, 2016. Katika mwaka 2017/18, Shilingi milioni 150 zinahitajika na Shilingi bilioni 1.6 fedha za mkopo kutoka GEPF kwa ajili ya: kuendelea na uzalishaji wa mashine za mbao na vipuri; kufanya utafiti wa namna ya kuifanya KMTC iwe kituo cha kuzalisha vipuri Tanzania; kuendelea kutangaza bidhaa za KMTC; kujenga foundry kubwa; kufanya ukarabati wa mfumo wa umeme wa kiwanda; na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi. Kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

### 1.22 Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Tandahimba na Newala

Tandahimba and Newala Cashewnut Union (TANECU) chini ya ufadhili wa Benki ya TIB wamepanga kufufua na kuendeleza kiwanda cha kuendeleza Korosho Mkoani Mtwara. Benki ya TIB imewasilisha mapendekezo ya ushirikiano wa pamoja (Joint Venture) ili kuwezesha ufufuaji na uendelezaji wa kiwanda hicho.

### 1.23 Ujenzi wa Kiwanda cha Uzalishaji wa Bidhaa za Hospitali, Simiyu

Kwa kuzingatia upatikanaji wa malighafi ya pamba kwa wingi Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unashirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu kujenga kiwanda cha bidhaa za pamba na maji tiba yanayotumika hospitalini. Mkoa wa Simiyu umekwisha tenga na kutoa ardhi eneo la Nyaumata, Wilaya ya Bariadi na NHIF imeingia makubaliano (MoU) na Taasisi nyingine za Umma za TIB, MSD, TFDA, TIRDO, TEMDO, NEMC na NDC; kuingia mikataba ya utekelezaji wa upembuzi yakinifu utakaofanywa na TIRDO kwa ajili ya huduma za ushauri wa kitaalamu. Benki ya TIB imekubali kutoa fedha za awali Shilingi milioni 150 za usaidizi wa kitaalam na NDC wametengeneza Hadidu za Rejea zitakazotumika na wataalamu kufanya upembuzi yakinifu.

### 1.24 Mradi wa Kuzalisha Mafuta ya Mawese

Mradi utaendeshwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa kushirikiana na kampuni ya ubia Nava Bharat Venture (NBV). Kiasi cha hekta 4,000 katika kijiji cha Kimala Misale, Kisarawe, Pwani zimekwishapatikana kwa ajili ya mradi na umilikishaji upo katika hatua za mwisho za uhaulishaji wa ardhi hiyo. Mradi unahitaji hekta 10,000, ambapo hekta 6,000 zitapatikana kutoka vijiji vya jirani baada ya mradi kuanza. Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 270 zitawekezwa kutekeleza shughuli zifuatazo: kukamilisha umiliki wa hekta 4000 katika Kijiji cha Kimala Misale; kufanya tathmini ya athari za mradi kijamii, kiuchumi na katika mazingira na kupata cheti; kuwezesha kuanza kwa mradi wa kilimo cha michikichi na kujenga kiwanda katika kijiji cha Kimala Misale; kufuatilia eneo la ziada kwa ajili ya mradi (hekta 6,000) katika vijiji vya Dutumi na Madege; na kuhamasisha wakulima wadogo kuhusiana na kilimo cha mkataba na kusimamia na kutathimini shughuli za mradi.

### 1.25 Mradi wa Kiwanda cha Mbolea Asili (Biofertilizer)

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 560 zitawekezwa na shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi wa Kiwanda cha Mbolea Asili (Biofertilizer), katika Eneo la Kiwanda cha Biolarvicides (Viuadudu) ni: kumuajiri mtaalamu mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu; kuanza ujenzi wa kiwanda cha mbolea asili isiyo na kemikali; na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

### 1.26 Maeneo ya Viwanda ya KMTC na Kange

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 610 zitawekezwa na shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi wa kujenga miundombinu katika eneo la viwanda la KMTC na

Kange (Tanga) ni: kugawa eneo la viwanda la KMTC lenye ukubwa wa hekta 229.13 lililoko Wilayani Hai, Mkoani Kilimanjaro; usanifu wa barabara za ndani katika eneo la KMTC; kufanya usanifu wa mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa maji na Kusimamia na kutathmini shughuli za mradi. Kwa upande wa eneo la Kange Tanga Shilingi milioni 260 zitawekezwa kwa ajili ya: kufanya usanifu na ujenzi wa barabara za ndani; kuunganisha miundombinu ya usambazaji wa maji na umeme katika eneo la viwanda Kange na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

### 1.27 Mradi wa Mgodi wa Mawe wa Kuzalisha Kokoto za Reli

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 170 zitawekezwa na shughuli zilizopangwa kufanyika katika mradi wa mgodi wa mawe wa kuzalisha kokoto za reli, ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nguzo za umeme, taa za barabarani na simu (concrete electric poles) - Muheza Tanga ni: kukamilisha taratibu za kupata hati ya umiliki wa ardhi; kuandaa andiko la mradi kwa ajili ya kupata fedha za kuaza uzalishaji; kuomba mkopo kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kununua mitambo ya kusaga kokoto; kufunga mitambo na kuanza uzalishaji; na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

### 1.28 Kuendeleza Kongane (Clusters) za Viwanda vya Ngozi

Mradi unalenga kutatua changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya viwanda vya ngozi katika eneo la hekta 107 Zuzu mkoani Dodoma ili kuongeza ufanisi kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu duni, ukosefu wa mitaji, masoko na teknolojia duni. Wasindikaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi watapatikana vifuasi na huduma nyingine muhimu kwa urahisi katika eneo moja. Katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya: ujenzi wa kongane la sekta ya ngozi na bidhaa za ngozi; kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa Mpango wa Biashara; kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan); kuandaa "Layout Plan and Detailed Design"; kufanya tathmini ya athari ya mazingira (Strategic Environmental Assessment - SEA); ujenzi wa miundombinu ya usafishaji taka; uwekaji wa mfumo wa umeme; ujenzi wa barabara ndani ya kongane; kuandaa Hadidu za Rejea za kuwapata Wataalamu Waelekezi; kusimamia na kuratibu shughuli zote za mradi; na kuanza ujenzi wa baadhi ya majengo ya kufanyia shughuli za viwanda (industrial sheds).

## 2. Ubunifu na Teknolojia

### 2.1. Shirika la Teknolojia ya Magari (TATC - Nyumbu)

Mradi unalenga kujenga uwezo wa ndani wa nchi katika kuunganisha/ utengenezaji wa magari ya *armoured personnel carrier* (APC) na malori ya mizigo mizito la Nyumbu (heavy duty Nyumbu trucks) kwa matumizi mbalimbali ikiwemo usafirishaji wa mizigo. Mradi unapangwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Kituo cha Teknolojia ya Magari – Nyumbu na Kampuni ya NORINCO kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Mradi unatarajia kugharimu jumla ya Shilingi bilioni 149 lakini utatekelezwa kwa awamu. Katika awamu ya kwanza mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 21.05 zitawekezwa kwa ajili ya kutengeneza gari 2 za mfano za APC, kutengeneza magari 10 ya APC, lori la mizigo mizito la Nyumbu, ununuzi wa vifaa maalum na kugharamia mafunzo ya wataalam wa TATC nchini China na gharama za kujikimu za wataalam kutoka Kampuni ya NORINCO kutoka China kuja kutoa mafunzo kwa wataalam na mafundi mchundo wa TATC nchini.

### 2.2. Kuendeleza Teknolojia ya Makaa ya Mawe

Mradi huu unalenga kuanzisha na kutumia teknolojia itakayowezesha kutumia vumbi la makaa ya mawe ili kuzalisha mkaa safi wa coal briquette (makaa ya mawe yanayotumika katika majiko) ambayo hayana moshi kabisha ili yaweze kutumika kama mbadala wa kuni na mkaa utokanao na miti kwa matumizi ya nyumbani na viwandani. Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira, utaongeza ajira na kipato cha mtu mmoja mmoja.

### 2.3. Kuimarisha Uzalishaji wa Nguo na Viatu

Wakuu wa nchi za EAC katika kikao chao cha mwezi Machi, 2016 waliagiza kupunguza matumizi ya viatu na nguo za mitumba kwa awamu ndani ya miaka mitatu. Mpango wa kutekeleza maagizo hayo katika sekta ya ngozi kwa 2017/2018 ni: kuwatambua watengenezaji wa viatu na bidhaa za ngozi; kuweka huduma muhimu katika maeneo ya kimkakati ili kusaidia watengenezaji wa viatu wadogo kwa kuanzia mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mwanza, Dodoma, Tabora na Shinyanga; kuanzisha vituo vya kuoneshea bidhaa za wazalishaji wadogo wa ngozi na bidhaa za ngozi kwa lengo la kuwezesha bidhaa zao kulifikia soko kiurahisi; kuwatambua na kuwasajili waagizaji na wauzaji wa viatu na bidhaa za ngozi kwa nia ya kuwafanya wafanye kazi kwa kuzingatia sheria na kuhamishia ajira ya wauzaji waliokuwa wanauza viatu na bidhaa za mitumba kutumika kuuza viatu na bidhaa mpya; na kuhamasisha taasisi za Serikali kama vyombo vya ulinzi na usalama, shule, kununua viatu, buti za jeshi, gloves, mikanda, kutoka katika viwanda vya ngozi na bidhaa za ngozi vya ndani ya nchi.

## 3. Kilimo cha Mazao

### 3.1 Mradi wa Mashamba ya Mpira - Morogoro na Tanga

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 430 zitawekezwa na shughuli zilizopangwa kufanyika ni: kutafuta na kubaini mbegu bora za mpira kwa ajili ya kupanda katika maeneo yaliyo wazi; kutafuta mwekezaji wa muda mrefu wa kuingia naye ubia katika kuendeleza mashamba ya mpira; kutafuta na kubaini maeneo mapya yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha mpira; na kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

### 3.2 Mradi wa Kilimo cha Ufuta katika Kijiji cha Mandawa

Katika mwaka 2017/18 Shilingi milioni 150 zitawekezwa kwa ajili ya: kukamilisha umiliki wa ekari 2,000 katika kijiji cha Mandawa; kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kilimo cha ufuta katika vijiji vya Mandawa, Hoteli Tatu na Likawage; kukamilisha taratibu za kumilikishwa ardhi katika vijiji vya Mandawa, Hoteli Tatu na Likawage; kutafuta mwekezaji kwa ajili ya kilimo cha ufuta katika vijiji vya Mandawa, Hoteli Tatu na Likawage; kuhamasisha wakulima wadogo kwa ajili ya kilimo cha mkataba; kusimamia na kutathmini shughuli za mradi.

## KIAMBATISHO NA. II

# BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO, 2017/18

| VOTE | VOTE NAME | PROJECTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | ARCHIVES MANAGEMENT DEPARTMENT | 6284 | Public Service Reform Programme II | 2,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 2,000,000,000.00 | - |
| 5 | NATIONAL IRRIGATION COMMISSION | 4486 | Agriculture Sector Development Program | 5,600,000,000.00 | 6,815,947,000.00 |
| | | 4496 | ASDP | - | - |
| | | | Expanded Rice Production Project | - | 7,282,665,150.00 |
| | | 4498 | CFAST | - | 404,800,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 5,600,000,000.00 | 14,503,412,150.00 |
| 7 | THE TREASURY REGISTRAR | 6251 | Public Finance Mgt Reform Programme | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| 14 | FIRE AND RESCUE FORCE | 6311 | Acquisition &Renovation Fire Buildings | - | - |
| | | 6582 | Fire and Rescue Services | 3,500,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 3,500,000,000.00 | - |
| 16 | ATTORNEY GENERAL OFFICE | 6389 | Construction of Office Building | - | - |
| | | 6550 | UNDP Support Programme | - | - |
| | TOTALVOTE | | | - | - |
| 21 | THE TREASURY | 4903 | Village Empowerement | 60,000,000,000.00 | - |
| | | 4916 | Small Enterpreneurs Loan Facilities | - | - |
| | | 4945 | PPP Faciltation Fund | 5,000,000,000.00 | - |
| | | 5491 | Global Fund Management Project | - | 2,293,002,878.00 |
| | | 6206 | IRDP Expansion | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6251 | Implementation of Best Programme | 600,000,000.00 | 500,000,000.00 |
| | | | Public Finance Mgt Reform Program | 600,000,000.00 | 500,000,000.00 |
| | | 6255 | TRA Tax Modernization Project | - | - |
| | | 6265 | Programme to support to National Authori | - | 1,195,020,526.00 |
| | | 6294 | MDAs Performance Budget Support and Mgt | 1,295,000,000,000.00 | - |
| | | 6296 | Regional Support on Budget Process | 100,000,000.00 | 135,354,000.00 |
| | | 6338 | Construction of UN Building | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6508 | Poverty Monitoring Master Plan (PMMP) | 200,000,000.00 | - |
| | | 6575 | Tanzania Statistical Master Plan Project | 500,000,000.00 | 27,013,324,337.00 |
| | TOTALVOTE | | | 1,364,000,000,000.00 | 31,636,701,741.00 |
| 23 | ACCOUNTANT GENERAL DEPARTMENT | 6251 | Expenditure Management | - | 68,000,000.00 |
| | | | Public Finance Mgt Reform Programme | 2,000,000,000.00 | 1,532,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 2,000,000,000.00 | 1,600,000,000.00 |
| 28 | MINISTRY OF HOME AFFAIRS-POLICE | 5415 | Child Protection and Participation Progr | - | 253,623,000.00 |
| | | 6107 | Technical Equipments(Radio and Access) | 237,500,000.00 | - |
| | | 6210 | Strengthening Tanzania Anti-Corruption A | - | - |
| | | 6301 | Construction of Offices & Quarters ZNZ | 200,000,000.00 | - |
| | | 6302 | Construction of Office &Quarters TZ | 300,000,000.00 | - |
| | | | Construction of Office and Quarter | 2,100,000,000.00 | - |
| | | | Construction of Offices & Quarters TZ | 1,350,000,000.00 | - |
| | | | Police Mtwara | 132,500,000.00 | - |
| | | | Police Njombe | 530,000,000.00 | - |
| | | 6303 | Rehabilitation of Police Buildings | 150,000,000.00 | - |
| | | 6389 | Construction of Office Building | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 5,000,000,000.00 | 253,623,000.00 |
| 29 | MINISTRY OF HOME AFFAIRS-PRISONS SERVICES | 1201 | Enhancement of Prison Industries | 2,200,000,000.00 | - |
| | | 6306 | Completion of Prison Wards | - | - |
| | | 6307 | Completion of Staff Houses | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 6308 | Rehabilitation of Central Prisons | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6517 | UNICEF Support to Multisectoral | - | 54,742,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 7,200,000,000.00 | 54,742,000.00 |
| 30 | PRESIDENT'S OFFICE AND CABINET | 4921 | Property and Formalization Program | 1,500,000,000.00 | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | SECRETARIAT | | | | |
| | | 6109 | National Expenses Management Project | 3,500,000,000.00 | - |
| | | 6203 | Supp. to Prevention of Corruption Bureau | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6208 | Strengthening Tanzania Ant- Corr. Action | - | - |
| | | 6211 | Policy Coherence | - | - |
| | | 6220 | Support to Tanzania Social Action Fund | 3,000,000,000.00 | 357,570,890,000.00 |
| | | 6339 | Rehabilitation of State House | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 6391 | Uongozi Institute | 1,000,000,000.00 | 7,500,000,000.00 |
| | | 6405 | African Union Advisory Board Building | - | - |
| | | 6576 | Presidential Trust Fund | 500,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 14,500,000,000.00 | 365,070,890,000.00 |
| 31 | VICE PRESIDENT'S OFFICE | 5301 | Climate Change Adaptation Programme | 850,000,000.00 | 1,400,000,000.00 |
| | | 5303 | National Biosafety Programme | 54,000,000.00 | 1,826,352,437.00 |
| | | 5304 | O-Zone Depleting Substance Project | 89,750,000.00 | 227,500,000.00 |
| | | 5305 | Stockhome Conversion Implementation Proj | 63,500,000.00 | 334,600,000.00 |
| | | 5307 | The National Environment Trust Fund | 334,454,000.00 | - |
| | | 6309 | Const of V/P office &residence in Znz | 400,000,000.00 | - |
| | | 6389 | Const and Rehab of V/P offices and S/lod | 600,000,000.00 | - |
| | | 6569 | Lake Tanganyika Enviroment Mgmt.Project | 531,896,000.00 | - |
| | | 6571 | EMA Implementation Support Progamme | 76,400,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 3,000,000,000.00 | 3,788,452,437.00 |
| 32 | PRESIDENT'S OFFICE-PUBLIC SERVICE MANAGEMENT | 6251 | PFMRP | - | - |
| | | 6284 | Public Service Reform Program II | 7,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 7,000,000,000.00 | - |
| 33 | ETHICS SECRETARIAT | 6212 | Strenghening Public Awareness on PLCE | - | 1,650,000,000.00 |
| | | 6234 | Support to Ethics Project | - | - |
| | | 6389 | Construction of Office Building | - | - |
| | | | Strenghening Public Awareness on PLCE | - | - |
| | TOTALVOTE | | | - | 1,650,000,000.00 |
| 34 | MINISTRY OF FOREIGN AFFAIRS AND EAST AFRICA COOPERATION | 6391 | Acquisition, Expan and Rehab. of Mission | 8,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 8,000,000,000.00 | - |
| 35 | PUBLIC PROSECUTIONS DIVISION | 6208 | Strengthening Tanzania Ant- Corr. Action | - | - |
| | TOTALVOTE | | | - | - |
| 37 | PRIME MINISTER'S OFFICE | 4494 | MIVARF | 700,000,000.00 | 42,445,159,919.00 |
| | | 4937 | Governments Press Development Programme | - | - |
| | | 4944 | Private Sector Competitive Programme | 300,000,000.00 | 16,258,594,844.00 |
| | | 5306 | Strengthening Climate Information | - | 1,021,618,000.00 |
| | | 6351 | Construction of PMO Building | 5,000,000,000.00 | - |
| | | 6403 | Tanzania Strategic Cities Project | - | - |
| | | 6510 | Devt of Capital City- Dodoma | - | - |
| | | 6575 | Strengthening National Disaster Prepared | - | 440,000,000.00 |
| | | 6577 | Mwananchi Empowerment Fund Project | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 6,000,000,000.00 | 60,165,372,763.00 |
| 38 | DEFENCE | 6103 | Defence Schemes | 4,150,000,000.00 | - |
| | | 6327 | Construction & Reh of Buildings | 3,850,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 8,000,000,000.00 | - |
| 39 | NATIONAL SERVICE | 6327 | Constc and Rehab of Nation Service build | 6,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 6,000,000,000.00 | - |
| 40 | JUDICIARY | 6210 | Strengthening anti corruption programme | - | - |
| | | 6215 | Citizen Centric Judiacial Modernization | - | 1,066,508,000.00 |
| | | 6296 | Child Justice Programme | - | 91,503,000.00 |
| | | 6310 | Contruction and Rehab of DistriCourt Bld | 5,970,000,000.00 | - |
| | | 6311 | Expansion of IJA Building | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6312 | Contruction and Rehab of Prim Court Bld | 2,530,000,000.00 | - |
| | | 6313 | Rehabilitation of Court of Appeal | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 6314 | Contruction and Rehab of High Court Bld | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 6391 | Contruction and Rehab of Judges Houses | 1,500,000,000.00 | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | TOTALVOTE | | | 17,000,000,000.00 | 1,158,011,000.00 |
| 41 | MINISTRY OF CONSTITUTION AFFAIRS AND JUSTICE | 6201 | e-Justice | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6517 | UNICEF Support to Multisectoral | - | 1,806,020,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 1,000,000,000.00 | 1,806,020,000.00 |
| 42 | THE NATIONAL ASSEMBLY FUND | 6251 | Public Finance Management Reform Program | - | 200,000,000.00 |
| | | 6318 | Information Communication and Technology | 2,800,000,000.00 | - |
| | | | Rehabilitation of Office Building | 3,000,000,000.00 | - |
| | | | Rehabilitation of Parliamentary Building | - | - |
| | | 6360 | Parliamentary Infrastructrure Project | 1,200,000,000.00 | - |
| | | | Parliamentary Infrastructure Project | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 7,000,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| 43 | MINISTRY OF AGRICULTURE, LIVESTOCK DEVELOPMENT AND FISHERIES - AGRICULTURE SECTOR | 2221 | Agriculture Training Institute | - | - |
| | | 4486 | Agriculture Sector Development Program | 57,150,000,000.00 | - |
| | | 4492 | Compsive Agri. Dev.Lower Rufiji | 250,000,000.00 | - |
| | | 4493 | Agriculture Sector Dev. Programme | - | - |
| | | | Southern Agricultural Corridor of TZ | 1,500,000,000.00 | - |
| | | 4496 | Expanded Rice Production Project | 200,000,000.00 | 7,688,303,800.00 |
| | | | Expanded Rice Production Project(ERPP) | - | 2,911,696,200.00 |
| | | 4497 | Storage Capacity Expansion Project | - | 61,100,000,000.00 |
| | | 4498 | CFAST | 500,000,000.00 | 18,953,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 59,600,000,000.00 | 90,653,000,000.00 |
| 44 | MINISTRY OF INDUSTRY, TRADE AND INVESTMENT | 1122 | Lake Natron | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 1208 | SMEs Industrial Infrastructure Exp & Cap | - | - |
| | | 1209 | Strenghening TWLB Capacity for efficienc | - | - |
| | | 1210 | Revival of General Tyre & Rubber Plantat | 70,000,000.00 | - |
| | | 1214 | Integrated Industrial Development Prog. | 10,000,000.00 | - |
| | | 3160 | Mchuchuma Coal to Electricity Project | 100,000,000.00 | - |
| | | 3161 | Liganga Vanadium Titanium | 100,000,000.00 | - |
| | | 4486 | Agriculture Sector Development Program | - | - |
| | | 4901 | Implementation of Best Programme | - | - |
| | | 4920 | Tanzania Mini Tiger Plan 2020 | 11,483,360,000.00 | - |
| | | 4933 | EPZ Development | 1,200,000,000.00 | - |
| | | 4938 | Rural Micro, Small & Medium Enterprises | - | - |
| | | 4941 | Coordination of Develop Budgets and Proj | - | - |
| | | 4948 | KAIZEN | 100,000,000.00 | - |
| | | 4949 | Support for Trade Mainstreaming | 300,000,000.00 | - |
| | | 6253 | Support Gender Mainstreaming in Trade | 50,000,000.00 | - |
| | | 6260 | Institutional Support | 58,161,708,000.00 | 265,309,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 73,575,068,000.00 | 265,309,000.00 |
| 45 | NATIONAL AUDIT OFFICE | 6210 | Strengthening Tanzania Ant- Corr. Action | - | - |
| | | 6233 | Instutional Support to OCAG | 800,000,000.00 | - |
| | | 6245 | Good Financial Governance Programme | 400,000,000.00 | 2,300,948,000.00 |
| | | 6251 | PFMRP | 400,000,000.00 | 1,500,000,000.00 |
| | | 6327 | Construction and Rehabilitation of Bldgs | 6,400,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 8,000,000,000.00 | 3,800,948,000.00 |
| 46 | MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY | 2225 | Institute of Marine Science Project | - | - |
| | | 2228 | Support on Research and Development | - | 16,338,695,082.00 |
| | | 3280 | Rural Water Supply and Sanitation | - | 1,037,435,000.00 |
| | | 4302 | Program for Agriculture&Natural Resource | - | - |
| | | 4304 | University of Dodoma Project | 1,700,000,000.00 | - |
| | | 4305 | UNICEF Support to Basic Education | - | 1,762,311,500.00 |
| | | 4306 | Rehabilitation of ADEM | 500,000,000.00 | - |
| | | 4312 | Education Sector Development and program | - | 36,325,000,000.00 |
| | | | Education Sector Development Program | - | 124,051,011,004.00 |
| | | 4314 | Mkwawa Univers. College of Educat.Projec | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4320 | Srengthening Tanzania Institute of Educ. | 40,000,000,000.00 | - |
| | | 4321 | Primary Education Dev. Programme | - | |

| VOTE | VOTE NAME | PROJECTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | (LANES) | | 39,798,464,881.00 |
| | | 4323 | Teacher Education Support Program(TESP) | - | 15,690,000,000.00 |
| | | 4340 | Higher Education Students Loans | 427,554,000,000.00 | - |
| | | 4341 | Construction of Mwl J.K. Nyerere Univers | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 4358 | Nelson Mandela Project | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4370 | Community Intervention (CBAE/COBET) | - | - |
| | | 4371 | Rehabilitation of Schools and Colleges | 2,500,000,000.00 | 6,170,041,582.00 |
| | | 4378 | ICT in Education | - | - |
| | | 4381 | Mwalimu Nyerere Memorial Academy | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4383 | DAR ES SALAAM UNIVERSITY COLLAGE OF EDUC | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4384 | DIT Teaching Tower | 1,500,000,000.00 | - |
| | | 4390 | Secondary Education Dev. Prog.(SEDP) | - | - |
| | | 4392 | Support of Science & Tech | - | - |
| | | 4393 | Colleges & Inst. Food Ration &PT/BTP | 27,415,616,000.00 | - |
| | | 4397 | Support VETA | 54,800,000,000.00 | 5,382,362,200.00 |
| | | 4398 | Open University College | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4575 | TCU | - | - |
| | | 5492 | Support of Science & Tech(ESPJ) | - | 57,783,750,000.00 |
| | | 6212 | Rehabilitation of Govt Building | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6229 | Rehabilitation of Folk Dev Collg FDCs | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 6235 | Strengthening Inspectorate | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6324 | Construction of Dodoma Library | 500,000,000.00 | - |
| | | 6333 | Expansion and Rehab. of ATC | 1,000,000,000.00 | 562,110,000.00 |
| | | | Mbeya Institute Of Science and Technolog | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 6336 | Rehabilitation & Expansion Project-DSM | - | - |
| | | 6345 | Research and Development | 10,000,000,000.00 | 3,671,024,751.00 |
| | | 6350 | Rehabilitation and Expansion Project DSM | 5,500,000,000.00 | - |
| | | 6352 | TAEC Laboratories | 1,500,000,000.00 | - |
| | | 6353 | Mzumbe University Constr.of PMO Building | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6354 | Rehabilitation and Expansion -UCLAS | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 6359 | NACTE PROJECT | - | - |
| | | 6361 | Rehabilitation & Expansion Project-SUA | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 6363 | Rehabilitation of Arusha Technical Colle | - | - |
| | | 6364 | Rehabilitation & Expansion - MUHAS | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6365 | Rehabilitation & Expansion - MUCCOBS | 1,300,000,000.00 | - |
| | | 6389 | Tanzania Education Authority | 10,000,000,000.00 | - |
| | | 6574 | Climatic Change Adapt. and Mit. in TZ | - | 1,500,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 606,769,616,000.00 | 310,072,206,000.00 |
| 48 | MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENTS DEVELOPMENT | 2324 | International Boundaries | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 2326 | Planning, Surveying & Land Titling Prog | 8,000,000,000.00 | - |
| | | 2327 | Implementation of Kigamboni New City m p | - | - |
| | | 2328 | Promotion of Appropriate Tech. for Affor | 300,000,000.00 | - |
| | | 4942 | Private Sector Competitiveness Project | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4943 | Land Tenure Support Programme | 2,000,000,000.00 | 9,000,000,000.00 |
| | | 6327 | Construction and Rehabilitation of Build | 1,100,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 16,400,000,000.00 | 9,000,000,000.00 |
| 49 | MINISTRY OF WATER AND IRRIGATION | 2325 | Monitoring and coordination of WSDP | 1,954,798,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| | | 3216 | Expans.and Rehabil. of rural water suppl | 20,702,742,400.00 | 4,000,000,000.00 |
| | | 3223 | Borehole Drilling&Dams Construction | 12,483,257,600.00 | - |
| | | 3280 | Rural Water Supply and Sanitation | 158,500,000,000.00 | - |
| | | 3306 | Rehab & Expansion of Urban Water Supply | 15,800,000,000.00 | 36,510,000,000.00 |
| | | 3307 | Expansion of Urban Water Supply | 63,000,000,000.00 | 28,000,000,000.00 |
| | | 3308 | MOWI Institutional Strengthening | 10,275,845,000.00 | 1,071,745,000.00 |
| | | 3309 | Regional HQ Water project | 5,000,000,000.00 | - |
| | | 3340 | Masasi -Nachingea Water Project | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 3341 | Same- Mwanga- Korogwe Water Project | 12,000,000,000.00 | 25,000,000,000.00 |
| | | 3342 | L Victoria-NZG-Igunga-TBR-SikongeProject | 1,000,000,000.00 | 20,000,000,000.00 |
| | | 3403 | Lake Victoria Shy/Kahama Water Supply | 11,000,000,000.00 | - |
| | | 3435 | Water Quality and Ecosystem Management | 2,500,000,000.00 | 6,427,360,000.00 |
| | | 3436 | Capacity Development for MOWI Agencies | 5,887,000,000.00 | 5,900,000,000.00 |
| | | 3437 | DSM Water Supply and Sanitation Project | 22,500,000,000.00 | 40,000,000,000.00 |
| | | 3438 | Kidunda Dam Construction Project | 10,000,000,000.00 | - |
| | | 3439 | Kimbiji and Mpera Water Project | 5,000,000,000.00 | 5,000,000,000.00 |
| | | 6275 | Management Support to Urban Utilities | 8,700,000,000.00 | 490,000,000.00 |

| VOTE | VOTE NAME | PROJECTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6276 | Management Support to LGAs | 16,314,000,000.00 | 14,410,000,000.00 |
| | | 6545 | Development & Mgt of Water Resouces | 25,000,000,000.00 | 27,180,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 408,617,643,000.00 | 214,989,105,000.00 |
| 50 | MINISTRY OF FINANCE AND PLANNING | 6251 | PFMRP | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 |
| | | | Public Finance Management Programme | - | - |
| | | | Public Finance Management Reform Program | 300,000,000.00 | 1,510,500,000.00 |
| | | | Public Finance Mgt Reform Progamme | 500,000,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| | | | Public Finance Mgt Reform Programme | 1,200,000,000.00 | 5,060,000,000.00 |
| | | 6321 | Construction of IAA Modern Library Proje | - | - |
| | | 6326 | Construction & Reh.of Treasury Building | - | - |
| | | 6369 | Rehabilitation of ESAAMLG HQ Building | 1,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 3,500,000,000.00 | 8,070,500,000.00 |
| 51 | MINISTRY OF HOME AFFAIRS | 6258 | Support to Refugee Areas | - | - |
| | | 6501 | National Identity Card | 20,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 20,000,000,000.00 | - |
| 52 | MINISTRY OF HEALTH, COMMUNITY DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN - HEALTH | 2204 | Human Resource Development | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 2208 | National Institute for Medical Research | 800,000,000.00 | - |
| | | 5406 | Control Of Communicable Diseases | 36,500,000,000.00 | 104,304,328,000.00 |
| | | 5409 | Support to Maternal Mortality Reduction | 8,600,000,000.00 | - |
| | | 5411 | Strenghening of Referral Hospitals | 8,000,000,000.00 | 2,952,890,000.00 |
| | | | Strengthening of Refferal Hospitals | 236,000,000,000.00 | 409,940,000.00 |
| | | 5412 | Ocean Road Cancer Institute | 14,500,000,000.00 | - |
| | | 5416 | Health Plans and Management | - | 1,369,619,000.00 |
| | | 5422 | Mbeya Referral Hospital | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 5423 | Mtwara Referral Hospital | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 5424 | Kibong'oto Infectious Disease Hospital | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 5425 | Mirembe Mental Health Hospital | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 5426 | Bugando Medical Centre | 500,000,000.00 | - |
| | | 5427 | Kilimanjaro Christian Medical Centre | 500,000,000.00 | - |
| | | 5451 | Support to Social Welfare Services | - | - |
| | | 5485 | Health Plans and Management | - | - |
| | | 5486 | Health Sector Programme Support | - | 113,865,692,000.00 |
| | | 5487 | Muhimbili National Hospital | 18,000,000,000.00 | - |
| | | 5491 | Muhimbili Orthopaedic Institute | 3,800,000,000.00 | - |
| | | 5492 | HIV/AIDS Control Programme | - | 205,885,099,000.00 |
| | | 5496 | Tanzania Food and Nutrition Center | 100,000,000.00 | - |
| | | 5498 | Support to TB/Leprosy Control Programme | - | 20,718,384,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 336,300,000,000.00 | 449,505,952,000.00 |
| 53 | MINISTRY OF HEALTH - COMMUNITY DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN | 4312 | Education Sector Development Programme | - | - |
| | | 4950 | Womens Economic Empowerment | - | - |
| | | 5414 | Young Child Survival and Dev.Prog | - | 208,900,000.00 |
| | | 5415 | Child Protection and Participation Prog | - | - |
| | | 5451 | Support to Social Welfare Services | 1,168,000,000.00 | 52,773,891.00 |
| | | 6229 | CDTI Tengeru | - | - |
| | | | Rehabilitation of Folk Dev.College(FDCs) | - | - |
| | | 6259 | Resource Planning For Gender Programme | - | - |
| | | 6290 | Programming and Data Processing Project | - | - |
| | | 6330 | Community Developm Training Institutions | 832,000,000.00 | - |
| | | 6550 | UNDP Support Project | - | 344,604,109.00 |
| | TOTALVOTE | | | 2,000,000,000.00 | 606,278,000.00 |
| 55 | COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS & GOOD GOVERNANCE | 6550 | UNDP Support Programme | - | 2,272,796,000.00 |
| | | 6579 | Inspection of Juvenile Dentention Facili | - | - |
| | TOTALVOTE | | | - | 2,272,796,000.00 |
| 56 | PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION | 3280 | Rural Water Supply and Sanitation | - | 756,550,000.00 |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES | | | | |
| | | 4169 | Support-Road Maintanance &Rehabilitation | 27,526,400,000.00 | 42,212,194,000.00 |
| | | 4170 | The Roads Funds | 247,737,600,000.00 | - |
| | | 4285 | Dsm Rapid Transport | 31,000,000,000.00 | - |
| | | 4303 | Hombolo LGTI | - | - |
| | | 4305 | Policy Advocacy and Analysis | - | 270,396,000.00 |
| | | 4307 | Kibaha Education Centre | - | - |
| | | 4313 | Primary Education Development Programe | - | 13,193,860,000.00 |
| | | 4390 | Secondary Education Development Programm | - | 1,111,400,000.00 |
| | | 4486 | Agriculture Sector Development Program | - | 500,000,000.00 |
| | | 5308 | Decentralising Climate Financing Project | - | 1,007,210,000.00 |
| | | 5420 | Basic Health Service | - | 15,000,000,000.00 |
| | | 5421 | Health Sector Programme Support | - | 1,231,680,000.00 |
| | | | Health Sector Programme Support | - | - |
| | | 5493 | Global Funds HIV | - | 847,687,000.00 |
| | | 5495 | Prevantion of Transmission | - | 101,400,000.00 |
| | | | Prevention of Transmission of HIV/AIDS | - | - |
| | | 6250 | Local government reform programme | 1,000,000,000.00 | 2,171,808,000.00 |
| | | 6251 | PFMRP III | 800,000,000.00 | 1,500,000,000.00 |
| | | 6380 | Rehab.of PMO-RALG's Build.office-DOM | 500,910,000.00 | - |
| | | 6403 | Tanzania Strategic Cities | - | 5,955,779,000.00 |
| | | | Tanzania Strategic Cities Programme | - | - |
| | | 6405 | Urban local Government Strenthening Prog | - | 17,488,784,000.00 |
| | | 6580 | DSM Metropolitan Dev.Project | - | 5,343,030,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 308,564,910,000.00 | 108,691,778,000.00 |
| 57 | MINISTRY OF DEFENCE AND NATIONAL SERVICE | 6103 | Defence Scheme | 15,818,000,000.00 | - |
| | | | Defence Schemes | 189,182,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 205,000,000,000.00 | - |
| 58 | MINISTRY OF ENERGY AND MINERALS | 1118 | Regional Mining Offices Development | 1,500,000,000.00 | - |
| | | 1119 | Minerals | 3,200,000,000.00 | 5,700,000,000.00 |
| | | 3102 | New And Renewable Energies | 21,014,253,000.00 | 14,500,000,000.00 |
| | | 3110 | TZ-Energy Dev and access Project | - | 18,094,327,000.00 |
| | | 3113 | Rural Energy Fund | 469,090,426,000.00 | 30,000,000,000.00 |
| | | 3115 | Petroleum Sub-Sector Development Project | 71,500,000,000.00 | 570,000,000.00 |
| | | 3121 | 132 KV Makambako-Songea | 3,000,000,000.00 | 8,000,000,000.00 |
| | | 3147 | Transfer to TANESCO | - | 12,209,000,000.00 |
| | | 3152 | TZ Extractive Industr.Transp Iniatiative | - | 1,383,000,000.00 |
| | | 3156 | Energ. Rural TZ-Power supp-Ngara,Brm, Mp | - | - |
| | | 3157 | Iringa-Singida-Shinyanga (BPIT) | - | 1,060,000,000.00 |
| | | 3160 | Kiwira Coal Mines and 200MW Power Plant | 10,000,000,000.00 | - |
| | | 3162 | Constrn of Natural Gas pipeline-Mtwara-D | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 3163 | 240MW Kinyerezi Gas Fired Plant | - | 10,000,000,000.00 |
| | | 3164 | 150 MW Natur. Gas Fired Plant Kinyerezi | 90,000,000,000.00 | - |
| | | 3166 | North west grid Extension Project | 24,200,000,000.00 | 15,400,000,000.00 |
| | | 3169 | Rusumo Falls Hydroelectric | - | 7,653,000,000.00 |
| | | 3170 | North-East Grid (Dar-Tanga-Arusha 400kw | 67,800,000,000.00 | 24,000,000,000.00 |
| | | 3191 | Electricity V Project | - | - |
| | | 6298 | Institutional Support | - | 26,758,000,000.00 |
| | TOTALVOTE | | | 763,304,679,000.00 | 175,327,327,000.00 |
| 60 | TRADE AND INVESTMENT | 4486 | Agriculture Sector Development Program | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 6260 | Institution Support | 4,350,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 6,350,000,000.00 | - |
| 61 | ELECTORAL COMMISSION | 6297 | Demoratic Empowerment Project | - | - |
| | | 6583 | Electoral Support Programme | 10,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 10,000,000,000.00 | - |
| 62 | MINISTRY OF WORKS, TRANSPORT AND COMMUNICATION - TRANSPORT | 4156 | Construction of Kigoma Airport | - | - |
| | | 4158 | Construction of Mpanda Airport | - | - |
| | | 4159 | Construction of Tabora Airport | - | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJECTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 4206 | Construction of Songwe Airport | - | - |
| | | 4209 | Construction of Mwanza Airport | - | - |
| | | 4211 | Rail Rehab & SBUs Improvement for TAZARA | 26,000,000,000.00 | - |
| | | 4213 | The Railway Infrustructure Fund | 218,569,000,000.00 | - |
| | | 4215 | Rail Rehabilitation-Branch Lines-RAHCO | - | - |
| | | 4216 | Rail Rehabilitation-Main line RAHCO | 1,000,000,000.00 | 250,000,000,000.00 |
| | | 4217 | Tabora - Kigoma, Isaka - MZ Rail Project | - | - |
| | | 4218 | Mtwara - M/bay, Liganga & Mchuchuma Rail | 2,000,000,000.00 | - |
| | | 4219 | Dsm City Commuter Train | 2,000,000,000.00 | - |
| | | | DSM City Commuter Train Project | - | - |
| | | 4220 | Construction of Mtwara Airport | - | - |
| | | 4221 | Construction of Sumbawanga Airport | - | - |
| | | 4222 | Construction of Shinyanga Airport | - | - |
| | | 4223 | Tanga-Arusha-Musoma Railway Project | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 4224 | Rehabilitation of Kilimanjaro Int. Airpo | - | - |
| | | 4226 | Development of Regional Airports | - | - |
| | | 4227 | Modernization of Dar es Salaam Port | 187,123,000,000.00 | - |
| | | 4228 | Improvement of Tanga Port | 12,604,000,000.00 | - |
| | | 4229 | Extension of Mtwara Port | 87,044,000,000.00 | - |
| | | 4230 | Improvement of Lake Victoria Ports | 6,295,000,000.00 | - |
| | | 4231 | Improvement of Lake Tanganyika Ports | 18,500,000,000.00 | - |
| | | 4232 | Improvement of Lake Nyasa Ports | 15,290,000,000.00 | - |
| | | 4233 | Ports Cargo Handling Equipment | 160,425,000,000.00 | - |
| | | 4281 | Construction of New Standard Gauge | 900,000,000,000.00 | - |
| | | 4286 | Construction of Msalato Airport | - | - |
| | | 4287 | Construction of Bukoba Airport | - | - |
| | | 4289 | Construction of Terminai III JNIA | - | - |
| | | 4290 | TMA Radar, Equipment and Infrastructure | 6,200,000,000.00 | - |
| | | 4291 | Government Aircrafts Maintenance | 10,000,000,000.00 | - |
| | | 4293 | Rail Equipment and Tracks Maintenance | 30,800,000,000.00 | - |
| | | 4294 | Acquisition of New Aircraft - ATCL | 500,000,000,000.00 | - |
| | | 4295 | Procurement and Rehab. of Marine Vessels | 24,496,000,000.00 | - |
| | | 6267 | Institutional Support | 8,000,000,000.00 | 285,183,000.00 |
| | | 6377 | Construction and Rehab. of NIT Buildings | 10,300,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 2,227,646,000,000.00 | 250,285,183,000.00 |
| 64 | FISHERIES SECTOR | 4486 | Agriculture Sector Development Program | 1,225,000,000.00 | - |
| | | 4701 | 0 | 775,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 2,000,000,000.00 | - |
| 65 | PRIME MINISTER'S OFFICE - LABOUR, YOUTH DEVELOPMENT, EMPLOYMENT AND DISSABILITIES | 4945 | Youth Development | 1,000,000,000.00 | - |
| | | 6218 | ILO Support Project | - | 1,400,000,000.00 |
| | | 6230 | Study and Expert Fund | - | - |
| | | 6581 | Support National Skills Development Prog | 15,000,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 16,000,000,000.00 | 1,400,000,000.00 |
| 66 | PLANNING COMMISSION | 4940 | Pro-Poor Growth | 579,000,000.00 | - |
| | | 4941 | Coordination of Develop Budgets and Proj | 3,100,000,000.00 | - |
| | | 6251 | Public Finance Management Reform Program | - | - |
| | | 6526 | Population Planning Project | 796,800,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 4,475,800,000.00 | - |
| 67 | PUBLIC SERVICE RECRUITMENT SECRETARIAT | 6225 | Enhancement of e-recruitment system | 750,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 750,000,000.00 | - |
| 68 | MINISTRY OF WORKS, TRANSPORT AND COMMUNICATION - COMMUNICATION | 4225 | Regional Communications infrastr. Progr. | - | - |
| | | 4283 | The National ICT Backbone Infrastructur | 10,000,000,000.00 | - |
| | | 4285 | New post Codes and addressing System | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 4383 | Communication Scient and Tech Project | 200,000,000.00 | - |
| | | 4384 | Dar-es-salaam Institute of Technology | - | - |
| | | 6226 | E-Waste Mgt & ICT Hardware Assembly | 800,000,000.00 | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Cent | | |
| | TOTALVOTE | | | 14,000,000,000.00 | - |
| 69 | MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM | 4629 | Support to Forest (National Programme) | - | - |
| | | 4631 | Enh Forest nature Rsrv ntwk for B C TZ | - | - |
| | | 4646 | Participatory forest mgt,REDD&CCIP | - | 3,000,000,000.00 |
| | | 4647 | Private Plantation and Value Chain in TZ | - | 1,700,860,000.00 |
| | | 4648 | Capacity Building in Forestry and Beekee | 200,000,000.00 | - |
| | | 4649 | Natural Resources Management - LED | - | 2,690,580,000.00 |
| | | 4809 | Wetlands Mgt and Sustainable Development | - | 2,633,457,365.00 |
| | | 4810 | Capacity Buliding in Game Reserves | 34,103,284,000.00 | - |
| | | 4811 | Sustainable Mgt of Natural Resources | - | 5,975,102,635.00 |
| | | 4812 | Surpt to Combating WL CRM and advn consv | - | - |
| | | 5202 | Construction of Theme Park in DSM City | 250,000,000.00 | - |
| | | 5203 | Resilient NR For Tourism and Growth | - | 1,000,000,000.00 |
| | | 6251 | Public Sector Managt. Reform Prog.III | - | - |
| | | 6367 | Utalii House Phase II Project | 250,000,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 34,803,284,000.00 | 17,000,000,000.00 |
| 91 | ANTI DRUG COMMISSION | 5497 | Implementation of HIV/AIDS against IDU's | - | - |
| | TOTALVOTE | | | - | - |
| 92 | TANZANIA COMMISSION FOR AIDS | 5488 | AIDS Trust Fund | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 5494 | Mainstreaming HIV/AIDS in National Dev. | - | 132,922,955.00 |
| | | 5495 | Global Fund HIV/AIDS Prevention Project | - | 322,420,045.00 |
| | | 5499 | Support to NMSF Grant for Tanzania | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 3,000,000,000.00 | 455,343,000.00 |
| 93 | IMMIGRATION DEPARTMENT | 6301 | Construction of Immigration Reg. Offices | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 6339 | Rehabilitation of Government Houses | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 4,000,000,000.00 | - |
| 96 | MINISTRY OF INFORMATION, CULTURE, ARTS AND SPORTS | 4279 | Expansion of TBC Coverage | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 4353 | Rehabilitat. of Bagamoyo College of Art | - | - |
| | | 6293 | Liberation Heritage Program | 1,500,000,000.00 | - |
| | | 6355 | Construction of Open Air Theatre | - | - |
| | | 6523 | National Sports Complex | 1,820,000,000.00 | - |
| | | 6567 | Public Information | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 6,320,000,000.00 | - |
| 98 | MINISTRY OF WORKS, TRANSPORT AND COMMUNICATION - WORKS | 4108 | DSM-Chalinze-Morogoro Express Way | 12,771,000,000.00 | - |
| | | 4109 | Wazo Hill -Bagamoyo Msata Road | 25,912,000,000.00 | - |
| | | 4110 | Usagara - Geita -Bwanga - Kyamyorwa Road | 35,379,000,000.00 | - |
| | | 4112 | Kigoma - Kidahwe - Uvinza -Kaliua-Tabora | 27,858,000,000.00 | 20,000,000,000.00 |
| | | 4115 | Marangu-Tarakea-Rongai-Kamwanga/Sanya | 18,932,696,000.00 | 15,000,000,000.00 |
| | | 4117 | Nangurukuru - Mbwemkulu Road | - | - |
| | | 4118 | Dodoma - Manyoni Road | 1,036,000,000.00 | - |
| | | 4122 | Nelson Mandela(Port Access) Road | 308,000,000.00 | - |
| | | 4123 | Dumila - Kilosa Road | 5,207,000,000.00 | - |
| | | 4124 | Sumbawanga - Matai-Kasanga Port | 20,957,000,000.00 | - |
| | | 4125 | Ferry, Ramps and Vending Machines | 1,361,000,000.00 | - |
| | | 4126 | Construction of Brigdes | 26,301,000,000.00 | 10,000,000,000.00 |
| | | 4127 | New Bagamoyo Road (Kawawa Jct - Tegeta) | 318,000,000.00 | - |
| | | 4128 | Kyaka - Bugene - Kasulo Road | 7,830,000,000.00 | - |
| | | 4129 | Isaka - Lusahunga Rehabilitation | 18,768,000,000.00 | - |
| | | 4130 | Manyoni - Itigi - Tabora Road | 30,783,000,000.00 | 15,081,250,000.00 |
| | | 4131 | Korogwe-Handeni road | 4,500,000,000.00 | - |
| | | 4132 | Regional Roads Rehabilitation | 30,000,000,000.00 | - |
| | | 4133 | Mwanza - Shinyanga Boarder Road (Rehab) | 342,000,000.00 | - |
| | | 4134 | Handeni - Mkata Road | 1,458,000,000.00 | - |
| | | 4135 | Mwandiga - Manyovu Road | - | - |
| | | 4136 | Road Safety Activities | 2,193,840,000.00 | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 4137 | Unity Bridges | - | - |
| | | 4138 | De-Congestion of Dsm Road | 12,409,000,000.00 | - |
| | | 4139 | Procurement of Ferries | 6,683,000,000.00 | - |
| | | 4143 | Ndundu - Somanga Road | 626,000,000.00 | - |
| | | 4144 | Rehabilitation of Ferries | 1,956,000,000.00 | - |
| | | 4147 | Kidatu - Ifakara Road | 433,000,000.00 | 19,823,867,000.00 |
| | | 4148 | Tabora-Ipole - Koga - Mpanda Road | 7,729,000,000.00 | 61,544,938,000.00 |
| | | 4149 | Makutano-Nata-Mugumu/Loliondo-Mto wa Mbu | 17,397,000,000.00 | - |
| | | 4150 | Ibanda - Itungi Port | 13,465,000,000.00 | - |
| | | 4151 | Tanga - Horohoro Road | 865,000,000.00 | - |
| | | 4152 | Nzega - Tabora Road | 23,736,000,000.00 | - |
| | | 4154 | Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi Road | 31,000,000,000.00 | - |
| | | 4155 | Nyanguge - Musoma / Kisesa Bypass | 30,332,000,000.00 | - |
| | | 4156 | Construction of Kigoma Airport | 1,050,000,000.00 | 6,200,000,000.00 |
| | | 4158 | Construction of Mpanda Airport | 700,000,000.00 | - |
| | | 4159 | Construction of Tabora Airport | 2,450,000,000.00 | 8,600,000,000.00 |
| | | 4160 | Magole - Mziha Road | 8,704,000,000.00 | - |
| | | 4161 | Dsm Road Flyovers and Approaches | 1,890,000,000.00 | 45,000,000,000.00 |
| | | 4162 | Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi Road | 25,188,000,000.00 | - |
| | | 4163 | IPole - Rungwa Road | 435,000,000.00 | - |
| | | 4164 | Kidahwe-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi Road | 19,284,000,000.00 | - |
| | | 4165 | Mafia AirportAccess Road | 1,006,000,000.00 | - |
| | | 4166 | Dodoma University Road | 1,852,000,000.00 | - |
| | | 4167 | Const. of Nyerere (Kigamboni) Bridge | 2,231,000,000.00 | - |
| | | 4170 | The Roads Fund | 642,284,000,000.00 | - |
| | | 4172 | Providing Lane Enhancement | 359,000,000.00 | - |
| | | 4173 | Widening of Pugu Road (JNIA-Pugu) | 122,000,000.00 | - |
| | | 4174 | Widening of Kimara - Kibaha Road | 122,000,000.00 | - |
| | | 4175 | Upgrading of Kisarawe - Mlandizi | 100,000,000.00 | - |
| | | 4176 | Widening of Bandari Road | - | - |
| | | 4178 | Upgrading of Pugu - Bunju Road | 436,000,000.00 | - |
| | | 4179 | Construction of Weighbridge Dar Port | 218,000,000.00 | - |
| | | 4180 | Tunduma - Sumbawanga Road | 5,215,000,000.00 | - |
| | | 4181 | Kagoma - Lusahunga Road | 10,826,000,000.00 | - |
| | | 4182 | Arusha - Namanga Road | 1,218,000,000.00 | - |
| | | 4183 | Singida - Babati - Minjingu Road | 2,855,000,000.00 | - |
| | | 4185 | Dsm - Mbagala (Kilwa Road) | 2,132,910,000.00 | 10,000,000,000.00 |
| | | 4186 | Msimba- Ruaha- Mbuyuni - Mafinga(TANZAM) | 21,749,000,000.00 | 83,023,840,000.00 |
| | | 4187 | Korogwe -Mkumbara-Same Road | 535,000,000.00 | - |
| | | 4188 | Mbeya- Makongolosi Road | 22,038,000,000.00 | - |
| | | 4189 | Chalinze - Segera - Tanga Road | 3,000,000,000.00 | - |
| | | 4190 | Itoni- Ludewa Manda | 8,465,000,000.00 | - |
| | | 4192 | Ruvu Bridge | - | - |
| | | 4193 | Handeni-Kibereshi-Kibaya-Singida Road | 500,000,000.00 | - |
| | | 4195 | Dodoma - Iringa Road | 4,784,000,000.00 | 8,668,010,000.00 |
| | | 4196 | Dodoma - Babati Road | 11,739,000,000.00 | 104,985,137,000.00 |
| | | 4197 | Masasi - Songea - Mbambabay Road | 13,429,394,000.00 | 51,086,750,000.00 |
| | | 4198 | Access Road to Uongozi Institute | 50,000,000.00 | - |
| | | 4206 | Construction of Songwe Airport | 1,530,000,000.00 | - |
| | | 4209 | Construction of Mwanza Airport | 18,580,000,000.00 | 5,000,000,000.00 |
| | | 4210 | Construction of Arusha Airport | 700,000,000.00 | - |
| | | 4220 | Construction of Mtwara Airport | 4,550,000,000.00 | - |
| | | 4221 | Construction of Sumbawanga Airport | 5,200,000,000.00 | 13,200,000,000.00 |
| | | 4222 | Construction of Shinyanga Airport | 1,800,000,000.00 | 13,800,000,000.00 |
| | | 4224 | CONSTRUCTION OF KILIMANJARO INTERNATIONA | 5,000,000,000.00 | 27,568,640,000.00 |
| | | 4226 | DEVELOPMENT OF REGIONAL AIRPORTS | 17,390,000,000.00 | - |
| | | 4285 | Bus Rapid Transport | 100,000,000.00 | 25,000,000,000.00 |
| | | 4286 | Construction of Msalato Airport | 3,500,000,000.00 | 2,000,000,000.00 |
| | | 4287 | Construction of Bukoba Airport | 2,550,000,000.00 | - |
| | | 4289 | CONSTRUCTION OF TERMINAL III JNIA | 35,000,000,000.00 | - |
| | | 6221 | Inst. Support to Safety and Environment | 151,500,000.00 | - |
| | | 6267 | Institutional Support | 250,000,000.00 | - |
| | | 6327 | Construction of Government Houses | 12,450,000,000.00 | - |
| | | 6383 | Constrction of Tanroads Headquarters | 5,280,000,000.00 | - |
| | | 6571 | EMA Implementation Support Programme | 154,660,000.00 | - |
| | TOTALVOTE | | | 1,350,000,000,000.00 | 545,582,432,000.00 |
| 99 | MINISTRY OF AGRICUTURE - LIVESTOCK DEVELOPMENT | 4486 | Agriculture Sector Development Program | 4,000,000,000.00 | - |
| | | 4495 | EA Agricultural Productivity Project | - | - |
| | | 5492 | SWIOFISH | - | - |

| VOTE | VOTE NAME | PROJE CTCODE | PROJECT DESCRIPTION | LOCAL ESTIMATES | FOREIGN ESTIMATES |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 6501 | SWIOFISH | - | - |
| | TOTALVOTE | | | 4,000,000,000.00 | - |
| | | | | 7,962,777,000,000.00 | 2,670,865,382,091.00 |

**KIAMBATISHO NA. III**

## RATIBA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA, 2017/18

| NA | SHUGHULI | MUDA | MHUSIKA | MATUMIZI YA TAARIFA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 | Julai 2017 – Juni 2018 | Wizara zote na Sekta Binafsi | |
| 2. | Kuwasilisha Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Rasilimali Fedha | Juni 2017 | Wizara zote | Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Mipango |
| 3. | Uchambuzi wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Rasilimali Fedha | Juni 2017 | Tume ya Mipango | Wizara ya Fedha na Mipango, na Wizara Husika |
| 4. | Kuwasilisha Taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 | Oktoba, 2017 Januari, 2018 Aprili, 2018 Julai, 2018 | Wizara zote | Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha na Mipango |
| 5. | Kuchambua taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinazowasilishwa na Wizara zote (MDAs) | Oktoba, 2017 Januari, 2018 Aprili, 2018 Julai, 2018 | Tume ya Mipango | Kamati ya Uongozi ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo |
| 6. | Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo | Oktoba, 2017 Januari, 2018 Aprili, 2018 Julai, 2018 | Tume ya Mipango | Kamati ya Uongozi ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo |